

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tano – Tarehe 15 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe.Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 69

Hitaji la Ambulance Manyovu

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA (K.n.y. MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA) aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka *ambulance* katika vituo vya afya jimbo la Manyovu ambako maisha ya akina mama yameathiria na vifo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jimbo la Manyovu lina hospitali moja inayomilikiwa na Taasisi ya dini, vituo vinne vya afya ambavyo viwili kati ya hivyo vinamilikiwa na Serikali.

Kati ya vituo viwili vya afya vinavyomilikiwa na Serikali jimboni Manyovu, Kituo cha Afya cha Muyama kina gari la wagonjwa lilitolewa na UNFPA lenye namba za usajili DFP 1382 L/C, Kituo cha Afya cha Janda hakina gari; kinategemea gari kutoka Muyama na Vituo viwili vya binafsi vina magari ya kuhudumia wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua upungufu wa huduma za usafiri uliopo, Serikali imepeleka gari la kubebia wagonjwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu katika mwezi wa Aprili, 2011 lenye namba za usajili SM 9063. Gari hilo lilipokelewa na Halmashauri tarehe 22/4/2011 na kukubidhiwa kituo cha afya cha Janda tarehe 13/5/2011. Hatua hii imefanya vituo vyote viwili vya afya vinavyomilikiwa na Serikali kuwa na magari ya kubebia wagonjwa.

MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA: Ahsante sana kwa majibu mazuri. Nashukuru sana kwamba sasa tatizo hilo limeshughulikiwa ipasavyo. Lakini nina swalii moja la nyongeza. Katika jimbo la Kalenga tuna hospitali teule inaitwa ya Ipamba, pale Tosamaganga ina tatizo linalofanana na hilo la kukosekana kwa gari la *ambulance*. Naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kushughulikia tatizo hili? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, hiyo hospitali teule alioitaja sikusikia hilo jina. Aaah Tosamaganga ni Iringa huko.

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho haya magari tuliyogawa yalikuwa ni magari 42, 43. Hiki kituo anachokisema kama ni *designated hospital* kwa maana ya hospitali teule wala hatuna tatiozo kwa sababu inakuwa ni utaratibu ambao umekubaliwa na Serikali. Ninayo orodha ndefu hapa nitamwomba tu Mheshimiwa Daktari wakati tutakapomaliza hapa nitakwenda kukaa naye pale nita-*consult* hii orodha yangu hapa. Kwa sababu sasa sipati nafasi ya kuiangalia hapa. Halafu nitajua kwamba tunafanya nini.

Lakini nataka tu niseme kwamba tunajitahidi kwa kadri fedha zitakavyoruhusu kwa ajili ya vituo vingine pamoja na maeneo mengine ambayo ni muhimu kwa ajili ya kupata hiyo huduma.

MHE. SAID M. MTANDA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa wananchi wa Kata ya Milola kwa kushirikiana na wafadhili wamejenga kituo kikubwa sana cha afya na kwa kuwa Jimbo la Mchinga linakabiliwa na tatiozo sugu kabisa la miundombinu. Je, Serikali iko tayari kuwapatatia *ambulance* wananchi wale wa Milola ili waweze kupata utaratibu huu wa matibabu hasa kuzingatia umbali kutoka Milola kwenda Lindi Mjini ambako ndiko kuna hospitali ya Mkoa umbali ni mkubwa sana?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, unakujua kote maana umetembea, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri kwenye hiyo orodha ambayo ninayo hapa kwa sababu hospitali sisi hatupeleki *ambulance* kwenye kituo cha afya au kwenye zahanati tunapeleka kwenye Halmashauri ili iweze kuhudumiwa. Katika hii orodha niliyonayo Halmashauri ya Mji wa Lindi inaonekana kwamba imepata *ambulance* moja. Sasa inawezekana kabisa hapo sipo anapozungumza Mheshimiwa Mtanda kwa sababu nafahamu katika Jimbo lake aliko. Nitaomba pia kama nilivyosema hapa, nikitoka hapa nitakaa naye pale tuweze ku-*consult* hii orodha yangu halafu tutajua kwamba tunamsaidiaje kwenye hili eneo.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo yaliyopo katika Halmashauri ya Kasulu yanafanana kabisa na matatizo ambayo yako katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuhusu wagonjwa Na kwa kuwa katika magari 43 aliyoyasema Mheshimiwa Naibu Waziri, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya nayo ilipangiwa gari la kubebea wagonjwa na wakapewa na namba na wakachangia kwa maana ya malipo madogo madogo ya awali. Lakini huu ni mwezi wa tatu hiyo gari haijaenda Chunya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambiaje wananchi wa Chunya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama takwimu zake anazozileta hapa na kama anajua mpaka na namba ya gari hii itanirahisia tu Mheshimiwa Spika. Mimi nataka nimwahidi kabisa kama na namba ya gari kama limekwenda kwingine nitajua ni kwa nini limekwenda huko . Kwa hiyo, nitachekei na nitampa taarifa kamili.

Na. 70

Uhamisho wa Watumishi wanaohamia Wilaya mpya ya Bahi

MHE. OMARY A. BADWEL aliuliza:-

Kwa sababu Wilaya ya Bahi ni mpya inalazimu watumishi kuhamia Wilaya hii kutoka Dodoma Mjini:-

- (a) Je, Serikali itakuwa Tayari kuwalipa fedha zao za uhamisho kuptitia Bajeti ya 2009/2010 wakati watumishi hao wakiendelea kuhamia Bahi?
- (b) Kama Serikali haikutenga fedha zao katika Bajeti ya 2009/2010 itakuwa tayari kutenga fedha hizo katika Bajeti ya 2010/2011?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Omari Ahmed Badwe, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mpango uliopo wa kuhamia Makao Makuu ya Bahi, Halmashauri imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, nyumba ya kuishi Mkurugenzi na nyumba tatu za Wakuu wa Idara ambazo zimejengwa kupitia Bajeti ya mwaka 2010/2011. Jitihada hizi zimewesha watumishi kuhamia Bahi wakiwemo watumishi 15 wa Idara ya Elimu ambao wamelipwa fedha zao za uhamisho kwa kiasi cha shilingi milioni 24,990,000.

Idara ya Uhasibu hajahamia Bahi kutokana na kutokuwepo kwa mfumo unaouunganisha Halmashauri hiyo na Wizara ya Fedha na Uchumi (*Integrated Financial Management System and Epicor System*). Katika mwaka mwaka 2011/2012 Halmashauri inatarajia kujenga nyumba 5 za watumishi ambapo shilingi milioni 350 zimetengwa kwa kusudi hilo.

Mipango mingine ni upimaji wa viwanja 517 katika mji wa Bahi na watumishi wa Halmashauri hiyo wamepewa kipaumbele ili kujenga nyumba za kuishi. Aidha, watumishi watakaohamia katika Makao Makuu ya Bahi watalipwa fedha za uhamisho kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo kwa awamu na kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri inatarajia kuomba maombi maalum katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 fedha kwa ajili ya uhamisho wa watumishi watakaohamia Bahi katika awamu ya pili. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI itaendelea kuwasiliaiana na Wizara ya Fedha na Uchumi ili kuwezesha upatikanaji wa fedha hizo. Aidha, Halmashauri inashauriwa kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kuweka vipaumbele vya utekelezaji wa miradi itakayochochea ukuaji wa uchumi wa Wilaya hii mpya.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amefahamu mapema kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Bahi inatarajia kuomba fedha zilizobaki kwa ajili ya kuwalipa watumishi katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 lakini na kwa kuwa fedha hizo tumeziomba katika miaka mitatu mfululizo uliyopita na hatujapewa.

Je, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametambua hili mapema na amesema hapa ndani ya Bunge sasa atanihakikishia mimi kupitia Bunge hili kwamba jambo hili analijua na atahakikisha fedha katika awamu hiyo inayokuja ya Bajeti tutapewa ili watumishi hawa walipwe mafao yao ya kuhamia Bahi?

Pili Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watumishi hawa wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi pamoja na kwamba hajalipwa fedha zao za uhamisho lakini kwa uzalendo mkubwa wameshaanza kuhamia Bahi pamoja na matatizo wanayokumbana nayo, lakini nilishamwandikia Mheshimiwa Waziri barua juu ya tatizo kubwa la maji ya Ofisi ile ya Halmashauri ambayo wanahamia hawa watumishi.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari sasa kutusaidia zile fedha tulizoomba kwa dharura ili tuweze kuweka maji katika Ofisi ile ya Halmashauri? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hizi anazosema Mheshimiwa Badwe ni kweli. Ukiacha Idara ya Elimu ambayo nimeisemea hapa ambayo imelipwa na watumishi wake wameweza kwanza kwenda kule, hao wengine hawajapata kwa sababu waliiwekwa katika maombi maalum.

Jana nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji, nimemwita Ofisi ni nikamwambia tunafanya nini katika hili na wote kwa pamoja tumeahidi kwamba tutafuatilia kwa maana ya kupitia Wizara ya Fedha ili tuone kwamba hela nytingine zilizobakia zinapatikana kwa sababu wameweka katika

maombi maalum. Inakwenda kwenye *range* ya shilingi karibu milioni 500 na kitu hivi kwa maana ya kuwalipa. Hilo la kwanza.

Lakini la pili nimekwenda mimi Bahi ni kweli matatizo ya maji anayosema katika mji wa Bahi ni kikwazo kikubwa sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Badwel anasema kweli kabisa hapa anachokisema hapa. Sasa nilipokwenda pale mimi tulichoshauri cha kwanza, kwanza kuna ujenzi unoaoendelea pale mkubwa sana na kwa hiyo tumewaomba wananchi waone uwezekano wa kuvuna maji ili kwa maana kipindi hiki cha mpito waweze kufaidika.

Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji hapa miji yote hii sasa tumeweka mpango maalum ili kuhakikisha kwamba tunaondoka na tatizo hili la maji. Matumaini ni kwamba Bahi nayo itakuwa katika mpango huo na tutaisaidia kwa misingi hiyo. (*Makofî*)

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Naomba tu kujua kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Bahi ilitokana na Wilaya ya zamani ya Dodoma Vijijini ambayo ilizaa Bahi na Chamwino. Napenda kujua Serikali inasemaje juu ya uhamisho wa watumishi wa Wilaya ya Chamwino kutoka Mjini kwenda Makao Makuu ya Wilaya ya Chamwino?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, haya maswali ya Wilaya hizi mpya hata kama utaendelea kuwaruhusu wengine majibu yake yatakuwa ni haya haya niliyoyatoa hapa. Wote Chato, Bahi, Siha wale wanaotoka Misenyi, wanaotoka Tunduru kule wote wale wa Wilaya mpya wote wakikuuliza swali hapa Uyui watakuuliza swali hilo hilo.

Ninachotaka kusema hapa ni kweli wanachosema Waheshimiwa Wabunge kwamba hawa wananchi watumishi ili sasa waweze kuondoka katika zile Halmashauri mpya kule Makao Makuu ambako yamejengwa wanatakiwa sasa walipwe hizi haki zao. Sasa hatutaki tuseme hapa kwamba kwa vile watumishi hawajalipwa haki zao kwa hiyo hawaendi kule.

Tumewaaagiza kwa mfano Uyui tumewaaambia, hawa anaowasema Mheshimiwa Chibulunje tumekwenda sisi Chamwino pale wanakaa hapa mjini wanakwenda kule, wanarudi jioni unawakuta wote wapo hapa, wote ukiwaliliza unawakuta wote wako hapa. Maelekezo ya Serikali ni kwamba kwa kutumia hata zile fedha za ndani tulizo nazo pale ndani. Kwa maana *own source* tuhakikisha kwamba watumishi wetu wanakwenda kule katika Halmashauri, katika Makao Makuu ambapo yamejengwa. Tusipofanya hivyo maana yake ni kupata huduma hafifu sana kule.

Lakini nataka nikuahidi hapa kwamba tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba hela hizi zinapatikana ili watumishi hawa walipwe waweze kuhamia katika hayo Makao Makuu mapya na pale tumesitiza kwamba wanaweza wakaenda wakapanga badala ya kungoja kila mtumishi apate nyumba yake.

SPIKA: Ombi limetolewa kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri lile swali la kwanza la *ambulance* na orodha uliyosema kwamba utampa Mheshimiwa Dkt. Mgimwa wanaomba ungegawa kwa wote ile orodha uliyokuwa umesema. Kwa hiyo, nategemea *uta-circulate* ile orodha utawagawia watajua wenyewe. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani.

Na. 71

Mji Mdogo Mombo kuwa Halmashauri ya Mji

MHE. STEPHEN H. NGONYANI aliuliza:-

Mji mdogo wa Mombo umejitosheleza vigezo vyote vya kuwa Halmashauri ya Mji:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mji mdogo wa Mombo, kuwa Halmashauri ya Mji?

(b)Je, ni lini Mji Mdogo wa Mombo utaacha kubebwa na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ili kujitosheleza kwa kiwango cha mapato yanayopatikana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji huundwa kutokana na kupandishwa hadhi wa Mamlaka ya Mji Mdogo kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Taratibu za kufuata ni mapendekezo ya kupandisha hadhi kujadiliwa katika vikao vya kisheria ambavyo ni Baraza la Madiwani la Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (*DCC*) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kwa lengo la kupata ridhaa ya vikao hivyo ambavyo vinawakiliwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopatikana kutoka kwenye Halmashauri ni kwamba upo mpango unaoendelea wa kujadili, kuona, kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mombo kuwa Halmashauri ya Mji wa Mombo.

Kikao cha Baraza la Madiwani kilichokaa tarehe 27/10/2011 na kujadili mapendekezo hayo ambapo maazimio yalikuwa ni taarifa irejeshwe kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango maalum ili ifanyiwe marekebisho kabla ya kujadiliwa tena katika Mkutano utakaofanyika tarehe 29/11/2011 katika kikao cha Baraza la Madiwani.

(b)Mheshimiwa Spika, maombi haya yakiwasilishwa rasmi Ofisi ya Waziri Mkoo TAMISEMI yatafanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria sambamba na wataalam kuhakiki vigezo hivyo baada ya kuitishwa kwenye ngazi husika.

Aidha, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mombo ikionekana imekidhi vigezo itapandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji wa Mombo na kuwa Mamlaka kamili inayojitegemea na kuacha kubebwa na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yalinipa ufanuzi zaidi. Kwa kuwa mji mdogo wa Mombo ulianzishwa toka mwaka 2005 na kwa kuwa wewe mjomba wetu unapita pale kila wakati unakunywa chai unaona maendeleo ya mji wa Mombo unavyoendelea haraka.

Kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 14/9/2010 na kwa kuwa wakulima wadogo wadogo wanansumbuliwa sana kwa kuchangishwa pesa kubwa ambazo hazina faida kwoo, badala yake zinakwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya.

Je, Serikali hamna huruma na mji huo ili ukawa Halmashauri ya Mji?

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri mjomba wake.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza labda kwa ajili ya wale wengine ambaa pia watataka kuuliza swalii hili. Hii Mamlaka inayozungumzwa pale ni Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mombo ambayo iko tayari.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo ni kipindi cha mpito kuelekea Halmashauri ya Mji, yaani wafanane kama ilivyo pale Korogwe. Nia na shabaha ya mpango huu ni kuhakikisha kwamba, hakuna ujenzi wa holela holela au wa hovyo hovyo na baadaye unakuta kumekua *squatter*, ndicho anacho *address* hapa; kwa hiyo, Mheshimiwa Ngonyani, pale yuko *right* kabisa.

Kwa hiyo, ndicho tunachozungumza hapa, ukimsikiliza Profesa Anna Tibaijuka, anazungumza habari hii ya watu kujenga hovyohovyo wanajijengea hovyo hovyo tu.

Mheshimiwa Spika, sasa leo linaletwa ombi hapa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaombwa kwamba, akubalia baada ya kukidhi vigezo vyote hivi Halmashauri ile iwe Halmashauri ya Mji.

Hakuna tatizo lolote. Nenda kasome hotuba ya Mheshimiwa Ngwilizi, mle ndani anasema mahali popote ambapo pana Makao Makuu ya Wilaya, amekubali kwamba tuanze kuhakikisha kwamba panakuwa ni Mamlaka ya Mji Mdogo.

Sasa Mombo sio Makao Makuu, lakini Mombo mkiangalia inavyokua kwa wale wanaokwenda Arusha, huwezi ukaiacha ikakaa vilevile. Baadaye utakosa mahali pakuweka nguzo, utakosa mahali pa kupitisha barabara na maji, utakosa kila kitu, utashindwa kufanya pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ninachosema kimoja hapa; akina Ngonyani wakituletea hapa kwa maana ya Halmashauri tukaangalia, hatumalizi hapa tukasoma halafu Waziri Mkuu anasema sawa, nimekubali! Tunachukua timu ya Wataalamu, wanaondoka wanakwenda mpaka kule Mombo ili kwenda kuangalia.

Mambo tunayoyaangalia pale ni kwanza, kuwe na idadi ya watu wasiopungua 30,000. Pili Mamlaka husika iwe na uwezo wa kujitegemea walao kwa 50%. Tatu kuwe na huduma za jamii zifuatazo; hospitali, shule ya sekondari, Kituo cha Polisi, maduka ya reja reja yenyi leseni yasiopungua 50. Nne kuwe na Makao Makuu ya Tarafa, na kadhalika. Sasa nikisema nikusomee hapa kama wamekidhi na nini, nitakuwa najibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoomba tu ni Mheshimiwa Ngonyani na sisi tutashirikiana na wewe. Wewe sukuma hivi vikao, peleka moja kwa moja kwenye *Regional Consultative Committee*, peleka kwenye *DCC*, peleka kwenye Baraza la Madiwani ije hapa. Ikimaliza sisi tuta-*fast track* tutakusaidia. Chai tunakunyuwa pale Mombo, hatutaki kuona Mombo inajengwa hovyo hovyo pale, halafu tunajibu hii.

MHE. DONALD K. MAX: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Na mimi swali langu ni kama la Mheshimiwa Ngonyani, lakini nasema kwamba, Wilaya ya Geita ni kubwa mno tuko wakazi milioni 1.2 pale mjini Geita. Huu mji mdogo umeanza siku nyingi, toka mwaka 2004 mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Sasa nilikuwa naomba suala la Geita lingeangaliwa, wakazi ni wengi mno pale mjini? Nashukuru. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Max, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tunategemea kupata mikoa mipyä minne, Mkoo mmojawapo Makao Makuu itakuwa Geita. Miji mingi ambayo ni Makao Makuu ya Mkoo ina hadhi ya *Town Council*.

Kwa hivyo, sasa hivi Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI*, tunafanya utafiti kuona kama Bariadi, Geita, inaweza kupandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji. Kwa sababu, hatuna maeneo ambayo ni Makao Makuu ya Mkoo lakini yanaitwa Mamlaka ya Mji Mdogo.

Kwa hiyo, naomba tu nimhakikishie ndugu yangu Max kwamba, sisi tuko pamoja na yeye, tutafanya utafiti, kama tutaona mapungufu tutamwambia, ili Geita siku moja iwe ni Makao Makuu ya Mkoo yenyi hadhi ya *Town Council* kama ilivyo kwenye mikoa mingine.

Kuzuia Uharibifu Wa Mazingira

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE aliuliza:-

Mazingira yameendelea kuharibiwa kwa kiwango cha kutisha hususan katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu, lakini Serikali haionyeshi juhudzi zozote za kuzuia hali hiyo:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaweka mikakati ya uhakika ya kuzuia uharibifu wa mazingira?
- (b) Je, ni lini maeneo ya vyanzo vya maji yataainishwa na kupimwa il kuzuia uharibifu huo mkubwa?
- (c) Je kuna maafisa mazingira katika ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata au Vijiji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, kuwa tatizo la uharibifu wa mazingira ni kubwa katika vyanzo vya maji na misitu ya maeneo mbalimbali nchini.

Kwa kutambua ukubwa wa tatizo hili, mwaka 2006 Serikali iliandaa mikakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo ya maji. Mkakati huu uliainisha changamoto 12 za mazingira na hatua za kukabilaiana na changamoto hizo, pamoja na kuweka mikakati ya utekelezaji wake. Aidha Ofisi ya Makamu wa Rais kuititia Idara ya Mazingira inaendelea kuelimisha wananchi kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na mikakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji.

(b) Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa usimamizi wa mazingira ni jukumu la kila mtu, napenda kuwaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane na Waheshimiwa Madiwani pamoja na viongozi wa wilaya katika ngazi zote kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi wote kwa ujumla kuhusu utunzaji wa mazingira.

(c) Mheshimiwa Spika, mikakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji wa mwaka 2006 uliainisha hatua za kuchuuliwa katika kukabilaiana na changamoto mbalimbali. Mojawapo ya hatua hizo ni pamoja mikoa husika kuainisha maeneo ya vyanzo vya maji na kuhifadhi. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, mikoa ya Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro na Manyara, inaendelea na utekelezaji wa kuainisha na kutambua vyanzo vya maji pamoja na kuhifadhi. Naomba nitoe wito kuititia Bunge, hili mikoa mingine pia ifanye kazi kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa mazingira namba 20 ya mwaka 2004 kimeelekeza kila Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya na Miji kuteua kwa ajili ya Ofisa Usimamizi wa Mazingira. Aidha, Sheria imeelekeza Halmashauri za Wilaya kuteua Afisa Mazingira katika kila eneo la utawala la mji Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji. Tayari Halmashauri zote zimeshaajiri Maafisa Mazingira na tunaomba ngazi nyongine za utawala zifanye hivyo.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza; kwa kuwa, Serikali imekuwa ikiweka mikakati mingi sana ya kuzuia uharibifu wa mazingira, lakini mikakati hiyo imeonekana kwamba iko kwenye nadharia zaidi kuliko utendaji. Kwa sababu, mazingira yanaendelea kuharibiwa na hakuna chochote ambacho kinafanyika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka sasa hali hii iwe *practical* zaidi kuliko nadharia?

Mheshimiwa Spika, la pili; kwa kuwa, uharibifu wa mazingira ni kama ni janga la kitaifa. Je, ni lini au ni namna gani sasa Serikali itaimarisha Sheria za kuzuia mazingira? Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mchungaji Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kufanya utendaji uonekane kuliko nadharia ni kwamba kama nilivyojibu katika jibu la awali kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira peke yake, haitaweza kulinda na kuhifadhi mazingira ya nchi nzima. Kama nilivyojibu kwamba, Halmashauri za Miji na Manispaa na maeneo mengine yote yametakiwa kuwa na Maofisa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande wetu Idara ya Mazingira, tuna uhaba wa wafanyakazi; kwa sasahivi tuna wafanyakazi 23 tu, ambao hawatoshelezi kuzunguka nchi nzima. Hata hivyo, tumeomba kibali kuititia Wizara ya Utumishi na tumeruhusiwa kwa mwaka huu kuajiri 23 wengine kwa hiyo, tunahisi tukipata *labour force* hii ya nguvu kazi hii itatusaidia kuzunguka Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba nitoe wito na hapa ninajibu pamoja na swalii jibu la pili kwamba, utunzaji na uhifadhi wa mazingira sio kazi ya Idara ya Mazingira peke yake. Mikakati ipo, Sera zimebekwa na Serikali, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane na Madiwani na Watendaji wengine katika kulinda mazingira yetu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa mazingira katika Jimbo la Kawe na hususan maeneo ya *Kawe Beach* ambapo pamoja na mambo mengine, wenye fedha wanajenga baharini kinyume na sheria lakini vilevile wanajenga kuzuwia kingo za mto. Taarifa ambayo Wizara yako inayo na Mheshimiwa Waziri wa Mazingira alitembelea pale na maagizo yameshatolewa kutoka kwenye Wizara tatu, Wizara yako, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi kwamba, watu waliojenga pale wanatakiwa wavunjive. Lakini utekelezaji umekuwa duni na kuna tuhuma kwamba, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imehongwa na vilevile Jeshi la Polisi limehongwa kwa sababu, hawataki kutoa ushirikiano kwa *NEMC*.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kauli ya Wizara, mnasema nini kuhusiana na sakata hilo? Na ni lini watu waliojenga mtoni na baharini watavunjiwa? Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenyewe kwamba, Wizara yangu ilijibika kikamilifu baada ya kipindi cha Bajeti na tulishirikiana na yeye katika kutembelea eneo hilo na yote aliyoyasema tuliyona kwa pamoja. Kama alivyosema kwamba, majukumu haya yako katika Wizara tatu. Wizara yangu kama kiungo, itaitisha mkutano tena na Wizara zote tatu na tuweze ku-review hatua zilizofikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine kubwa ni kwamba, Mheshimiwa Halima kama Mbunge wa eneo, tunategemea kupata taarifa nydingi kutoka kwake na ushirikiano mkubwa kutoka kwake. Suala la kuhongwa au kutokuhongwa kwa Halmashauri, sio rahisi Wizara kulijua hilo lakini tutamtegemea yeye kutupa taarifa ili tuweze kuzifanyia kazi Wizara zote tatu. (*Makofii*)

Na. 73

Ucheleweshaji wa Michango ya Watumishi Kwenye Mifuko ya Hifadhi

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko mengi mionganoni mwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwamba, waajiri wamekuwa wakichelewa kuwasilisha michango ya Pensheni ya Uzeeni ya Wafanyakazi wao kwenye mifuko hiyo:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa waajiri hao wanaokiuka Sheria na taratibu zilizopo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria zilizoanzisha Mifuko ya Jamii, michango wanayokatwa watumishi kutoka mishahara yao kila mwezi, huwasilishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na waajiri wa Watumishi.

Aidha, michango ya mwajiri kwa watumishi wote wa Serikali huwasilishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kila mwezi na Wizara ya Fedha. Uamuzi wa kuitumia Wizara ya Fedha kuwasilisha michango kwa watumishi wote wa Serikali, ulichukuliwa ili kusiwe na ucheleweshaji wa michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali ni kuwakumbusha waajiri kwamba, kuwasilisha michango ya watumishi ni matakwa ya kisheria na ni lazima yaheshimiwe.

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali inasitiza na inawaagiza waajiri wote kuhakikisha kuwa wanawasilisha michango ya uanachama wa watumishi wao iliyokatwa kutoka mishahara yao kwa mujibu wa sheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kila mwezi bila kuchelewa.

Waajiri wanapaswa kutambua kuwa michango ya uanachama ni sehemu ya mishahara ya watumishi hivyo, si sahihi na ni kinyume cha sheria kushindwa kuwasilisha michango katika muda uliotajwa na sheria ya kila Mfuko.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya kila Mfuko imeweka adhabu kali kwa ucheleweshaji wa michango husika, viwango vya adhabu ni; tozo ya asilimia tano kwa kiwango kilichopitwa na mwezi mmoja na riba ambayo inajumlishwa kama sehemu ya deni kwa kila mwezi unaofuata.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako kuwa, kuna vifungu katika sheria za kila mfuko vinavyoipa nguvu mifuko kuwafikisha Mahakamani waajiri wanaochelewesha kuwasilisha michango kwa Mifuko husika.

Hivyo basi ninawaagiza waajiri wasisubiri mpaka wakapelekwa Mahakamani ili kutekeleza matakwa ya sheria kwa sababu, kutokufanya hivyo kunaongeza gharama za ziada za kisheria za kuendesha kesi na riba. Hivyo ni vyema wakawasilisha michango hiyo ndani ya muda uliopangwa na sheria za Mifuko yao ili kuepuka gharama hizi ambazo kimsingi zinaweza kabisa kuepukika na kupunguza mzigo wa gharama zisizo za lazima kwa Serikali.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, swalii la kwanza. Kwa kuwa, mpaka kufikia mwezi Juni, 2011 Shirika la Mfuko wa Pensheni laWatumishi wa Umma (PSPF) liliikuwa halijapokea jumla ya shilingi milioni 12 kutoka kwa Mamlaka za Maji zifuatazo; Mamlaka ya Maji ya Musoma Mjini, Tabora Mjini, Kigoma Mjini na Songea Mjini.

Je, Serikali inatoa tamko gani kali kwa Mamlaka hizi, ambazo zinakiuka taratibu za kisheria na zenye lengo la kuwataabisha wastaafu watakapostaafu, kwa kulipwa kiwango ambacho sio sawasawa?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa, ni utaratibu unaoeleweka kwamba, mtumishi anapopandishwa cheo au daraja na mshahara wake pia unaongezeka. Je, ni kwa nini mchakato wa kuanza kulipa mshahara mpya, hususan kwa walimu na wafanyakazi wa Wizara ya Afya,

unachukua muda mrefu sana mpaka miaka miwili au mitatu na hatima yake ni kumfanya mtumishi anapostaafu anaendelea kulipwa mafao kwa kutumia kiwango cha mshahara wa zamani na sio mpya? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la pili ambalo ni kwamba, watumishi hasa walimu na wale wa Wizara ya Afya ambaao kwa kweli hupandishwa vyeo halafu wanashindwa kurekebishiwa mishahara yao kwa wakati na hivyo kusababisha wanapolipwa mafao yao wanatumia mishahara ya zamani kutoa mafao hayo.

Mheshimiwa Spika, napenda ifahamike wazi kwamba hayo ni makosa makubwa kwa sababu, hawa watumishi wananyimwa haki zao kwa kukokotolewa mafao kwa kutumia mishahara ya zamani.

Labda tatizo linaweza likatokea kwamba, mtumishi anapopandishwa cheo, la msingi kwa mtumishi huyo aidha awe Wizara ya Afya, awe Mwalimu au mtumishi mwingine ye yule, anatakiwa ye ye mwenyewe akishapandishwa cheo, anatakiwa hicho cheo akikubali kimaandishi. Ni lazima aandike barua ya kukubali kupandishwa cheo na wengi ninafikiri hawatambui hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachukua nafasi hii kuwaambia kwamba, waajiri wote na watumishi wote, waelewe kwamba unapopandishwa cheo ni lazima *u-acknowledge* kukubali kule kupandishwa cheo. Hiyo ndio itakayokusaidia kwamba, mshahara wako utarekebishiwa na hatimaye unapostaafu, basi mshahara wako wa mwisho utatumika kukokotoa mafia yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la kwamba waajiri wanachelewesa kupeleka makato ya watumishi wao, kwa mfano kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba, PSPF haijapokea kiasi cha bilioni 12!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili ni tatizo la waajiri wengi ambaao hawapeleki makato ya watumishi wanayokata kwa wakati kwa hiyo, inaleta shida kubwa sana. Nichukue fursa hii niseme kwamba, Serikali inapenda kuchukua nafasi hii kuwasisitizia na kuwataka waajiri wake kuchukua hatua za makusudi katika kuhakikisha kwamba, makato yanayofanyika yanawasilishwa kwa mifuko bila kuchelewa. Hii itasaidia sana kulipa mafao kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hawa ambaao ni wengi kiasi hicho ninaomba sana Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine, kama wana taarifa za watu ambaao hawajalipa, tuwasiliane na sisi watu wa Hazina tuweze kuwasaidia zaidi.

Na. 73

Malipo ya Pensheni Kulipwa kwa Wakati

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Mtumishi wa Serikali anapomaliza muda wake wa utumishi anastahili kulipwa pensheni yake kwa wakati ili aweze kujikumu kimaisha.

Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwalipa watumishi wa Serikali kwa wakati pale anapostaafu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo utaratibu wa muda mrefu wa kuhakikisha kuwa watumishi wanaostaafu wanalipwa mafao yao kwa wakati mara baada ya kustaafu ambaao ni pamoja na kwamba:-

(i) Mtumishi anayetarajiwa kustaafu anatakiwa kutoa notisi ya kustaafu kwa mwajiri wake miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu kufika. Iwapo mtumishi atashindwa kutoa notisi, mwajiri wa mtumishi anatakiwa kumfahamisha mtumishi tarehe yake ya kustaafu.

(ii) Mwajiri baada ya kupata notisi kutoka kwa mtumishi anawajibika kukusanya majalada ya matumishi yakiwa na kumbukumbu zote sahihi za mstaafu mtarajiwa na kuwasilisha majalada hayo Hazina miezi mitatu kabla ya tarehe ya kustaafu kufika. Hazina baada ya kupata majalada ya mstaafu mtarajiwa uyapitia ili kuona usahihi wa kumbukumbu kabla ya kuyapeleka ukaguzi. Pale inapobainika kuwa kuna upungufu wa nyaraka za mstaafu mtarajiwa Hazina huyarejesha majalada kwa mwajiri ili aweze kufanya marekebisho ya kasoro zilizopo na kuyarejesha tena Hazina. Majalada ya wastaafu watarajiwa yenye kumbukumbu zilizo kamilika na sahihi hufanyiwa hesabu na kupelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kukaguliwa. Majalada yale ambayo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali atayapitisha kuwa hayana kasoro wala upungufu ndiyo ambayo wastaafu watarajiwa uandaliwa malipo yao na wastaafu kupokea hundi za mafao yao mara baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, iwapo utaratibu nilioueleza hapo juu utafuatwa na kutekelezwa na wadau wote watumishi wanaostaafu watalipwa mafao yao mara tu wanapostaaafu na kuondokana na ucheleweshaji.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kuwa hizo taratibu ndizo ambazo zinafuatwa na ngazi mbalimbali za Serikali ili kuwezesha wastaafu hao waweze kupatiwa mafao yao kwa wakati.

Ni kwanini sasa kumekuwa na ucheleweshaji wa kulipwa mafao ya wastaafu hao mfano walimu na wale wazee waliokuwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambaa mpaka sasa mafao yao hayajalipwa.

Kuna taratibu mbili za kulipa mafao ya wastaafu hao, kuna taratibu ambayo inatumia ile ya miezi mitatu, mitatu na kuna utaratibu ule ambaao unatumia miezi sita. Kwa kuwa katika utaratibu wa kutumia miezi sita kila baada ya miezi sita kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa mafao hayo. Kitu ambacho kinasababisha mafao hayo kuwafikia wale wastaafu hususan miezi ya Januari, hayo mafao yanakuja kulipwa mwezi wa pili na inasababisha wastaafu hao washindwa kukimbizana na msimu wa elimu kuwapeleka wanafunzi shule na msimu wa kilimo.

Ni kwa nini sasa Serikali isiachane na huo utaratibu wa kuwalipa wastaafu mafao yao kila baada ya miezi sita na wakauchukua ule wa miezi wa mitatu ambaao unaonekana kukidhi mahitaji ya wastaafu hao? (Makofi)

SPIKA: Majibu Naibu Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Nikianza na lile suala mwisho ya kwamba wastaafu badala ya kulipwa miezi sita sasa iangaliwe kwamba wapunguziwe kidogo waweze kulipwa ili waweze kukidhi haja zao za haraka kama vile kulipa karo za shule.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu sasa baada ya kuangalia wastaafu wote waliokuwa wanalamika kwamba muda wa miezi sita ni mrefu sasa Serikali imeridhia na kuanzia mwezi wa Januari wastaafu wote watalipwa miezi mitatu kuanzia mwezi wa Januari. (Makofi)

Hilio swali la pili kuhusu wastaafu kuchelewesha kulipwa mafao yao hasa wale wa *East Africa Community* na walimu, kwa upande wa walimu sehemu kubwa kwa kweli ni upotetu wa kumbukumbu wakati wa kustaafu. Kumbukumbu kama zinakuwa hazipo basi hata malipo yanachelewa kulipwa ya mafao wakati wa mwisho. Hili la *East Africa Community*, naomba nitangazie Bunge lako Tukufu kwamba karibu wastaafu wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamelipwa wote na zimetumika bilioni 117 kwa ajili ya zoezi hili na wale ambao watakuwa wamebaki wachache, ambao tu labda watakuwa wapo bado ni kwamba kumbukumbu zao nyingi hazina uhakika. Kwa hiyo, inachukua muda kuzihakiki na wengi wanaenda mahakamani na baada ya mahakama ikibainika kwamba anastahili kulipwa atalipwa.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Spika, imegundulika mara nyingi mafao yanalipwa wastaafu siyo sahihi, kama ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika miaka ya 2006, 2007/2008 kwa mfano. Katika majalada 7114 kwa mwaka 2006, majalada 516 yalilipwa pungufu shilingi 416. Katika mwaka 2007, katika majalada 5332 majalada 142 yalilipwa pungufu shilingi 288. Sasa Serikali haioni pamoja na utaalalm walionao wanawanyima haki zao wastaafu hawa ambao ni wanyonge na Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hayo?

SPIKA: Kwa maana ya kwamba mstaafu mmoja anapungukiwa mia nne na au unamaana gani hata hatujakuelewa vizuri.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Kiwango cha majalada ambayo yanakaguliwa mfano 7114, majalada 516 yangelipwa pungufu shilingi milioni mia nne. Sasa kwa wingi wake huo ina maana kila mmoja kuna upungufu mkubwa wa fedha katika mchakato wa kukokotoa. Je, Serikali haina wataalam wa kutosha?

SPIKA: Nadhani umeelewa wewe ulikuwa mkaguzi utakuwa unaelewa, kwamba hawalipwi kiwango wanachostahili, Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma.

WAZIRI WANCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kama alivyotangulia kujibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, kwamba utaratibu kabla mwajiriwa hajapata mafao yake. Lile faili likishakokotolewa na Wizara ya Fedha linapelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali ili kujiridhisha kwamba kile kiwango ambacho atalipwa au kimekokotolewa ni sahihi au laah! Kwa hiyo, baada ya kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndipo mafao yale sasa ndipo yanapotolewa.

Kwa hiyo, ile taarifa ni kwamba kama isingepite kwa Mdhibiti wale watumishi wangelipwa chini ya kiasi kile.

Kwa hiyo, mwajiriwa yoyote kabla ya kupata mafao yake ni lazima yapitie kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili ajiridhishe kwamba ukokotoaji upo sahihi. Kwa hiyo huwa hilo linafanya kabla ya mafao hayajatolewa.

Na. 75

Kashfa ya Kugushi vyeti kwa Waajiriwa wa JWTZ

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT aliuliza:-

Kuna baadhi ya vijana wanaojiunga na JWTZ kwa vyeti vyaa kugushi na wakati mwingine hugundulika wakiwa wameshafuzu mafunzo ya kijeshi.

Je, ni adhabu gani ya kisheria inachukuliwa kwa atakayebainika na kashfa kama hiyo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda swalii la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mbunge wa Koani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya vijana kuandikishwa jeshi hufanyiwa usaili ukiwemo ukaguzi wa vyeti. Vyesti vinavyotiliwa mashaka hupelekwa Baraza la Mitihani (*The National Examinations Council of Tanzania*) kwa uthibitisho zaidi kama ni vya kugushi au halali.

Mheshimiwa Spika, vyesti vinavyothibitishwa kuwa ni vya kugushi hushikiliwa na Baraza la Mitihani, hivyo ni wajibu wa Baraza la Mitihani kusimamia mchakato wa kuchukua hatua za kisheria na ikigundulika wakati huo huo huondolewa kwenye mchakato wa usaili.

Mheshimiwa Spika, itokeapo kugundulika baada ya kusajiliwa na kuanza mafunzo kuwa mwanajeshi ana vyesti vya bandia au kwa mfano katumia vyesti halali vya mtu mwingine mwanajeshi huyo hushitakiwa katika mahakama ya kijeshi kwa kosa la udanganyifu wa nyaraka.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, mpaka sasa ni wanajeshi wangapi waliokumbwa na kosa la udanganyifu wa nyaraka na kati ya hao ni wangapi wanawake wakinamama kama mimi?

Hao wanaojunga na jeshi la Kujenga Taifa, hupata wapi taarifa za kuijunga na jeshi hilo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Andrew Clement, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuanzia na swalii ni wangapi amba o wamekwishashikwa na hatia hiyo. Kwa taarifa nilizonazo na za haraka haraka ni kwamba kuanzia mwaka 2000 mpaka 2011 askari waliopatikana na hatia ya kufukuzwa kazi ni mmoja tu. Lakini kwa sasa hivi wapo askari kama saba amba o wanaubiri mashitaka baada ya vyesti vyao kugundulika kuwa vina utata. Mimi nataka nichukue nafasi hii nipongeze jeshi kwa kuhakikisha wanaingiza vijana amba o ni waadilifu kiasi ambacho siyo wengi wanaofoji.

Lakini (b) ya lile swalii lake la kwanza la kwamba ni wangapi amba o ni wanawake nataka niseme tu katika hao waliogundulika hakuna mwanamke hata mmoja. (*Makofii*)

Wengi wanaoshikwa ni wale unakuta wameshaingia vizuri na vyesti vyao labda vya form four lakini vya kidato cha nne labda mpaka sita lakini wakiingia humo ndani wakati mwingine wanataka kuijendeleza na wanataka kupanda cheo. Kwa hiyo, wanaweza kuazima vyesti vya watu wengine wakavitumia. Sasa ho ndiyo wengi walioshikwa kwa nafasi hizo.

Kwa hiyo napenda nichukue nafasi hii nisisitize kabisa wanajeshi wetu wakuu wahakikishe kwamba masuala ya kuwa kwamba una uhakika wa ile elimu ambayo una claim kwamba unayo yanazingatiwa mpaka jeshini.

Swali lingine alilouliza nadhani ni lile la wanaojiriwa wanakuwa ni wa namna gani, kwanza niseme tu kwamba askari wa kawaida wanaajiriwa kuititia Jeshi la Kujenga Taifa na askari wa kawaida ni wale unakuta wa kidato labda cha nne mpaka cha sita kuititia Jeshi la Kujenga Taifa wakienda kule wanachukuliwa kutokea kule kule jeshi linapotaka kuajiri.

Lakini wengine wale amba o ni ma-professionals kwa maana ya wanataalam wenye *diploma* mbalimbali, madaktari, labda ma-accountants hata ma-engineers, wahandisi na kadhalika Makao Makuu ya Jeshi hutangaza hizo nafasi zinapotokea katika magazeti na nadhani hivi karibuni tu walitangaza na wengi wame-apply.

Kwa hiyo nataka tu nihimize tu kwamba watu wajitahidi tuweze kuingia huko jeshini tuweze kujenga nchi yetu na kulinda nchi yetu. Ahsante sana. (*Makofî*)

Na. 76

Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya Ujenzi wa Barabara ya Ikwiriri - Mloka - Vikumburu

MHE. DKT. SEIF S. RASHID aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya kutoka Ikwiriri-Mloka-Vikumburu ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa imeainisha katika mpango wa ujenzi wa barabara ya mko wa awamu kwa km.36 kila mwaka katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. Lakini katika mpango wa mwaka 2011/2012 barabara hiyo haikutajwa:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais katika mpango wa Wizara husika kwa mwaka 2012/2013?
- (b) Je, lini ujenzi huo unategemewa kuanza?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalî la Mheshimiwa Dkt. Seif Selemmani Rashid, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Napenda kumthibitisha Mheshimiwa Mbunge kuwa ahadi ya mheshimiwa Rais aliyoitoa kuhusu kujenga barabara ya Ikwiriri - Mloka - Vikumburu kwa kiwango cha changarawe imeanza kutelekezwa.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara hii yenye urefu wa kilometra 162.6 ilipandishwa hadi mwezi Agosti, 2009 kutoka barabara ya wilaya hadi kuwa barabara ya mko. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, jumla ya shilingi milioni 98.66 zilitengwa kwa ajili ya barabara hii.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya shilingi 49,502,000 zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya kawaida barabara hii katika sehemu ya Ikwiriri hadi Mloka. Tayari mkandarasi ameteuliwa na Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara hii ili iweze kuitikwa kwa urahisi majira yote ya mwaka.

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina swalî moja la nyongeza, kutokana na ukweli kwamba barabara hii ilianza kutengenezwa kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea kutengwa kwa fedha kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011 na kwamba bado matengenezo hayo hayajaonyesha ukamilifu wa ujenzi na watu kutoridhika kabisa na utengenezaji huu ambao ulikuwa umefanyika na hasa kile kipindi cha kukaribia kwenye uchaguzi kulikuwa na maburudoza yakifanya kazi kwa kipindi kifupi na baada ya pale hakuna kitu ambacho kilionekana kuonekana pale mpaka hivi sasa.

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari, Serikali itakuwa tayari sasa kuwaambia wana Rufiji kwamba zitatengwa fedha kwa ukamilifu wa ujenzi wa barabara hiyo katika awamu moja?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalî la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Seif Selemmani Rashid, Mbunge wa Rufiji, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, napenda kumthibitisha Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo husika kwamba Serikali imejipanga kuitengeneza hii barabara. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba barabara hii ilikuwa barabara ya wilaya ilipandishwa hadi mwezi Agosti, 2009.

Wizara ya Ujenzi imeanza kuishughulikia na kuipangia Bajeti katika Bajeti yake ya mwaka 2010/2011 na katika Bajeti yake ya mwaka huu 2011/2012. Katika Bajeti ya mwaka huu zimetengwa kiasi cha milioni 49 ambacho nina uhakika kitaanza kutumika. Nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba kwa vile barabara hii sasa imetambuliwa kwamba iko chini ya *TANROAD*, tunaendelea kuishughulikia kuitengeneza hata kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara.

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASIR: Mheshimiwa Spika, stendi ya mji ya Korogwe ilijengwa kwa gharama kubwa sana lakini kuna sitofahamu ya kuachwa sehemu ya kazi na mkandarasi aliopewa sababu ikiwa ni malipo ambayo mpaka sasa bado hayaafanya.

Je, Wizara haioni ni muhimu sasa kumalizika kwa kazi ile ya stendi ile ya Korogwe kwa kumlipa mkandarasi ili hatimaye na barabara inayoelekea Magunga hospitali iweze kujengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Nasir hilo swali lako linauhusiano gani na barabara?

MHE. YUSUPH ABDALLAH NASIR: Mheshimiwa Spika, hili swali linahusu Wizara ya Ujenzi na mkandarasi alipelekwa na *TANROAD*.

SPIKA: Basi ahsante sana naomba hili swali halihusiki kabisa. Mheshimiwa Mipata.

MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuanza vizuri kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kutuma Kamati ya kwenda ku-access barabara za kupandishwa hadhi ambazo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alizitolea ahadi.

Je, ni lini majibu ya accessment za barabarani zilizoletwa Wizarani kwa ajili ya kikao cha mwisho cha Wizara zitatoa taarifa ya majibu?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupandisha barabara kutoka kuwa barabara ya wilaya kwenda ya mkoa au kutoka ya mkoa kwenda ya Taifa au hata kuteremsha barabara kutoka ya Taifa kurudi ya mkoa au kutoka kwenye mkoa kwenda kwenye wilaya huwa inashughulikiwa na Kamati zinazotumwa kule kwa ajili ya kufanya shughuli.

Kwa hiyo ni lini tutatoa itatokana na ile taarifa itakavyopelekwa kwenye bodi za barabara za mikoa na Mwenyekiti wa bodi hizo ambazo ni wakuu wa mikoa watakapoandika kwetu na kufanya uchambuzi taarifa tutatoa kamili kwamba ni barabara ipi imepandisha hadhi na ipi imeteremshwa hadhi.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi imekwishabaini tatizo la kivuko cha watembea kwa miguu eneo la Mabatini Jijini Mwanza, ambalo linachangia kuwepo kwa msongamano wa magari katika barabara iendayo Nyakato. Ili kutatua tatizo hili la msongamano, kunahitajika kupanua barabara kuwa njia mbili kuanzia eneo la Nata hadi Buzuruga kwa makisio ya gharama ya shilingi bilioni nne na pia kujenga daraja la juu eneo la Mabatini kwa ajili ya watembea kwa miguu kwa makisio ya gharama ya shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Spika, kazi za upembizi wa barabara pamoja na ujenzi wa daraja la juu zitaanza mara fedha zitakapopatikana.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na kuwapa pole nydingi Wakazi wa Jiji la Mwanza hasa Wakazi wa Mabatini, ambapo swali lenyewe

linalenga kwa mafuriko yaliyowapata juzi. Ninapenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Jibu la Waziri linasema ujenzi wa daraja hilo unatokana na upatikanaji wa fedha na kwa uzoefu nilionao bajeti yetu ya Taifa huwa inaongezeka karibu trillioni mbili au mbili na nusu kila mwaka. Je, siyo wakati mwafaka sasa Waziri katika Miradi yake akaliwekea umuhimu au kipaumbele suala zima la daraja hili?

(ii) Kwa kuwa ametamka yeche mwenyewe kwamba kuna huo upanuzi wa barabara na ndio hilo daraja nalo litakuwepo katika kujengwa; je, anaweza sasa kuwaambia wahusika au ndio ukawa wakati mwafaka wa kuwaambia wahusika watakaoguswa na upanuzi huo wa barabara kwa sababu mara nyingi huwa kunajitokeza mgogoro wa Wananchi na Serikali kuwa nani kakutwa na barabara au barabara imemkuta?

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mabatini ni kweli kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kwamba, panahitajika daraja au *fly over* itakayoweza kusaidia kupunguza msongamano katika barabara yote itokayo Buzurugwa hadi Nata.

Kuhusu nani wataguswa katika upanuzi huo, sheria ipo wazi na sheria ni msumeno. Upanda wa barabara ya kutoka Mwanza kwenda Buzuruga hadi Nyakato mpaka Musoma kwa mujibu wa Sheria Namba 13 ya Mwaka 2007 ni mita 30. Kwa hiyo, Wananchi wa Mwanza, ndugu zangu Wasukuma waliojenga kwenye *road reserve*, waanze kuondoka ili tutakapoanza kupanua hakuna atakayelipwa fidia kwa sababu sheria ni msumeno na kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, Ibara ya 26, Kifungu namba (1) na (2) kinasema kila raia wa Tanzania ana wajibu wa kuheshimu Katiba na Sheria. Kwa hiyo, tutakapoofika wakati huo wa kutengeneza au kupanua barabara hiyo, wote walio ndani ya *road reserve* hakuna cha fidia.

Ninapenda pia kutoa wito kwa Wananchi wanao-park malori na magari katika maeneo ambayo yanatakiwa kupita watu na hasa katika maeneo ya Mabatini, Nyakato Buzuruga mpaka kwenye Stendi ya Barnabas, waache kufanya hivyo kwa sababu wanavunja sheria kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mheshimiwa Selasini Joseph Roman, atauliza swali.

Na. 78

Uboreshaji wa Viwanja vya Michezo

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha viwanja vya michezo na kuhakikisha angalau kila Kata ina viwanja bora vya michezo kwa ajili ya vijana na Wananchi wa maeneo husika kama mkakati wa kupunguza wimbi la vijana walioko mitaani ambao hawakupata fursa ya kuendelea na masomo basi wajifunze michezo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Selasini Joseph Roman, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Serikali inapenda kuona maeneo mengi kadiri iwezekanavyo, ikiwa ni pamoja na yale yaliyo katika ngazi ya Kata, yanakuwa na viwanja vingi na

bora vya michezo. Ili kuhakikisha kuwa viwanja hivyo vinapatikana na kutumika ipasavyo, Wizara imepanga mikakati ifuatayo:-

- Kufanya tathmini ya viwanja vilivyopo na ubora wake.
- Kuhamasisha Halmashauri nchini kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya viwanja vya michezo katika ngazi zote ikiwemo ya Kata.
- Kuhamasisha na kuishirikisha jamii katika ngazi mbalimbali ili kutunza na kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya michezo.
- Kuendesha mafunzo ya utunzaji na uendeshaji wa viwanja kwa wamiliki na wadau wa michezo katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu zaidi ni kuzihamasisha Halmashauri na watu binafsi wenye uwezo, hasa ndani ya Halmashauri hizo, kuwekeza katika ujenzi wa viwanja vya michezo, hata kama vitatumika kibashara. Mfano mzuri ni Kampuni ya Bakresa ambayo imejenga uwanja wake huko Chamazi, Wilaya ya Temeke, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa, Klabu ya Yanga ya Dar es Salaam na kadhalika. (*Makofii*)

Hatua hiyo itawezesha kuweipo kwa viwanja bora vya michezo ambavyo vitawezesha vijana waliopo mitaani ambao hawakupata fursa ya kuendelea na masomo wajifunze na pia kushiriki kikamilifu katika michezo mbalimbali.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, pili, ninatambua kwamba, katika nchi yetu vipo viwanja mbalimbali vya michezo hususan vya mpira wa miguu:-

(i) Je, Serikali inaweza kutuambia viwanja hivi ni vingapi na vina hadhi gani kwa ajili ya kutumika kwa michezo hasa mpira wa miguu?

(ii) Je, wamiliki wa viwanja hivi ni akina nani na viwanja hivi kwa sasa hivi vinawasaidiaje vijana hasa wa Rombo katika kuendeleza michezo yao na kujenga afya zao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba ujibu kwa kifupi sana maana muda umekwisha.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza, viwanja mbalimbali ambavyo tunavyo kama Serikali inavitambua ni vingapi, mimi ninapenda niseme kwamba kwa *statistics* za haraka haraka vile viwanja ambavyo tunawenza tukavipanga katika madaraja mbalimbali ukitoa vile ambavyo ni vya kwenye shule na katika vyuo vikuu na kadhalika, tunavyo kama 27 na hivyo viwanja tunaweza tukavigawanya katika madaraja kama manne. Kwanza, kuna vile vinavyoangukia katika daraja la kwanza ambavyo tunawenza tukasema ni vitatu na vyote vipo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hivi ni Uwanja wa Taifa, Uwanja wa Uhuru na Uwanja na Karume na labda kwa sasa hivi Kiwanja cha Azam kinawea kikaingia katika hii *grade* ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, daraja lingine ni la pili na vipo viwanja kama saba katika Mkoa wa Mwanza, Dodoma, Tabora, Songea, Morogoro, Arusha na hata Mbeya. Ninaposema hivi inaonekana kabisa kuna viwanja vya dhati katika Mikoa mbalimbali hapa nchini na vingine vipo katika daraja la tatu na vilivyopo katika daraja la tatu vipo kama sita katika Mikoa ya Tanga, Shinyanga, Iringa, Kagera, Mtwara na Mwanza, vinaweza kuangukia katika daraja la tatu. Mwanza kuna kiwanja kingine pia.

Pia viwanja ambavyo vinaweza kuangukia katika *grade* ya nne vipo kama kumi katika Mikoa ya Lindi, Singida, Rukwa na hata Kilichopo hapa Dodoma na Kilichopo Moshi. Ninataka nisisitiza hapa kuwa, Moshi labda hicho ndiyo Mheshimiwa Selasini kinawenza kumfaa, tunawenza tukazungumzia hicho labda kinawenza kumfaa na Wananchi wake wa Rombo pia na wale wa Moshi wanawenza kufaidika katika hicho kiwanja, lakini kipo katika daraja la nne. Kwa hiyo, ninataka nichukue nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Selasini pamoja na Wabunge waliopo huko Moshi kuhakikisha wanafuatilia hili kwa karibu na kuhakikisha kwamba hicho Kiwanja cha Moshi kinapanda na kufika daraja la kwanza.

Sasa wamiliki wa hivi viwanja ni akina nani? Labda niseme tu kwamba, wamiliki wa hivi viwanja kwanza ni Serikali Kuu pamoja na Halmashauri. Viwanja viwili katika hivi ambavyo nimevizungumzia vinamilikiwa na Serikali Kuu, yaani Uwanja wa Taifa pamoja na kile cha Uhuru. Vingine vinamilikiwa zaidi na Halmashauri na hivyo vipo vingi tu, vipo kama kumi. Kwa hiyo, ukiangalia Serikali pamoja na Halmashauri zinamiliki viwanja kama 12 na vingi vyao vipo katika ile *grade* ya kwanza na ya pili.

Vingine vinamilikiwa na Chama cha Mapinduzi ambavyo ni kama viwanja 12. Mimi ninataka nichukue nafasi hii, nihimize wale ambaa ni wamiliki wa hivi viwanja kuhakikisha kwamba, vinakuwa katika hali nzuri. Kwa ujumla wametusaidia sana, kwa mfano, Chama cha Mapinduzi kimehakikisha viwanja vyake vinatumika vizuri kuendeleza masuala ya michezo hapa nchini bila ubaguzi kwamba una-*belong* kwenye chama gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, viwanja vingine vinamilikiwa na vilabu vya michezo na kama nilivyotoka kuzungumza ni vitatu, mpaka sasa hivi kuna Mtibwa, Azam. Ninataka nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa, niwapongeze Azam, kama Sera yetu ya Michezo inavyoagiza, kuhakikisha kwamba vyama vikubwa vikubwa vinavyoingia katika *Premium League* viwe na nyenzo zao au miundombinu yao ya kuchezea michezo. Viwanja vingine kama nilivyongumza vinamilikiwa na Vyuo, Taasisi na Shule mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Kwa urefu wa majibu, ninaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

Na. 79

Magari ya Abiria Kusimamishwa Mara Nyingi na Askari

MHE. ALI KHAMIS SEIF aliuliza:-

Magari ya abiria kutoka Mkoani kwenda Chakechake husimamishwa mara kwa mara kwenye Vituo vya Polisi vya Mtambile na Chakechake na pia askari wa barabarani nao husimamisha magari hayo mara nyingi na kuwa kero kubwa.

Je, Serikali itakubliana nami kwamba umefika wakati wa kuondoa utaratibu wa kusimamisha magari ya abiria kwenye vituo hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimepokea hiyo taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, huko Mkoani na Chakechake kuna kero barabarani.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, usimamishaji wa magari katika maeneo mbalimbali ni utaratibu wa muda tu na iwapo sababu zilizofanya kuwepo kwa utaratibu huo zitathibitika kupunguza au kuisha kabisa bila shaka utaondolewa.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, jibu la Mheshimiwa Waziri kuwa utaratibu huu ni wa muda kwanza sikubaliani nalo na pili inaonekana kwamba Serikali hawakulifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, juu ya hilo nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Utaratibu huu wa magari ya abiria kusimamishwa katika Vituo vyá Polisi upo zaidi ya miaka 40 sasa. Serikali ipo tayari suala hili kulifanyia kazi ili kero hii iondoke?

(ii) Kama anakubaliana na wazo langu kazi hiyo itaanza lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Maswali mafupi na majibu mafupi pia kwani muda sina.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge asiwe na ghadhabu kwa sababu niliposema kwamba, utaratibu ni wa muda ninasema tunapoweka *barriers* katika barabara huwa kuna sababu zake na kwa kawaida hizi *barriers* huwa zinakuwepo kwa muda, ndiyo maana yangu hiyo na ndiyo utaratibu wenyewe.

Anaposema zimekuwepo kwa muda, nimemwambia katika jibu langu la msingi kama Mheshimiwa Mbunge amenisikiliza vizuri na nimwombe kabisa arejee pale; nimesema kwamba, nimepokea hiyo taarifa yake kwa maana ya kusema kwamba tutaitazama kwa undani zaidi.

Kwa hiyo, hilo suala la kusema kwamba tuchukue tu maamuzi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, halitawezekana kwa sababu wakati mwingine katika vituo hivi mahali ambapo magari yanapita, vitu kama silaha vinapita, madawa ya kulevyia yanapita na kadhalika. Ndiyo maana nimesema itakapothibitika, tutafanya utaratibu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hali kama hiyo isipokuwepo basi kutakuwa hakuna sababu ya kuwa na vikwazo vyá namna hiyo barabarani.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, tunakwenda kwa *gender*.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia fursa hii.

Kwa kuwa kumewekwa *barrier* kati ya Tarime Mjini na Sirari; ninataka kujuua kuna umuhimu gani wa kuwepo kwa *barrier* kwenye Kijiji cha Nkende wakati kuna *barrier* Sirari na karibu na Kirumi; maana imeleta usumbufu kwani haisimamishi tu magari inasimisha pia magari madogo ya abiria na hata pikipiki?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo:-

Hilo alisemalo ni dhahiri kabisa na lalamiko hilo lileetwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipoutembelea Mkoa wa Mara muda si mrefu na nimhakikishie kwamba, tunalifanyia kazi na pale ambapo tutaona kweli upo usumbufu, raia wanansumbuliwa, hatua za haraka zitachukuliwa kuondoa *barriers* za namna hii.

Na. 80

Uchimbaji wa Tanzanite Nchini

MHE. ANNE K. MALECEL A aliuliza:-

Utafiti uliofanyika unaonesha kuwa itachukua zaidi ya miaka elfu moja kupatikana nchi nyiningine itakayochimba na kuhodhi Vito vya *Tanzanite*:

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya *Tanzanite* kuwa mali na alama ya Taifa na hivyo ikawaunganisha wachimbaji wadogo kuchimba vito hivyo kwa niaba ya Taifa ili isipoteze utambulisho wake?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anne Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Madini ya *Tanzanite*, imeweka mikakati mbalimbali ya kulinda madini hayo ikiwa ni pamoja na kuanzisha *Mererani Controlled Area* ili kudhibiti uingiaji na utokaji wa wageni katika eneo la machimbo ili kupunguza biashara ya magendo ya madini hayo. Aidha, Serikali imeanzisha *Certificate of Origin* ili kudhibiti utoroshwaji wa madini hayo nje ya nchi kwa kila anayesafirisha.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kutangaza na kuhamasisha matumizi ya *Certificate of Origin* umeandaliwa, ambapo Serikali imewasiliana na nchi ambazo ni wanunuzi wakubwa wa *Tanzanite* ikiwa ni pamoja na Marekani na India kuto Kubali kuingiza madini hayo yasiyokuwa na hati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 imeyafanya Madini ya *Tanzanite* kuwa *specified gemstones*, lengo ni kuweka utaratibu maalum wa kuchimba na kuuza madini hayo. Vilevile Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 inaelekeza kuwa, leseni za uchimbaji wa madini ya vito ikiwa ni pamoja na *Tanzanite* ni kwa Watanzania tu, isipokuwa pale ambapo Waziri mwenye dhamana ya madini kwa kushauriana na Bodi ya Ushauri wa Madini, atakapoona uchimbaji unahitaji teknolojia na mtaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mbunge wa kuwaunganisha wachimbaji wadogo wa *Tanzanite* kwa lengo la kuongeza ushiriki wa Watanzania katika shughuli za uchimbaji wa madini haya ni mzuri. Serikali itaangalia utaratibu mzuri wa kuufanya kazi.

Umuhimu wa kuunganisha wachimbaji wadogo ni pamoja na kuwatengeneza mazingira ya kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi zao kwa vikundi, kupunguza ajali zinazotokea mara kwa mara katika machimbo hayo zinazotokana na mwilingiano wa mashimo, yaani mitobozano na uvutaji wa hewa chafu, kuongeza tija yao na kutengeneza njia za kupata ufumbuzi wa upatikanaji wa mitaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Mbunge na wadau wengine wa uchimbaji mdogo wa madini, washirikiane na Serikali ili kutengeneza utaratibu bora utakaoongeza ushirikishwaji wa Wananchi katika Sekta ya Madini.

MHE. ANNE K. MALECEL A: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa madini huwa yanakwisha na kwa utafiti nilioufanya kwa sababu mimi nina *interest* sana na madini ni kwamba *Tanzanite* inachimbwa kwa wingi na wageni kuliko Watanzania. Je, Serikali haioni kwamba madini haya yatafikia wakati yatakwisha, wenzetu kwenye nchi zao wameyaweka kwenye stoo na wao ndiyo watakuwa wanahodhi madini haya; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuangalia jambo hili kwa mara ya pili? Hilo ni swalii la kwanza.

(ii) Kwa kuwa hivi sasa kuna kila dalili ya kwamba Dunia itaingia kwenye mtikisiko wa kiuchumi na wenyewe mmeona Serikai kubwa kama Ugiriki na Italia zina matatizo ya kufilisika; na

kwa kuwa mataifa ambayo yako imara na makini wenzetu wameanza kuhodhi rasilimali zao na wenyе mafuta wanahodhi rasilimali zao na ndiyo maana tunapata matatizo ya bei kuwa juu; je, Serikali haioni kwamba ni muhimu na ni lazima sasa tusimamie madini yetu kwa sababu nina uhakika hatujayasimamia vizuri? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madini yanakwisha kama inavyokuwa kwa kesi ya *natural resources* kulingana na jinsi yanavyovunwa. Kwa upande wa Madini ya *Tanzanite*, yana *special characteristic* kwa sababu ni madini ya *zoisite* lakini *zoisite* yenye ni *only particular to Tanzania*. Yako maeneo kama 12 duniani ambayo yana *zoisite*, inayopatikana Tanzania ni *specific to the Tanzanian area* kwa maana mengine yanapatikana Austria na Norway yanafanana, lakini ya kwetu ni aina ya pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninakubaliana naye kwamba ni kweli ni madini ya kipekee. Tumekuwa tunafanya mikakati ya kufanya *marketing* ya *Tanzanite* kama *a special gemstone* na ndiyo maana tumesema ni *specified gemstone* kwa maana ya kwamba, huko mbele *marketing* yake na kadhalika, tunatarajia kwamba, watu wataitazama hivyo. Hayo pia yanategemea na masoko ya *Tanzanite* ambayo kusema kweli yameanza kutambua kama ni madini makubwa.

Mheshimiwa Spika, hili la kwamba, kuna kila dalili kuwa nchi itaingia kwenye mtikisiko wa kiuchumi na kwamba ni muhimu tuhifadhi madini yetu; ninakubali na ninapata tabu kidogo kutokana na hili la kwamba, watu wanachimba Madini ya *Tanzanite* ili kwenda kuyaweka kwenye hifadhi tu; kwa sababu katika utaratibu huo, madini yale lazima yawe na *monitoring circulation* ili yaweze kuuzwa na kurudi tena kwenye kuchimba.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninakubaliana naye kwamba, katika hali hii kuna suala zito la kuangalia tunakowenda kuhusu uchimbaji, siyo wa *Tanzanite* tu, lakini wa madini yetu yote na hilo tumelieleza kwenye Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kwenye Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

SPIKA: Kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Mnyaa.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika, hajajibu swali langu la pilii!

SPIKA: Amejibu!

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Aah, hajajibu mtikisiko wa hali ya kiuchumi duniani.

SPIKA: Ndiyo anasema kwamba; kwanza, haelewii kama kuna *monetary value* yake, lakini anakubaliana na wewe; ndivyo ambavyo amejibu.

Mheshimiwa Mnyaa swali linalofuata.

Na. 81

Mchango wa Elimu katika Maendeleo

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA aliuliza:-

Maendeleo ya kielimu yanahitajika sana kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kunufaika zaidi kiuchumi:-

(a) Je, kuna Vyuo Vikuu vingapi vilivyoko Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda, vinavyotambuliwa na *TCU* na vipi havitambuliwi?

(b) Je, ni wahitimu wangapi wanapatikana kila mwaka kwa kila nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki?

(c) Je, kuna idadi ya watu wangapi Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (K.n.y. WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Vyuo Vikuu vyote katika nchi za Afrika Mashariki vinavyotambuliwa na Serikali na Mamlaka za Ithibati za nchi hizo, vinatambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*). Idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki, vinavyotambulika katika Nchi za Afrika Mashariki sasa ni 148. Mchanganuo wa vyuo hivyo kwa kila nchi ni kama ifuatavyo; Tanzania (40), Kenya (51), Uganda (32), Burundi (6) na Rwanda (19).

Mheshimiwa Spika, Tanzania hatuna Chuo Kikuu hata kimoja kilichodahili wanafunzi bila kupata kibali cha Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*). Aidha, kwa nchi nyininge za Afrika Mashariki hatuna taarifa rasmi kutoka mamlaka husika za nchi hizo kuhusu vyuo vyao visivyotambulika.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Tanzania kwa miaka kumi iliyopita (2001 - 2010) ni 91,497, hii ikiwa ni wastani wa wahitimu 9,150 kwa mwaka. Taarifa rasmi ya idadi ya wahitimu wa Vyuo Vikuu katika nchi nyininge za Afrika Mashariki hazikubainishwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Takwimu za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2010 (*East African Community Facts and Figures 2010 Report*), inaonesha kuwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao milioni mia moja na thelathini. Idadi ya watu kwa kila nchi ni kama ifuatavyo; Tanzania (milioni 42) Kenya (milioni 39), Uganda (milioni 31), Burundi (milioni 8) na Rwanda (milioni 11).

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swalii la nyogeza. Kabla ya kuuliza swalii la nyogeza, nikupe taarifa kwamba, swalii la kipengele (b) halikujibiwa kikamilifu na Kanuni ya 46 inahitaji Mbunge ajibiwe kikamilifu.

Katika swalii la kipengele (b) nilitaka twakimu kwamba ni wahitimu wangapi wanapatikana kwa mwaka kwa kila Nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nimejibowi kwamba ni wastani wa watu 9,150 tu kwa Tanzania, hizo nchi nyininge hajataja. Hata hivyo, nitauliza swalii langu la msingi ambalo nilitegemea kuliuliza hapa.

Kwa takwimu zilizotolewa na Serikali na kubainisha kwamba Vyuo Vikuu 40 kwa Tanzania kwa *population* ya watu milioni arobaini na Vyuo 51 kwa Kenya kwa *population* ya watu milioni thelathini na tisa; idadi ya watu wanaohitimu Tanzania ni wastani wa 9,150 kwa mwaka. Sasa ninamweleza Mheshimiwa Waziri, Kenya kuna idadi ya watu 25,000 kwa mwaka...

SPIKA: Tunaomba uulize swalii kuliko kutuhutubia.

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, ndiyo ninakuja katika swalii.

SPIKA: Maana yake muda ni mwingi mno.

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, linajengeka hivyo. Uganda kuna watu zaidi ya 17,000 wanaohitimu kwa mwaka wakati Tanzania tuna watu 9,150:-

(i) Je, uwiano huu uliopo Jumuiya ya Afrika Mashariki na hali yetu ya elimu ilivyo huoni hapo Tanzania tuko nyuma sana katika mipango ya elimu?

(ii) Mipango ya Milenia kuhusu *Primary Education* inaonekana Tanzania ikifika mwaka 2015 itaitimiza kwa sababu *enrolment* iko asilimia 92.7. Je, tunayo mipango ya Milenia au namna nyingine kuhusu kuweka elimu yetu ikifika 2015 – 2020 iwe juu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kulikuwa na tofauti kubwa katika uandikishaji wa Wanafunzi katika ngazi ya Sekondari na Elimu ya Juu kati ya Kenya na Tanzania na kwamba; idadi ya wanafunzi wetu ilikuwa chini sana ukilinganisha na Kenya. Tangu mwaka 2006, Serikali imechukua hatua kubwa sana ya kupanua elimu ya Sekondari na katika hatua tuliyofikia sasa, tunao wanafunzi wengi wa Sekondari wanaelekeea Elimu ya Juu kuliko wale walioandikishwa kwenye Sekondari katika Nchi ya Kenya. Hili la kwanza.

Pili, mwanzoni idadi ya watoto wetu walikuwa katika Elimu ya Juu walikuwa wamefikia aghalabu asilimia 2.7, hivi sasa wanafunzi wetu walioko kwenye Vyuo Vikuu wamefikia asilimia 5.4. Kwa hiyo, hivi tunavyokwenda tuko kwenye njia nzuri ya kufikia kiwango ambacho kitatufanya tuwe *competitive* na wenzetu wa Afrika Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nieleze wazi kwamba, ni kweli Kenya ina Vyuo Vikuu vingi ukilinganisha na Tanzania, lakini suala siyo wingi wa Vyuo Vikuu bali ni idadi ya watoto waliodahiliwa. Hivi sasa katika Vyuo Vikuu kama Chuo Kikuu cha Dodoma, kitakapokuwa kimefikia idadi yake ya wanafunzi 40,000, ndani ya Chuo Kikuu cha Dodoma kutakuwa na vyuo vitano, sita, saba, unavyovitaja vyenye idadi huko Kenya. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunapaswa tuyachukue kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kufikia yale malengo ya Milenia tuko njiani na tunakwenda vizuri kuyafikia. Ahsante sana.

Na. 82

Siku ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kuwa Mapumziko

MHE. AMINA N. MAKILAGI aliuliza:-

Tarehe 8 Machi ya kila mwaka Wanawake wa Tanzania na wengine Duniani kote huadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, siku ambayo hutoa fursa kwa Wanawake kutathmimi mafanikio na changamoto zilizopo katika suala la kumkomboa mwanamke kisiasa, kijamii na kiuchumi. Siku hiyo ni ya kazi na baadhi ya waajiri ambao ni wakorofi hawatoi fursa kwa watumishi Wanawake na hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu:-

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuweka tarehe 8 Machi kuwa siku ya mapumziko ili Wanawake wote wa Tanzania waweze kushiriki kikamilifu?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Siku ya Wanawake Duniani huadhimishwa tarehe 8 Machi kila mwaka na Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa, Tanzania ikiwemo. Madhumuni ya Maadhimisho haya ni kujenga mshikamano mionganoni mwa Wanawake na kuihamasisha jamii kuhusu utekelezaji wa kaulimbiu inayoambatana na Maadhimisho hayo kila mwaka. Suala la kuifanya siku hii kuwa

ya mapumziko ni utaratibu wa nchi husika kulingana na uwiano wa siku za mapumziko zilizopo nchini pasipo kuathiri uchumi.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kuwa, waajiri wengi wamekuwa wakiwaruhusu wafanyakazi wao 'Wake' kwa 'Waume' kujumuika na Wananchi wengine kwenye maadhisho hayo. Sambamba na hilo, hatujawahi kupokea malalamiko rasmi kutoka kwa wafanyakazi hususan Wanawake, kunyimwa fursa na waajiri wao ya kushiriki katika maadhisho hayo.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Wanawake wa Tanzania wamekuwa mstari wa mbele kufanya kazi kwa bidii na maarifa bila shuruti na pasipo malalamiko, kiasi cha kuwafanya hata washindwe kufikisha malalamiko yao Serikalini juu ya waajiri wenye tabia mbaya za kuwazuia Wanawake kushiriki Siku ya Wanawake Duniani ikiwa ni pamoja na majukumu mengine. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kuwaagiza waajiri wakorofi waweze kuwaenzi Wanawake hawa? (*Makof!*)

(ii) Kwa kuwa Wanawake wa Tanzania wamekuwa mstari wa mbele kufanya kazi kwa bidii na maarifa kiasi cha kuchangia na kukuza Pato la Taifa letu; na kwa kuwa Wanawake walio wengi hawapati muda wa kupumzika; je, Serikali inatoa kauli gani juu ya kufikiria siku hii iwe ya mapumziko bila kuathiri Uchumi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, tuko nyuma ya wakati.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Siku ya Wanawake inabidi tuitumie kwa ajili ya ku-*celebrate* mafanikio ya kichumi, kisiasa na kijamii, ambayo Wanawake tumeyafikia. Katika baadhi ya nchi kwa mfano; Zambia, Uganda, South Africa, China na Nepal ni siku ya mapumziko (*National Holiday*).

Mheshimiwa Spika, tukipata maombi rasmi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tutayapeleka Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu wao ndiyo wenye dhamana ya ku-*identify* siku gani iwe ya mapumziko.

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe angalizo tu kwamba, tuna siku nyingi sana; tarehe 16 Juni, Siku ya Mtoto wa Afrika; tuna Siku ya Familia; na tuna Siku ya Wanaume. Kwa hiyo, ni suala la kutazama ni vipi mapumziko hayo hayataweza kuathiri shughuli za uchumi. Nitoe tu rai kwa waajiri kwamba, Siku ya Wanawake Duniani, inabidi itumike kwa ajili ya kupima mafanikio tuliyoyafikia na changamoto zilizopo. Kwa hiyo, inapofika Siku ya Maadhisho haya, waajiri tuwaachie Wanawake na Wanaume washiriki katika kuadhishisha Siku ya Wanawake.

Na. 83

Watanzania Waliopelekwa Nje Kimasomo Kutoka Tanzania Zanzibar

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO aliuliza:-

Elimu ya Juu pamoja na Ushirkiano wa Kimataifa ni masuala ya Muungano:-

(a) Je, ni Watanzania wangapi waliopelekwa nje ya nchi kwa masomo waliotoka Zanzibar?

(b) Je, Watanzania wangapi waliopelekwa masomoni nje ya nchi kwa msaada wa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi rafiki; kati yao waliofotoka Tanzania Zanzibar ni wangapi?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa sasa wanafunzi wote wanaopelekwa nje ya nchi kwa ajili ya masomo ni wale tu wanaopata *scholarship* kwa ushirikiano wa kiutamaduni. Ushirikiano huo ni ume uliopo kati ya Tanzania na nchi marafiki/wafadhili au Mashirika ya Kimataifa pamoja na wale wanaoteuliwa chini ya *scholarship* zinazotolewa na Nchi za Jumuiya ya Madola.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inapokea *scholarship* kutoka Nchi za China, Russia, Poland, Czech, Cuba, Algeria, Uingereza, Australia, Oman, Misri, India na Serbia. *Scholarship* hizo hutangazwa katika vyombo vy ya habari kwa Watanzania wote wenye sifa zinazohitajika. Sifa hizo ni pamoja na umri na taaluma kulingana na mahitaji ya nchi husika, bila kujali waombaji wanatoka Tanzania Bara ama Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, maombi ya *scholarship* yanayopokelewa hayatenganishwi kuonesha sehemu ya Jamhuri anakotoka mwombaji. Hii ni kwa sababu wapo waombaji ambao ni Wazanzibari lakini wanaishi katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na hivyo kutumia anwani za Bara. Hali kadhalika, wapo waombaji wanatoka Tanzania Bara lakini wanaishi na kutumia anwani za Tanzania Visiwani.

(c) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwaka wa masomo wa 2011/2012 kuna jumla ya wanafunzi 603 wanaosoma katika nchi zilizotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati Ndogo ya Ushauri kuhusu masuala ya Elimu ya Juu na Mafunzo (*Sub-Advisory Committee on Higher Education and Training – SACHET*), yenye Wajumbe kutoka Bara na Visiwani, ndiyo Kamati yenye jukumu la kuchagua waombaji wenye sifa, kutegemea na idadi ya nafasi zilizotolewa. Wajumbe wa Kamati hii wanatoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Ofisi ya Rais (Menejementi ya Utumishi wa Umma), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*), Baraza la Mitihani la Tanzania, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (Dar es Salaam), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (Zanzibar) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu (Bara).

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Zamani kulikuwa na nafasi maalum ambazo zilikuwa zinaletwa Zanzibar kwa wanaokwenda nje kusoma. Kitu gani kilichokwamisha nafasi hizo kuendelea kuleta Zanzibar na wakateuliwa na Wazanzibari wenyewe kwa ajili ya kwenda kusoma nje?

(ii) Kwa nini mgao huu usifuate mgao wa fedha ambao unazingatiwa katika Muungano wa nne nukta tano?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, muda haupo upande wetu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tauhida Cassian Nyimbo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kuhusu nafasi maalum kutoka Zanzibar, ama nafasi maalum kutoka Tanzania Bara, hapa nimejieleza vizuri tu kwamba, mambo haya kidogo yanachanganya. Mambo ya elimu yanafuata sana sifa na umri kama nilivyosema. Kwa hiyo, nimesema kwamba, kuna Watanzania wa Tanzania Visiwani wanaoishi Bara, wana sifa za kwenda kusoma na wanapo-*apply* wanatumia anwani za Bara. Vilevile kuna Watanzania Bara wanaoishi Zanzibar, wanatumia anwani za Zanzibar lakini ni wa Bara, hivyo tunashindwa kujua hiki kiende hivi na kile kiende pale. Kwa hiyo, inawezekana kabisa hata wakati huo kulikuwa kuna nafasi hizo maalum, lakini baadaye tulipokuja kugundua tatizo lipo hivyo, ndiyo maana tukaona tutumie mfumo wa sifa kamili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya mgawo wa fedha, nitafuatilia nione hili lilikuwa vipi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, ninashukuru maswali ya msingi yote yamekwisha. Niwatangazie wageni tulionao hapa.

Wapo wageni wa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani, ambao ni Mheshimiwa niliyemtambulisha jana Mheshimiwa Abubakar H. Bakari, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar alikuwepo jana; yupo Bwana Hassan Rashid, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar; yupo Bwana Said H. Said, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar; yupo Bwana Hassan A. Haji, Mwandishi wa Sheria Zanzibar; yuko Bwana George Masaju, Naibu Mwanasheria Mkuu; yuko Bwana Joseph Ndunguru, Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria na yuko Ndugu Mathew Mwaimu, Mkurugenzi wa Katiba na Haki za Binadamu. Hawa ni watu wanaofanya kazi na Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba.

Tuna wageni wengine watatu wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Phillip Mulugo, ambao ni Viongozi wa Juu wa Umoja wa Mameneja na Wamiliki wa Shule na Vyuo Binafsi Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Mark Mringo, Mkurugenzi wa *Paradigms Schools*; ninaomba hawa wasimame walipo. Karibuni sana.

Wapo wanafunzi 60 kutoka Shule ya Msingi ya Mlezi Dodoma na walimu wao; hawa wako wapi? Ahsanteni sana, karibuni sana.

Tuna wanafunzi wengine 14 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo Dodoma; hawa wapo wapi? Ahsanteni sana, karibuni na msome kwa bidii.

Ninaambiwa kuna uwepo wa vijana watano wa Timu ya Vijana ya Yanga wamekuja kuonana na Wabunge walio Wanachama na Washabiki wa Yanga. Hawa wapo wapi? Wasimame hawa vijana wa Yanga. Kwa hiyo, washabiki wao mkutane nao mkitoka huko nje. Karibuni sana, tunafurahi kwamba ninyi ni Washindi wa Kombe la Kagame. Ahsante sana.

Nikisema hivyo basi wanasema Spika ni Yanga, kesho nikisema wanasema Spika ni Simba; basi ni vizuri. (*Makof!*)

Matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa kutakuwa na kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, kutakuwa na kikao leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa B.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kutakuwa na Kikao cha Kamati, saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa C. Wale walikuwa B na hawa C.

Katibu wa Umoja wa Wabunge Wanawake (*Tanzania Women Parliamentary Group*), Mheshimiwa Angella Kairuki, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote

kuwa, kutakuwa na Semina kwa ajili ya Wabunge Wanawake wote, leo tarehe 15, saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa John Mnyika, ye ye anaomba ni watangazie Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA kuwa, leo tarehe 15 baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu, kutakuwa na Kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Jengo la Utawala, Ghorofa ya Pili; kwa hiyo, wanaohusika wanaarifiwa hivyo. Waheshimiwa Wabunge, sijawabishia baada ya maswali kwa sababu sijaelewa hivyo wanavyofanya.

Tunayo *Supplementary Order Paper*; Katibu kwa hatua inayofuata.

KAULI ZA MAWAZIRI

Hali ya Usalama Katika Mikoa ya Mbeya na Tabora

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kutoa tamko la Serikali katika Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya usalama katika Mikoa ya Mbeya na Tabora.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kuwa katika hali ya utulivu na amani, licha ya matukio mbalimbali ambayo yamejitokeza siku za hivi karibuni katika baadhi ya maeneo ikiwemo Mikoa ya Tabora na Mbeya, ambayo yalionekana kutishia hali ya usalama wa nchi yetu. Matukio haya yamesababisha Wananchi, Makundi mbalimbali ya kijamii hasa Wanaharakati, wakitaka kujuu ni nini vyanzo vya matukio hayo. Serikali inatoa tamko kwa matukio haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mbeya: Katika kutekeleza agizo la Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya, mnamo tarehe 11 Novemba, 2011, majira ya saa 3.00 asubuhi, Askari Mgambo wa Jiji la Mbeya walikuwa eneo la Mwanjelwa lililoko Jijini Mbeya, wakifanya Zoezi ama Operesheni ya Kuwakamata Wafanyabiashara Wadogo Wadogo (Wamachinga), waliokuwa wamepanga bidhaa zao pembezoni mwa barabara katika eneo ambalo awali palikuwepo Soko Kuu lililoungua moto siku za nyuma. Askari Mgambo walikuwa wanatekeleza uamuvi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya, uamuvi wa Halmashauri ni kuwaondoa Wamachinga hao kutoka maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wakati zoezi hilo likiendelea, ghafla Wafanyabiashara Wadogo Wadogo (Wamachinga), pamoja na vijana, yaani watu wengine, waliweza kuwazingira Askari wa Mgambo hao kwa nia ya kupinga utekelezaji wa uamuvi huo wa Halmashauri. Nguvu ya vijana ilikuwa kubwa kiasi kwamba Mgambo hao waliwahi kupiga simu Kituo cha Polisi kuomba msaada.

Hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Jeshi la Polisi baada ya kupata taarifa hizo lilichukua hatua za haraka za kudhibiti vurugu hizo kwa kupeleka Askari kwenye eneo la tukio kwa lengo la kutoa msaada kwa Askari wa Mgambo waliokuwa wamezingirwa na kutuliza fujo na vurugu zilizokuwa zikiendelea;
- (ii) Fujo zilizagaa na kuenea maeneo mengine ya Jiji la Mbeya. Barabara ya Mbeya/Iringa ilikuwa haipitiki kwa muda kutohana na vijana hao kuweka vizuizi vya mawe na magogo barabarani, hii ililetu usumbu mkubwa kwa wananchi wetu;
- (iii) Kutohana na vurugu hizo Jeshi la Polisi liliwakamata jumla ya watu 350, baada ya kuwahoji na kufanya utambuzi, watu 34 walifikishwa Mahakamani kwa kosa la kufanya vurugu na wote walipewa dhamana;
- (iv) Jeshi la Polisi waliwasiliana na Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa. Tarehe 12, kesho yake, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa kushirikiana na Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, ulifanyika Mkutano

wa Wananchi wakiwemo Wafanyabiashara Ndogo Ndogo kuwataka wawe watulivu wakati tatizo lillopeleke vurugu hizo lilikuwa likitafutiwa ufumbuzi; na

- (v) Kupitia jitihada hizo zilizofanywa na Serikali na Mbunge huyo, hali ya utulivu na amani imerejeshwa na Wananchi wanaendelea na shughuli zao za kawaida.

Mheshimiwa Spika, madhara yaliyotokana na vurugu hizo: Katika vurugu hizo watu 15 walijeruhija kwa risasi na mmojawao alifariki dunia na watu 235 walihojija na Polisi kuhusiana na vurugu hizo. Kulikuwa kuna uharibifu na upotevu wa mali za wafanyabiashara, magari yalishambuliwa kwa mawe, matairia yalichomwa barabarani, Mabenki na Vituo vya Polisi vilivamiwa na hofu mionganoni mwa raia iliyosababishwa na vurugu hizo kiasi kwamba shughuli za uzalishaji zilisimama.

Mheshimiwa Spika, vurugu zilizotokea Mkoani Tabora: Mnamo tarehe 12 Novemba, 2011 majira katika saa 5.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni, ilioke vurugu zilizosababishwa na mmoja wa Askari wanafunzi wa Jeshi la Kujenga Taifa, Kambi ya Msange, akiwa na wenzake walikwenda katika eneo la Soko Kuu la Tabora kwa nia ya kufanya manunuzi. Alipofika kwenye moja ya maduka, alipenda nguo na aksauliza bei yake; alipotajiba shilingi 20,000, yule Askari Mwanafunzi hakuridhika na bei akataka apunguziwe, kitu ambacho mwenye duka hakuafiki. Kilichofuata, yule Askari aliamua kuondoka na nguo hiyo bila ya kulipa kwa kigezo kuwa inafanana na Sare ya Jeshi. Mwenye duka alimfuata na kupiga kelele kuomba msaada kwa wafanyabiashara wenzake ambaa walimsaidia kupata nguo yake. Askari huyo alikwenda kutoa taarifa kwa wenzake waliokuwa kwenye basi kwamba amevamiwa na kupigwa na wafanyabiashara. Askari hao walijikusanya, wakaingia sokoni na kuanza kuwashambulia wafanyabiashara. Hapo ndiyo ilipotokea vurugu kubwa.

Mheshimiwa Spika, madhara yaliyotokana na vurugu hizo ni uvunjifu wa amani uliodumu takriban saa tano, ambaa ulisababisha Wananchi wasiokuwa na hatia kupigwa na kujeruhiwa, uharibifu wa mali zikiwemo mali za wafanyabiashara, magari ya wapita njia, vibaka na watu wasiokuwa waaminifu kutumia fursa hiyo kuiba mali za wafanyabiashara na hofu mionganoni mwa Wananchi wa Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Polisi: Mara taarifa hizi zilipopatikana, Polisi walikwenda eneo la tukio kwa lengo la kudhibiti vurugu na fujo ambazo ziliikuwa zikiendelea na kutokana na hali halisi ya tukio, wallazimika kuongeza nguvu kutoka Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU). Jumla ya watuhumiwa 90 walikamatwa kuhusiana na vurugu hizo. Jeshi la Polisi lilifanya gwaride la utambulisho kwa nia ya kuwabaini Askari waliohusika katika vurugu hizo, ambapo Askari 51 walitambuliwa. Lilifanyika gwaride mara ya pili na Askari wengine tisa walitambuliwa na kufikishwa Mahakamani kwa kosa la kufanya fujo.

Mheshimiwa Spika, kwa kauli hii ya Serikali, ninaamini Watanzania wamefahamu vyanzo vya vurugu hizo. Kwa niaba ya Serikali, ninapenda kutambua mchango mkubwa wa baadhi ya wenzetu waliosaidia kurejesha amani katika matukio hayo. Tunatambua mchango mkubwa uliotolewa na Uongozi wa Mkoa na Wilaya Mbeya na tunatambua mchango wa raia wema wa nchi yetu ambaa hawakushiriki katika ghasia hizo. Pia tunatambua mchango mkubwa wa Ndugu Salmin, Mkoo wa Usalama wa Taifa Mbeya (*Regional Security Officer*), hekima na busara zake zilichangia sana kuleta ufumbuzi wa tatizo huko Mbeya.

Hali kadhalika, huko Tabora tunawashukuru Viongozi wa Mkoa huo; Mkoo wa Mkoa, Uongozi wa Wilaya na Mkoo wa Polisi Mkoa na timu yake, kwa kazi kubwa ya kudhibiti vurugu zilizojitekeza. Serikali inawapa pole Wananchi wote katika Mikoa ya Mbeya na Tabora, walioathirika kutokana na vurugu hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika Mikoa yote miwili ya Mbeya na Tabora ni shwari. Wananchi wanaendelea na shughuli zao za kila siku bila hofu na kwa amani. Vurugu haziwezi kuwa njia ya kuondosha migogoro au suluhisho la mifarakano. Nchi yetu inaongozwa kwa sheria

zilizowekwa, Viongozi wenyе ridhaа ya wananchi kama Madiwani, Wabunge na kadhalika. Ninasisitiza Wananchi tufuate sheria bila kushurutishwa na tuwe na uzalendo na mapenzi kwa Taifa letu. Vilevile ni vyema ikaeleweka kuwa, Serikali haitaendelea kuvumilia vitendo vya uvunjaji wa amani ya Taifa letu kwa makusudi; tunasisitiza utawala bora kwa misingi ya sheria ndiyo njia pekee. Shukrani.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Kuhusu nini Mheshimiwa?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa jambo hili kwa Mikoa hii miwili, lakini kumekuwa na hali ya kujirudia rudia na migogoro baina ya Wafanyabiashara Ndogo Ndogo maarufu kama Wamachinga maeneo mbalimbali ya nchi. Kumekuwa na matukio vilevile ya Wananchi kugombana na Vyombo vya Dola.

SPIKA: Mwongozo ni upi sasa; mwongozo siyo hotuba!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, siombi mwongozo ninaomba kutoa hoja na Wabunge wenzangu waniunge mkono kwamba kauli hii ijadiliwe.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Kanuni hii ya Kauli ya Mawaziri ni Kanuni ya 49(1) na (2): "Waziri anaweza kutoa kauli Bungeni kuhusu jambo lolote linaloihusu Serikali. Kauli za namna hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahususi, halisi na zisizouza mjadala na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini." Ninaamini kwamba, Waziri pia ametoa nyaraka hapa ndani, kwa hiyo, kama unataka ijadiliwe basi utaleta kwa utaratibu mwengine.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, jana wakati tunaanza kujadili Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Katiba, wenzetu wa CHADEMA walitoka na zipo taarifa kwenye vyombo vya habari ambazo zimeendelea kusema kwamba ...

SPIKA: Samahani; sijaelewa wewe unaniomba kitu gani?

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Ninaomba mwongozo chini ya kifungu cha 68(7). Wenzetu CHADEMA walitoka na zipo taarifa kwamba, hawataendelea kushiriki kwenye mjadala huu wa Muswada. Hivi punde umetangaza kwamba Katibu wa Wabunge wa Chama cha CHADEMA anawatangazia Wabunge wa CHADEMA kwamba, watakwenda kufanya mikutano baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu. Sasa mimi nikawa ninajuliza hivi Vyama vya Siasa vitakuwa vimeruhusiwa kwenda kufanya mikutano wakati mjadala unaendelea Bungeni? Pia nikawa ninajuliza hivi siku moja Chama cha Mapinduzi wakiomba idhini hiyo hiyo wataruhusiwa wakafanye mikutano wa Chama chao wakati Bunge linaendelea?

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Huu ni mwongozo muhimu sana. (*Kicheko*)

Kwa kawaida tumekubaliana hapa kwamba, mikutano itafanyika saa 7.00 mchana, baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu kwa woga huo huo kwamba, ikifanyika wakati tunapoendelea hapa inawezekana Bunge likawa wazi. Wale ambao wanataka kufanya kazi katikati baada ya maswali, kawaida wananiomba ruhusa na mimi kutegemea na umuhimu wa hicho kitu labda kinatakiwa kifanyike tuweze kupata nafasi ya kuendelea na shughuli zetu vizuri, ninatoa ruhusa kufanya mikutano hiyo baada ya Kipindi cha Maswali na Majibu.

Sasa Katibu wa CHADEMA hajaniomba, lakini hata mnavyosema wali-walk out, niliona wana walk out kama watu wengine wowote, wala sijaambiwa rasmi kwamba wana walk out kwa

sababu gani. Kwa hiyo, nilishangaa! Ukweli ni kwamba, siyo ruhusa kufanya mikutano ya aina nyingine yoyote, isipokuwa kwa ruhusa inafanyika baada ya saa 7.00 mchana. (*Makof*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 *(The Constitutional Review Act, 2011)*

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Mheshimiwa Angella Kairuki, nilikwita jana, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, halafu Mheshimiwa Hamad.

Wengine wanaenda kunywa chai, haya Mheshimiwa Kairuki nimeshakwita.

MHE. ANGELLA J. M. KAIRUKI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu ambao upo mbele yetu asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kabla sijatoa mchango wangu, ningependa ku-declare kwamba, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ambayo ilipewa kazi ya kuchambua na kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzishukuru Serikali za pande zote mbili za Muungano na hususan Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa dhamira yake ya kuruhusu mchakato wa Mabadiliko ya Katiba kuanza kupitia tamko alilolitoa katika hotuba yake ya mwisho wa mwaka aliyoitoa tarehe 31 Desemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, hakuna Katiba yoyote inayoweza kupatikana katika ombwe. Katiba zote ni matokeo ya historia, mazingira na wakati. Suala hapa si Rais kuwa na mamlaka na madaraka makubwa, bali tunapaswa kujiuliza ni katika mazingira yapi uamuzi huo wa kumpa Rais mamlaka ulifikiwa; na je, mazingira hayo bado yana uhalisia hadi kufikia leo hii?

Mheshimiwa Spika, misingi ya Katiba zote ulimwenguni ni maridhiano katika njozi na matarajio ya Taifa letu. Katiba si tu mkataba kati ya watawala na watawaliwa; huu ni mtazamo finyu.

Mheshimiwa Spika, tunapofikia kuadhimisha miaka 50 baada ya Uhuru wetu, tunao uwezo wa kutosha kwa Taifa letu kuwa na masuala ya msingi ambayo tunakubaliana nayo. Kwa kweli sote ni mashahidi, hakuna ambaye amelala njaa kwa kuwepo kwa Muungano, hakuna aliye kosa kwenda shule kwa kuwepo kwa Muungano na hakuna ambaye amekosa huduma muhimu za afya kwa kuwepo kwa muungano. Sidhani kama kuna ambaye amekosa pia masuala hayo niliyoyataja kwa Rais kuwa na madaraka makubwa na mamlaka maalum.

Mheshimiwa Spika, tusipotoshwe kana kwamba tunajenga nchi mpya. Inanishangaza na kunisikitisha kuona wale ambao wamekuwa wakijipambanua kama Wafuasi na Warithi wa Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa letu na ambao mara mara wamekuwa wakienda kutembelea Butiama kuzuru kaburi la Baba yetu wa Taifa, wamethubutu kumdhihaki Mwalimu Nyerere hapa Bungeni jana na mafanikio aliyoeweza kuipatia nchi yetu. Wamediriki pia kumbeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na wamediriki pia kulibeza Taifa letu mbele ya Bunge letu Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hansard ya tarehe 28 Juni, 1962, wakati Bunge lilipokuwa likipitia Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Mwaka 1962, Baba wa Taifa alisema; Katiba inayoishi ni ile iliyoko moyoni mwa watu. Lazima nchi yetu iweze kujenga maadili ya Taifa letu ili kumwezesha Rais wetu kusema nina mamlaka ya kufanya hili kwa mujibu wa Katiba na siwezi kufanya hili kwa kuwa huu si Utanzania. Endapo hatuna imani baina yetu sisi wenyewe, hawa wanaopinga mchakato huu wana imani na nani au wana imani zaidi na wakoloni wetu?

Ninashangaa pia kuona wanaosema kwamba nchi yetu inao Utawala wa Kifalme (*Imperial Presidency*), nikinukuu maneno ya jana ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani; hivi Marais wetu wanakaa bila kikomo kweli? Si wanakaa miaka kumi anaingia Rais mwingine? Waache kuwapotosha Watanzania. Hii ni Katiba ya Watanzania, wawaache Wananchi wawe na uhuru wa kutoa mawazo yao ili tuweze kufikia mabadiliko ya Katiba tunayoitaka. Hizi hakika ni kauli za watu waliosoma nusu nusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa kwa kuwa na mimi ni Mwanasheria, njikite katika uchambuzi wa Muswada. Katika Ibara ya 4(h) ya Muswada huu uliopo mbele yetu, yameainishwa makundi mbalimbali ambayo Tume itayafikia katika kutoa maoni yao. Yametolewa makundi mbalimbali ambayo ninayaafiki, lakini ningependa kutoa maboresho kidogo ili makundi mengine mbalimbali kama vile Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Wakulima, Vyama vya Wafugaji, Vyama vya Wafanyabiashara pamoja na Vyama vya Wavuvi, viweze kuongezwa katika Ibara hiyo ya 4(h). Pia ninapendekeza katika Ibara ya (8) kuhusiana na Hadidu za Rejea; ukiangalia katika Muswada huu inaonesha kwamba, Rais atatengeneza Hadidu za Rejea kwa ajili ya Wajumbe wa Tume.

Ninapendekeza Hadidu hizo za Rejea ziwepo katika Muswada huu kuitia Jedwali liliopo katika Muswada. Kwa nini ninasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu Hadidu hizo zitakapokuwepo katika Jedwali, zitamwezesha Mheshimiwa Waziri kuzifanyia marekebisho pale itakapobidi. Sishauri ziwekwe kwenye Muswada huu nje ya Jedwali kwa sababu zitakapokuwa nje ya Jedwali, marekebisho yake itabidi Bunge hili Tukufu liweze kuitisha na sote tunafahamu Bunge hili linakutana katika vipindi maalum na Tume hii inaanza kazi tarehe moja Desemba mwaka huu na mambo yanaweza yakajitokeza yakahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Ibara ya (9); ninaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa misingi hii iliyoainishwa katika Ibara ya 9(2). Huwezi ukampatia mtu kazi, usimpe misingi muhimu ambayo ataizingatia anapofanya kazi hiyo. Hakuna anayebisha kwamba, tunao mgawanyo wa madaraka baina ya Bunge, Mahakama na Serikali. Tunayo misingi pia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Wapo ambaa wamekuwa wakisema ibara ndogo hii ya pili, inawanyima watu fursa ya kuweza kutoa maoni yao, siyo kweli. Ukiangalia Ibara ya 9(3) inawapa Wananchi fursa ya kuweza kutoa maoni yao, yenye lengo la kuendeleza na kuboresha masuala hayo yaliyotajwa. Ibara ya 9(3)(i), inatambua uhuru wa kuabudu na uvumilivu wa dini nydingine. Ninapendekeza Kifungu hicho kisomeke uwepo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Serikali isiyokuwa na dini na inayoheshimu uhuru wa kuabudu kama ambavyo inaaainishwa katika Ibara ya 3(1) ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, niende katika ibara ya 14(2). Katika Ibara hiyo, Waziri wa Katiba na Sheria amepewa Mamlaka ya kuamua ni kiwango gani walipwe Wajumbe wa Tume. Ninapendekeza kwenye Kifungu hicho atakayeamua asiwe Waziri, bali walipwe kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Fedha zinazotumika katika malipo Serikalini. Katika ibara ya 16(a) tunaona kuna Mabaraza ya Mapitio ya Katiba ambayo yameainishwa katika ibara hiyo. Hata hivyo, kwa mujibu wa masharti ya ibara hiyo, Mabaraza hayo yatajumuisha Wananchi; ni jambo jema kwani ni hatua ya kwanza ya Wananchi katika kushiriki katika kuandika Katiba yao. Hata hivyo, kifungu hicho hakijaeleza ni lini Mabaraza hayo yataundwa na ni nani ataitisha Mabaraza hayo. Mabaraza hayo yatakapokutana yatajadili nini kwa wakati gani; na pia hakielezi Rasimu hiyo ya Katiba itapelekwa lini katika Mabaraza hayo ya Mapitio ya Katiba. Ninashauri pia Ibara hiyo iainishe Mwongozo utakaotumika katika kuuliza maswali kwenye Mabaraza hayo. Hivyo; ni lazima kuwe na taratibu na Kanuni zitakazoainisha namna Mabaraza hayo yatakavyoitishwa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia katika Muswada huu paainishwe Rais atakapowasilishiwa Rasimu hii ya Katiba ni wakati gani Wananchi watachapishiwa Rasimu hiyo ya Katiba ili waweze kutoa maoni yao kabla Rasimu hiyo hajapelekwa katika Bunge Maalum. Katika ibara ya 18 ni sahihi kabisa kwa Ripoti kuwasilishwa kwa Rais na kwa Rais wa Zanzibar kwani ni wao ndiyo walioiteua Wajumbe; hivyo ni vyema Ripoti hiyo ikawasilishwa kwao. Hata hivyo, kwenye Ibara hiyo

ninapendekeza marekebisheso kidogo badala ya Rais kumwagiza Waziri kuwasilisha Rasimu ya Katiba katika Bunge Maalum ahusike Mwenyekiti wa Tume na siyo Waziri.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia ielezwe ni baada ya muda gani tangu Rais kupokea maoni ya Tume, Rasimu hiyo itawasilishwa katika Bunge Maalum? Itabidi niruke kidogo niende kwenye ibara zingine muhimu hususan ibara ya 24(3) ambapo inaeleza utaratibu maalum utakaotumika katika kupitisha Rasimu ya Katiba. Ibara hii ni vyema ikalipa Mamlaka Bunge Maalum, kijiwekea utaratibu wake kuhusiana na namna itakavyopitisha Rasimu ya Katiba na Masharti kuhusiana na namna Rasimu hiyo ya Katiba itakavyoungwa mkono badala ya theluthi mbili iliyoko hivi sasa katika Muswada huu. Katika Ibara ya (5) kunapaswa kuwa na ibara ndogo itakayoruhusu kuwa na Sheria za Mpito pamoja na marekebisheso mbalimbali yanayoweza kufanywa na Sheria zilizopo, yaani *consequential amendments, transition and saving provisions*, kwani hivi sasa kwa Muswada ulivyo kuna ombwe kubwa na haupo wazi masuala haya ya mpito yatashughulikiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25(2) inatoa Kinga na Uhuru wa Mawazo na Majadiliano kwa Wajumbe wa Bunge Maalum. Ibara ya (100) inayotajwa na Sheria ya Kinga ni kwa ajili ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. Hivyo, ninashauri Sheria mahususi iweze kuletwa Bungeni kwa ajili ya kutoa kinga kwa Wajumbe watakaohusika katika Bunge hilo Maalum. Pia ni vyema ukaletwa Muswada Maalum, utakaofanya marekebisheso katika Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuweza kuruhusu Mchakato wa Kura ya Maoni utakaoweza kutumika katika Mchakato huu wa Mabadiliko ya Katiba na pindi fursa zitakapojoitokeza katika masuala mengine mbalimbali, kwani tunaona hata wenzetu wa Zanzibar pia wanayo Sheria mahususi kwa ajili ya uendeshaji wa kura ya maoni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza, nililezea misingi ambayo Tume inatakiwa izingatie katika kufanya kazi. Ukiangalia Ibara ya (25), hajaaeleza Bunge hili Maalum litakapokuwa linatekeleza majukumu yake ya kupitia Rasimu hii ya Katiba, litazingatia masuala gani muhimu? Pia ni vyema misingi ile ikaainishwa katika ibara inayohusu majadiliano ya Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu pia hajaaelezwa gharama za Bunge Maalum zitatoka wapi wakati gharama za Tume zimeelezwa zitatoka wapi na hiyo ni kwa mujibu wa Ibara ya (14). Kwa hiyo ni vyema waainishe iwe wazi. Katika ibara ya 29(2) tunaoneshwa kutakuwa na Elimu ya Uraia na Uhamasishaji wa upigaji wa kura ya maoni; ni vyema Muswada huu ukaeleza elimu hiyo itatolewa katika kipindi gani na katika kipindi cha siku ngapi? Mfano, katika Ibara ya (32), Muswada unahitaji kufafanuliwa zaidi, kwa sababu ulivyo hivi sasa unachanganya. Ibara ya 32(2) inatoa takwa la kuungwa mkono na zaidi ya asilimia 50 toka kila upande; wa Zanzibar na upande wetu wa Bara, lakini hajaaeleza endapo Tanzania Bara tumefikia asilimia 55 na endapo wenzetu wa Zanzibar hawajafikisha asilimia 50 ni nini kitafuata? Kwa hiyo ni vyema tusiache wazi tukaacha ombwe kama hilo, tuyafunike. Ibara ya 32(4) inaeleza endapo kutakuwa na wingi wa hapanana tutarudi kwenye Katiba hii ya sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kupata fursa hii na mimi kuwa sehemu ya shughuli hii muhimu ya kupitia Sheria ambayo itasaidia kutunga Katiba Mpya. Tunapokuwa tunaadhimisha Miaka 50 ya Uhuru ni muda mwafaka kuangalia tumetoka wapi, tulipo na tunaelekewa wapi. Chombo hiki kwa maana ya Katiba ambacho tumekuwa tunakitumia katika safari yetu hii ni muda mwafaka kuangalia kama kweli kinahitaji service au tunahitaji kukaa na kukibadilisha ili tuweze kuendelea na safari yetu.

Mheshimiwa Spika, ninataka nitoe angalizo, Wananchi wetu wamekuwa waelewa sana na wanafatilia kwa umakini kabisa shughuli ambazo tunazifanya ndani ya Bunge letu hili. Nami nikiwa Mwakilishi wa Wananchi na mimi nina uchungu wa nchi hii, tusingependa kufanya mambo ambayo ni kinyume na matakwa ya Wananchi na mambo yasiyokuwa na maslahi kwa Taifa hili. Ninadhani wote tunaungana kimsingi kwamba, tunahitaji Katiba Mpya. Tutumie fursa hii, kwa kujadiliana kwa marefu na mapana, muundo wa Katiba Mpya tunayoihitaji. Nitoe rai kwa Wabunge wenzangu na Wananchi kwa ujumla kuwa, tusijadili Muswada huu wa Mabadiliko ya

Katiba kwa kuangalia Itikadi vya Vyama vyetu wala kwa kuangalia Udini, Ubara na Uzanzibari na wala Ukabila. Tuweke Utaifa mbele; tukifanya hivi tutafika safari yetu salama.

Mheshimiwa Spika, ninapata tabu sana kuona sasa hivi kumetokea madalali wanaotaka kuchukua umaarufu au kujipatia umaarufu katika suala la Katiba na wengine kutaka kuhamasisha vurugu na fujo katika suala hili la Katiba. Mimi ninaomba nitoe rai, tuwe na nguvu za hoja na siyo hoja za nguvu. Wanaohamasisha fujo na vurugu tuwakatae na tuwapuuze. Ninashangaa sana, kama mimi binafsi kuna hoja ambazo siafikiani nazo katika ngazi ya Kamati, ningekataa kushiriki katika zile Kamati. Vilevile kama sikubaliani na hoja hiyo, ningekataa kuwasilisha. Kwa wale waliokuwa wanaona kwamba hii hoja hawaiungi mkono hata uwasilishaji wa hapa nao wangekataa, lakini wameshiriki katika Kamati, wameleta mapendekezo yao; inashangaza baada ya hapo watu hao wanatoka nje. Kimsingi, unapowasilisha Bungeni na unaposhiriki katika Kamati, inamaanisha kwamba wewe unakubaliana na mchakato ule. Niwashi ndugu zangu wa Upinzani, hoja za msingi tutazijadili hapa, tusiwanyime Wananchi fursa ya kutoa mawazo yao na maoni yao. Wametuchagua kuja kuwasilisha mawazo yao hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchakato huu tunaoufanya ni mdogo, kuna mambo makubwa ya msingi ambayo yanatupasa kujadili na yatakuja katika hatua zinazokuja; kuna masuala ya matumizi ya rasilimali ya nchi yetu; masuala ya ardhi; masuala ya madini; masuala ya gesi; na kuna masuala ya mafuta. Hatunufaiki na hivi vitu, sasa tunatakiwa tuweke katika Katiba jinsi gani Wananchi wa Tanzania wanaweza kukaa na kunufaika na mali hizi. Vilevile kuna masuala ya Mikataba ambayo imekuwa inalalamikiwa mara kwa mara.

SPIKA: Mheshimiwa Ndugulile, kwa maana ya Muswada huu, hayo yatakuja kama Muswada huu utapita basi Wananchi ndiyo watapata fursa hii ya hayo unayoyasema. Sasa hivi jielekeze kwenye hili.

MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE: Mheshimiwa Spika, ndiyo huko nilikokuwa ninaelekeea kwamba, baada ya mchakato huu hayo ndiyo masuala makubwa ya msingi ambayo Wananchi watataka wajadili. Vilevile masuala ya Madaraka na Mamlaka ya Rais, masuala ya Muundo wa Serikali wenye tija na manufaa kwa Wananchi wa Tanzania, ushiriki wa vijana na akina mama na uwajibikaji wa Serikali kwa Wananchi. Hayo ndiyo masuala makubwa ya msingi ambayo Wananchi wangependa kuyajua. Vilevile kuna mambo mengine ambayo yameanza kujitokeza; hivi karibuni tumepewa masharti kwamba, tukihitaji misaada kutoka nje ya nchi lazima tuweke vigezo vya aina fulani kwa ajili ya masuala ya haki za binadamu. Hayo nayo yanaweza kuja na tutapata fursa ya kuyajadili wakati huo.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna watu wamekuwa wanahoji kwamba, mchakato huu utawanyima Wananchi ushiriki katika suala hili zima, lakini mimi binafsi ninaona tutapata fursa nzuri tu. Kwanza, katika mikutano ya kutoa maoni; pili, ushiriki katika Bunge la Katiba; na tatu katika kura za maoni. Hizo ni fursa tosha kwa Wananchi kuweza kutoa maoni yao na kusema yale ambayo wanadhani yanawagusa. Sasa kuna malalamiko mengine kwamba Rais ana mamlaka makubwa sana, lakini kwa hadidu za rejea ambazo tumeziweka na vifungu vipyta ambavyo vimewekwa, Rais tumembana kwa kiasi kikubwa sana. Tumempa maelekezo, kwa hiyo ile hofu kwamba Rais amepata madaraka makubwa sana, mimi sioni kama yana tija sana. Tumemweleza kwamba, idadi ya Wajumbe iwe kiasi gani, tumempa hadidu za rejea na sifa. Sasa wale wanaopinga mimi ninashangaa sana wanapinga kitu gani.

Mheshimiwa Spika, niongezee hapo; kwa wale waliokuwa wanasema kwamba Urais wetu sisi ni wa Kifalme, ninadhani kuna watu wanahitaji kwenda nchi za jirani waone Urais wa Kifalme maana yake nini. Kuna nchi jirani hapa ambayo sitaitaja, Mke wa Rais ni Waziri, Mtoto wa Rais ni Mkuu wa Kitengo cha Usalama na Kaka wa Rais alikuwa ni Waziri. Sasa katika Baraza letu la Mawaziri, mimi sijaona Mke wa Rais wala Mtoto wa Rais kuwa Waziri. Sasa haya mambo ndiyo watu wanayapotosha pasipo na msingi wowote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kidogo katika maoni ya jumla kuhusiana na vifungu vya Muswada huu. Kifungu cha 13(6) kimeongelea Watendaji wa Serikali ambao wataingizwa katika Sekretarieti, lakini hakijataja kiwango. Ninataka tuweke kiwango maalum. Wasiwe wengi

zaidi ya 20 na wasizidi 30 ili tupate timu nzuri ambayo itatupunguzia gharama lakini ambayo itakuwa na tija. Kifungu cha 18(2), kimeeleza kwamba, Tume itawasilisha taarifa yake kwa Rais na baada ya hapo, jukumu la kuwasilisha ile Rasimu ya Katiba, litafanywa na Waziri. Mimi ninataka nipayendekeze hili na ninaungana na msemaji aliyeppita kwamba, jukumu hili kwa sababu limekabidhiwa Tume, basi iwe ni Tume hiyo hiyo ambayo itawasilisha mapendekezo hayo kwenye Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, ombi hili limetoka kwa Wananchi wa Kigamboni, wanasema kuwa baada ya Tume ya kukusanya maoni na kutoa mapendekezo, wanataka kabla hajapelekwa katika Bunge Maalum la Katiba, Wananchi nao wangependa wapate tena fursa ya kuitia hiyo Rasimu. Hilo ni ombi ambalo Wananchi wa Kigamboni wametaka niliseme.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kifungu cha 18, kinachoongelea kwamba baada ya Rais kupokea ile taarifa kuna mchakato ambaeo utaendelea pale; hajjaainishwa kwamba ni mchakato gani na itakuwa kwa muda gani. Sasa katika hili, nilikuwa ninaomba sana kwamba, huo mchakato uelezwe na uweke bayana ni kitu gani ambacho kitafanyika pale na upewe muda maalum.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 20, ushiriki wa Wabunge na Baraza la Wawakilishi umewekwa wazi, lakini kupata wale Wajumbe wengine ambaeo watakuwa katika Bunge la Katiba haujawekwa wazi. Katika hili na mimi ninataka nitoe pendekezo kwamba, ule utaratibu wa kuwapata wale Wajumbe wengine watakaojazia katika Bunge la Katiba uwekwe wazi na itolewe fursa ya jinsi gani hawa watapatikana ili tupate uwakilishi mzuri na wenye tija katika hilo Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu cha 24(3) ambacho kinasema kwamba, Maazimio ya Bunge la Katiba yatapitishwa kwa idadi ya theluthi mbili. Sasa hapa ninaona tutakuwa tunaingilia mamlaka ya Bunge la Katiba. Mimi ninataka kutoa wazo kwamba, Bunge la Katiba lipewe uhuru wa kujadili na kuunda kanuni zake za jinsi gani ya kukaa na kuitisha Rasimu ya Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 27, badala ya Tume ya Uchaguzi kukaa na kusimamia zoezi hili, nilikuwa ninataka kutoa ushauri kwamba, kiundwe chombo huru ambacho kitasimamia na kuratibu zoezi la kura za maoni.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho ni kwamba, majukumu ya Wanasheria Wakuu wa Zanzibar na Tanzania Bara ni kutoa ushauri katika masuala ya kisheria kwa Serikali. Sasa, kuna vifungu ambavyo vinaleesa kwamba, watashiriki ama kutoa maoni, kumshauri Rais katika uundaji wa Tume na Wajumbe wa Bunge la Katiba. Mimi nilikuwa ninaona tuwaondoe hawa kwenye majukumu haya ili Rais apate fursa kwa vile vigezo ambavyo tutakuwa tumemuwekea ili apate uhuru wa ye ye kuchagua wale ambaeo anadhani wanafaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, hii ni fursa nzuri kwetu sisi Watanzania na ninashukuru kuwemo ndani humu kushiriki katika mchakato ambaeo utapelekeea kuwepo na Katiba Mpya. Niwaombe sana Watanzania kwamba, suala hili tusilichukulie kwa jazba, tusiliangalie kwa itikadi na tusiangularie kwa Uzanzibari wala Ubara; suala hili tuliangularie kwa Utaifa wetu na tunataka kulipeleka wapi Taifa letu. Tukifanya hivyo, tutafika safari yetu salama.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. (*Makofii*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza, ninaomba nichukue nafasi hii ya mwanzo kabisa, kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa msimamo wake juu ya kauli ya Waziri Mkuu wa Uingereza, ambayo inafedhehesha utu wa binadamu. (*Makofii*)

Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru pia Wananchi wa Igunga kwa kuendelea kuamini na kutambua ukweli kwamba, bado ni Chama cha Mapinduzi pekee ambacho kinaweza kutoa uongozi wa kuaminika kwa Taifa letu. Ninawapongeza sana walioshindana nasi ambao wamekubali kushindwa. Ninataka wale waliokubali kushindwa na wale tulioshinda tuendelee kuwapa darasa wale ambao bado wanatafuta kuivuruga amani ya nchi yetu kwa sababu ya maslahi binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Taifa letu linapata fursa nyingine na ya pekee ya kuandika upya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa Wasomi na Wanasheria waliobobeaa masuala ya Katiba, fursa hii ni adimu na ni lulu ambayo ikitumika kwa namna chanya inaweza kuleta mapinduzi makubwa ya kuwapa Watanzania Katiba inayoweza kuwafaa kwa wakati uliopo na inayoweza kuendelea kuwafaa kwa miaka zaidi ya 50 mingine ijayo. Vilevile ni kweli pia kwamba, ikitumika kwa namna hasi, inaweza ikawa ndiyo mwanzo wa kuvuruga amani na utulivu katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo hayana mbadala. Amani katika nchi yetu haina mbadala, Umoja wa Kitaifa hauna mbadala, uwepo wa Watanzania na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hauna mbadala. Katika hili nilitarajia sana Wabunge wa Bunge hili wangkuwa wa kwanza kutambua hili, maana nje ya Tanzania hakuna Bunge la Tanzania. Nje ya Tanzania unaweza kuwa na Bunge la Tanganyika, unaweza kuwa na Bunge la Zanzibar, mnawenza mkaapaska mkaenda vipande mkawa na Bunge la Simanjiro, Bunge la Singida, Bunge la Manyara, Bunge la Singida, lakini si Bunge la Tanzania. Kama Bunge la Tanzania mnapaswa kuanzisha mchakato utakaowapa Watanzania Katiba Mpya na si vinginevyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninasema hili kwa sababu watu wanataka kuharibu historia. Kwa mara ya kwanza nimemiskia msomi na mtaalam wa sheria kama anavyojiita na kama anavyotambulika, Mheshimiwa Tundu Lissu, akiwalaghai na kuwadhihaki Watanzania na kudhihaki historia ya Taifa letu kwa kumbeza Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa maneno yafuatayo: Ukurasa wa 12 wa hotuba yake anasema; "Ukuza ji na uhifadhi wa haki za binadamu ulikataliwa na Serikali ya Mwalimu Nyerere kwa miaka yote ya utawala wake." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninataka niwahakikishie Watanzania, Mheshimiwa Tundu Lissu ni Mwanasheria, ukienda katika ukurasa wa 20 wa Katiba kama unayo kama hii ya kwangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukienda ibara ya 12, haki ya usawa ipo kwa mujibu wa Sheria Na.15 ya Mwaka 1984. Nani alikuwa Rais wa Tanzania kama siyo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere? Nenda katika ibara ya 13, watu wote ni sawa mbele ya sheria, imewekwa kwa mujibu wa Sheria Na.15 ya Mwaka 1984. Aliyekuwa Rais wa nchi hii ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Nenda ibara za 15, 16 na 17, nenda mpaka kwenye haki za uhuru, zote utakuta zimebekwa kwa mujibu wa Sheria Namba 15 ya Mwaka 1984.

Ukianza mwanzo wa Ibara ya 12 mpaka Ibara ya 28, 29 na 30, misingi yote ile ya haki za binadamu imewekwa wakati wa Uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kwa mujibu wa Sheria Namba 15 ya Mwaka 1984.

Mheshimiwa Spika, ninataka nimwombe Mheshimiwa Tundu Lissu arudi darasani katika hili ili ajue kabisa kwamba Hati ya Haki za Binadamu imewekwa chini ya Uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, katika hotuba yake ukurasa wa 17, Mheshimiwa Tundu Lissu anasema: "Mwalimu Nyerere alimomonyoa Uhuru wa Zanzibar kwa kuongeza orodha ya Mambo ya Muungano kwenye Katiba ya Muungano."

Mheshimiwa Spika, ninamtaka Mwanasheria huyu na Mbunge mwenzetu arudi darasani. Kwa nini? Kwa sababu ukitaka masuala yote ya madaraka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, masuala yote ya Muungano yaliyoko kwenye orodha ya pili, nyongeza ya pili, ambayo yako kwenye ukurasa wa mwisho wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lazima yaamuliwe kwa theluthi mbili ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanaotoka pande zote mbili za Muungano. Hakuna namna unayoweza kumomonyoa madaraka na Uhuru

wa Zanzibar ndani ya Bunge hili kwa sababu ni lazima upate theluthi mbili ya Wazanzibari walioko kwenye Bunge hili na lazima upate theluthi mbili ya Watanzania Bara walioko kwenye Bunge hili. Kumtuhumu Baba wa Taifa kwamba alimomonyoa Uhuru wa Zanzibar ni kumtukana Mwalimu, kulitukana Taifa hili na kuibezza Historia ya Tanzania. Mtu huyu anapaswa kupuuzwa kwa kiwango ambacho hakina mfano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninataka nikumbushe tena Historia ya Taifa letu na historia ya nchi yetu; nchi yetu ni Muungano wa nchi mbili za iliyokuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika. Katika kubadilisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano, yapo mambo ambayo lazima uwe nayo akilini kwamba unapotaka kubadilisha Katiba ya nchi hii ni lazima utambue uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na uwepo wa nchi iliyokuwa inaitwa Zanzibar na uwepo wa nchi iliyokuwa inaitwa Tanganyika. Katika mazingira hayo, ukitaka kubadilisha Katiba na kuandika Katiba upya, wabia wote hao wawili wa Muungano katika mazingira ya haki wala siyo ya upendeleo, wanakuwa na haki sawa ya kujadili juu ya umoja wao na mustakabali wa Taifa lao. Katika hili, ninamwomba tena apate *tution* na sisi tuko tayari kwa ajili ya darasa hilo bila kulipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mawili nimeamua kuyagusia ambayo yanamhusu Baba wa Taifa ili kuweka historia vizuri na lazima nirudie pia kusema tunafanya kazi ambayo hatima yake ni kuipatia Tanzania Katiba mpya. Wapo ambao wanasesma ni lazima kubadilisha ibara ya 98 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili tuweke sheria inayoanzisha mchakato. Ninataka niwaambie, taratibu zote na historia ya Mabunge yote Duniani na Katiba zote Duniani, hakuna Katiba inayoweka tarehe ya kufa kama ambavyo hakuna binadamu anayejua tarehe ya kufa. Wananchi ambao ndiyo msingi wa mamlaka yote, wanapohitaji kutunga Katiba mpya, hawahitaji kupewa mamlaka ya kufanya hivyo kwa kuwa wanapohitaji kufanya hivyo wanakuwa juu ya Katiba ya nchi inayohusika.

Ukitaka, nenda katika kesi iliyofanyika hivi karibuni wakati wenzetu Kenya walipokuwa wanataka kubadilisha Katiba yao, walikuwa na kifungu kinachofanana na kifungu cha 98 cha Katiba yetu, hawakutunga sheria na baadaye walikwenda Mahakamani na Mahakama ikasema Wananchi wako juu ya Katiba na hawawezi kutungiwa masharti na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya nchi yao, kwa sababu marekebisho ya Katiba yanafanywa na Bunge kwa mujibu wa Katiba, lakini uandikaji upya wa Katiba, mamlaka yake yako kwa Wananchi. Ninawataka wasioliju hili, warudi darasani wakajifunze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninataka nichukue nafasi hii tena kukumbusha baadhi ya misingi mikuu ya Kitaifa ambayo imehifadhiwa kwa mujibu wa ibara ya 9(2) ya Muswada huu. Katika hili ningependa sana niwaambie wenzangu, mimi kwa bahati nzuri Mheshimiwa Spika ulinituma na kuniweka katika Kamati ya Katiba na Sheria kwa mamlaka uliyopewa na Kanuni za Bunge; ninakupongeza kwanza kwa uvumilivu wako na ambavyo unaweza kustahimili hata haya madongo mengine ambayo hayana nafasi na ambayo wakati mwingine yanafedhehesha na kudhalilisha Kiti cha Spika, ambayo yanatolewa na watu ambao wanashindwa kutii mamlaka yaliyowekwa wakati mwingine na Mungu kuititia kwa wanadamu wake.

Mheshimiwa Spika, Misingi hiyo Mikuu ya Kitaifa inayopaswa kuhifadhiwa na kuendelezwa ni hii ifuatayo:-

Hili ni vizuri Watanzania wakaelezwa, nimwombe sana Waziri wa Katiba na Sheria aeleze hili lieleweke; tunaposema misingi mikuu maana yake ni kuwepo kwa Jamhuri ya Tanzania, hilo ni la kwanza. Hivi tukisema kwamba Tume ya Uchaguzi itaendelea kuhifadhi na kuendeleza kwamba Watanzania wajadili, lakini haya mambo mionganoni mwa mambo yanayohitajika kuhifadhiwa ni pamoa na Jamhuri ya Muungano. Hatimaye mchakato wote na baadaye Wananchi watakapokwenda kwenye *Referendum* ni kupata Katiba ya Jamhuri ya Muungano mpya. Nje ya kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano unamtungia nani Katiba? Maana Bunge la Katiba litakaloundwa ambalo litaitwa Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *Referendum* itakayokwenda ambayo Watanzania watapata nafasi ya kutoa kura yao ya uamuzi au ya maoni, vyovyyote utakavyopenda kuiita, hatimaye itatoa kitu kinachoitwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima iwepo.

Mheshimiwa Spika, lingine, tumesema, mionganoni mwa mambo ambayo yanapaswa kuhifadhiwa ni uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini isiyokuwa na dini na inayoheshimu uhuru wa kuabudu. Hili nani anakataa; kila mtu ana dini yake, lakini nchi kama nchi haina dini. Hili nalo wenzetu hawataki kuliona. Uhifadhi wa haki za binadamu hili wanalikubali, lakini ndiyo hilo ambalo wanatumia kumdhihaki Baba wa Taifa. Ninataka niwaambie orodha hiyo iliyowekwa kwenye ibara ya (9) ni mambo ya msingi kwa faida ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ili niende kwenye vifungu; kuna suala zima la uundaji wa Tume. Muswada unasema, Rais baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar na kama ilivyo kwenye ibara ya (5), Rais atashauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar na kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Ushauri wangu; Wanasheria hawa wawili wapo kwa mujibu wa Katiba; kwa mfano, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano yupo kwa mujibu wa ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kazi yake ni kuishauri Serikali katika masuala ya sheria. Ningependa na Mwanasheria wa Zanzibar ambaye yupo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, jukumu lake pia ni hilo. Hawa hawana nafasi katika nafasi hii ya uteuzi wa Tume kwa sababu zifuatazo:-

Moja; Rais kwa mujibu wa ibara ya 33 amepewa mamlaka yeye ni Mkoo wa Nchi, yeye ni Mkoo wa Serikali, yeye ni Amiri Jeshi Mkoo. Kwa hiyo, yeye kama Mkoo wa Nchi anapata fursa ya kuiteua Tume ya Kukusanya Maoni na anapata pia nafasi ya kuwateua wale Wajumbe wengine walioko kwenye Bunge la Katiba. Mamlaka haya ya Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar, yasingepaswa yaingiliwe na mtu mwingine yejote.

Rais ni Taasisi; Mwanasheria Mkoo au Wanasheria Wakuu wabaki kuishauri Serikali katika masuala ya kawaida ya kisheria lakini siyo katika kuandaa Orodha ya Wajumbe wa Tume. Ningependa hili liangaliwe sana na liondolewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika ibara ya 24 lipo suala zima la namna ya kupitisha masharti ya Katiba katika Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge hili Malum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lipo juu ya Bunge hili kwa niaba ya Watanzania, lipo juu ya Katiba ya sasa, limepeewa mamlaka ya kujitungia kanuni zake za namna ya kujidhesha. Rai yangu na ushauri wangu juu ya utaratibu utakaotumika katika uendeshaji wa Bunge hili, iamuviwe na Bunge Maalum la Katiba lenyewe na siyo sisi kultungia masharti Bunge hilo, maana itakuwa ni kuingilia mchakato wa namna ya kupanga Katiba inayokuja na hapo tutautia doa mchakato mzima. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba, hili nalo lifanyike kwenye Kanuni za Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia tukumbushane baadhi ya mambo mengine ya msingi katika eneo ambalo kura za maoni zimepigwa na inahitaji zaidi ya asilimia 51 ya pande zote mbili za Muungano; ni vizuri Muswada huu ukaainisha kwamba, endapo hutapata zaidi ya nusu ya kura kutoka upande mmoja wa Muungano nini kitatokea. Maana Muswada wa kwanza unaonesha kwamba, tunarudi kwenye Katiba tunayoitumia sasa ya mwaka 1977. Bado rai yangu iko pale pale kwamba, iainishwe hivyo hivyo ili kama hilo nalo likikataa kwa upande wowote, turudi kwenye Katiba ya sasa ambayo ndiyo tunayoitumia, maana nchi haiwezi kukaa bila kuwa na Katiba ambayo inaweza kusaidia kuleta uongozi bora katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu, Katiba ni Waraka wa Kisiasa unaowezesha Wananchi kujitambua kama Taifa. Katiba vilevile ni Sheria Mama katika nchi ambapo ni chimbuko la sheria nyininge zote zinazotungwa katika nchi hiyo. Kwa hiyo, ni fursa ambayo Watanzania wanayo huko mbele tunakoenda.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa pia niligusie ni juu ya upotoshaji unaodaiwa kwamba hivi sasa tunatunga Katiba. Ningependa Watanzania waelewe katika hili kwamba, tunachotunga sasa hivi ni Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ambayo lengo lake ni kuweka Tume itakayoratibu na kukusanya maoni ya Watanzania; ni sheria itakayoweka utaratibu wa kuwepo kwa Bunge Maalum la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ni sheria itakayoweka utaratibu wa kuyaweka maoni hayo baada ya Bunge Maalum la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kupitisha; basi Watanzania wachukue nafasi yao ya kawaida ya mamlaka ambayo wanayo ya kutoa maoni yao juu ya Katiba wanayoitaka. Kwa hiyo, katika hili ni vizuri wenzetu wakaacha kuwapotosha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaheshimu sana maoni na mimi ninataka kuheshimu sana maoni ya wadau wengine wote. Kamati yako ilipata fursa ya kuwapata magwiji waliobobe katika eneo hili. Tulipata nafasi ya kukutana na Profesa Kabudi, Profesa Shivji, Mheshimiwa Warioba, Msajili wa Vyama vya Siasa na Wataalam wengine wengi sana wakiwemo watu wa *Legal and Human Rights Centre* walitoa maoni yao. Mwisho, wenye kuandika au kupitisha au kutunga Sheria ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ukichukua maoni ya Majaji Wastaifu, hayawezi kufanana na maoni ya Mheshimiwa Warioba, hayawezi kufanana na maoni ya Profesa Shivji na maoni ya Profesa Kabudi hayawezi kufanana na maoni ya *Legal and Human Rights Centre*. Kwa maana hiyo, lazima Bunge hili litunge sheria hii kwa jinsi linavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ninaomba Watanzania waendelee kutulia wakijua nchi yao iko salama.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza nikuombe radhi jana nilikuwa nimefunga, kwa hiyo, nilikwenda kufuturu sikukimbia Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kusema kwamba, msingi wa Bunge lako Tukufu kutunga sheria, kupitisha sheria linatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo sisi sote kabla ya kuanza kazi tulikula kiapo na kuilinda; nitashangaa sana mionganini mwetu kitu ambacho tumekula kiapo nacho na hatimaye tunashindwa kutembea kwenye kiapo chetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika Katiba hii sikuona mahali popote ambapo pameandikwa kwamba, hapa tuna mfalme, tuna dikteta, wala tuna nani! Sasa anapokuja kiongozi ambaye amekula kiapo kuilinda Katiba, ukawapotosha Watanzania ambao ndiyo waliokuteua kuja hapa ukala kiapo, ni dhambi ambayo haiwezi kusameheka hata kidogo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hilo lilikuwa jambo la kwanza. Lakini jambo la pili baya zaidi, ni kudharau na kutothamini mchango wa watu wengine, Wazanzibar kwa umaja wao walipiga kura ya maoni, wakakubali kwamba wao katika mazingira walijonayo wanahitaji wakati wowote Chama kinachoshinda kishiriki katika Serikali na kile ambacho kimeshindwa, ni maoni ya wananchi wa Zanzibar kwa asilimia 64. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, katika Katiba hii sehemu nyiningine imo Katiba ya Zanzibar na umekula kiapo hapa, halafu unakwenda kudharau raia wenzako! Halafu wewe unajifanya eti ndiyo mkombozi wa watu, mkombozi gani wa watu unaowadharau? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baya zaidi, nimesema kwa sababu limesemwa ndani ya Bunge lako Tukufu, ukurasa wa 20 hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu, anasema kwamba Bunge la Katiba halitofanya haki eti, CCM Zanzibar na *CUF* wapo kwenye Serikali ya pamoja kwa hiyo Wabunge wa *CUF* watakaotoka Zanzibar na kwa sababu wanashirikiana na CCM na wengine walioko huko, hilo Bunge la Katiba halitokuwa la haki. Hii ni dharau ya mwisho kabisa, kwamba sisi hatuna mawazo, mawazo yetu ni finyu na wao wachache 48 ndiyo wenye mawazo halali ya kuwalilisha Watanzania, kasema nani maneno haya? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwamba sisi walliotuchagua kwa kura katika Jimbo la Wawi, hawana mawazo, wale wenye mawazo mazuri ni wao, kauli yao hii hapa imetoka ndani ya *speech* ya jana amechangia katika Muswada huu. Nasema hizi dharau zingine msizipeleke, mnayo ajenda ya siri

dhidi ya Watanzania na dhidi ya nchi yetu na ndiyo maana mnaleta maneno ya kibaguzi ndani ya Bunge hili na maneno ya kichochezi ambayo hayawezu kusaidia Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sisi katika Chama cha *CUF*, Naibu Katibu Mkuu wetu Ndugu Mtatiro alifanya maandamano kupeleka rasimu ya Katiba katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tukidai mabadiliko ya Katiba, ni sisi tuliofanya hili, mbona wao hawakufanya? Hatukuwaona wakifanya hilo, tumeandamana kwa hili kwa kudai Katiba, leo Rais ambaye ana mamlaka kabisa kwa mujibu wa Katiba yetu, angesema anaunda Tume bila ya kuja Bungeni na Tume ikasimama na ikafanya kazi bila ya kutushauri. Lakini amefanya busara, ametuletea Muswada tuujadili na tuupitishe hapa, watu wanakataa wanasema kuna udikteta, udikteta gani zaidi ya madaraka aliyonayo akayakasimu mwenyewe, akayaleta kwenye Bunge. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri na mimi uliniingiza katika Kamati ya Katiba na Sheria kusaidia pamoja na wenzangu hawakufurahia, haya makabrasha niliyonayo ni maoni ya wadau mbalimbali, Majaji waliostaafu, watalaan mbalimbali, taasisi mbalimbali, tumekaa kwenye Kamati kulipitia moja baada ya moja. Mimi nilishakaa katika Bunge hili toka mwaka 1977 sijapata kuona Muswada wa Sheria umekuja Bungeni umewashirikisha watu kama huu, sijaona hata siku moja, hata siku moja sijapata kuona! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunataka nini? Eti leo tukatembee nchi nzima kwa kupeleka tena Muswada huu, tunachotaka kupeleka kule ni fujo, sisi tunakataa, sisi tunakataa kupeleka fujo! Kama ni mawazo yametoka na yametoka kikamilifu, wakati tunaingia kwenye Kamati wenzetu walikuwa hawaii kwenye Kamati, nikakaa nao, nikawaambia kama tuna mawazo kwa nini tusije kwenye Kamati tukazungumza? Leteni mawazo yenu tuyachambue yenyе maana tutayakubali, ndiyo baadaye wakaanza kushiriki.

Mheshimiwa Spika, tumekaa kwenye Kamati wameleta mawazo yao, tumekaa tulilokubali tumelikubali. Ilifika mahali mpaka Mheshimiwa Tundu Lissu anamwambia Mheshimiwa Chenge sasa hivi ukikubali mawazo yangu nitakuwa na mashaka, mara ilifika mahali Mheshimiwa Chenge akaona hii *point* ya Lissu ni sahihi, sasa leo anasema tukaanze tena mchakato, mchakato gani wa kuanza? Tunachohitaji ni mchakato wa kupatikana kwa Katiba, huo ndiyo msingi wa hoja iliyopo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana ndugu zangu *The Nation has to remain as a Nation*, hatuwezi kuwa na Taifa lenye vipande vipande na mawazo potofu, tubaki na Taifa na Taifa litapatikana kama mchakato huu wa Katiba tutakwenda nao kwa salama na amani, kwa utulivu kwa kuaminiana na kwa busara na kuheshimiana, hiyo *process* ndiyo itatusaidia kupata Taifa lilitotimia na ndiyo lengo la Rais kwamba, sasa jamani baada ya miaka hamsini ya Uhuru wa Tanzania Bara, baada ya miaka 46 ya Mapinduzi, hebu tukae tujitazame upya chombo ambacho tunakitumia kuendesha nchi kiweje? Hayo ndiyo madhumuni makubwa. Sasa nafikiri busara ikitaka kutumika turudi tukae, tupitishe Muswada.

Mheshimiwa Spika, nawashauri Watanzania wenzangu, hebu tusishawishike na taasisi mbalimbali hadi tukavunja amani ya nchi. Kamati ya Katiba na Sheria mapendekezo yaliyofanywa na katika *page* zetu yako 34, tumepitia Kifungu kwa Kifungu na kama kuna wakati ambao hatukutoka katika Kamati mpaka tumemaliza ni wakati huu, ukiwaacha wachache ambao hawakuwa *serious* ndiyo hawakuwa *serious*, waliokuwa *serious* wamefanya kazi hii bila ya kuchoka na katika hali ngumu kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania wanaoamini kwamba kazi haikufanyika, wajue kwamba, kazi imefanyika tena kwa uadilifu mkubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, *Schedules of Amendment* mnazoziona ni matokeo ya mambo matatu, maoni ya wananchi, maoni ya taasisi na mchango wa Kamati. Ndiyo maana mnaona mabadiliko makubwa ya Muswada huu, tumepunguza hata madaraka ya Rais katika Muswada huu na amekubali. Kwa sababu kila *stage* ambayo tunataka kushauriana tulikuwa tunakwenda, kwa mfano, tumekubali kwamba baada ya Taarifa ile ya rasimu kumalizika ikiipelekwa kwa Rais vile vile

iwe *tabled* wananchi waipate tumekubaliana, sasa wanasesma ooh itachakachuliwa, itachakachuliwaje wakati tumekubaliana kwamba, itakuja huku ndani na wananchi wataipata?

Tumekubaliana vile vile ile rasimu ikishamalizika kuna *stage* tutakwenda tena kwenye mabaraza kwenda kuipelekewa wananchi waione. Hii ndiyo rasimu iliyo toka, kuna uwazi gani zaidi ya huo? Lakini bado tunawapotosha wananchi, tunafanya kama hakuna jambo lili ofanyika na hii nasema ni dhambi ambayo ni mbaya sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo moja alisema jana Mheshimiwa Lissu kwamba Zanzibar imepewa uhuru mkubwa sana, nasema amekula kiapo, katika Katiba hii kifungu cha 98 kinasema kabisa *two third* ya mambo yote yanayohusu Katiba yataamuliwa kwa *two third* ya Bara na *two third* ya Zanzibar, *two third* maana yake nini? Siyo namba ya watu, hata mkiwa watu milioni kumi inayotakiwa ni *two third*, hata Wazanzibar wakiwa kumi inayotakiwa ni *two third* ya watu kumi, kasomeni *mathematic* vizuri, kwa hiyo *number it doesn't mean anything there*, ni *two third*. Kama hata Wazanzibar wakiwa kumi, hata Watanzania Bara wakiwa kumi ni *two third* yao. Kwa hiyo, kupiga kelele juu ya namba ni kwamba, tunataka uwakilishi wa mawazo yapatikane lakini *the final day*, mnapopiga mnatumia *two third*, sasa mnataka haki gani zaidi ya hiyo?

Mheshimiwa Spika, hiyo *two third* ameitaja mwenyewe ni *thirty percent* ya watu wote ndiyo *two third* ya Zanzibar, sasa *thirty percent* ni ndogo sana, lakini ha-propose yeye asilimia nyingine iwe ngapi, anaishia tu kulaumu iliyopo lakini hasemi anayo itaka hasa anataka iwe ni ngapi, aseme basi kwamba hatuwataki ninyi Wazanzibari tuwfute kabisa msiwepo na hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo wewe umekula kiapo itakuwepo tena? *What are you talking about?* Hebu tuwe *serious* katika suala zima la nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo kubwa tunalolifanya, tunahitaji kuwaelekeza Watanzania vizuri. *Role yetu kubwa kama Viongozi ni kuwaelekeza Watanzania kuonesha leadership* kwamba we need a country itakayobaki na amani, utulivu na umoja na haki za raia zilindwe, thus is what we want, kwamba rasilimali za nchi hii ziwafaidie Watanzania wenyewe ndiyo kitu kikubwa tunachokihitaji hapa. Kwa hiyo, jambo la kwanza ningeomba sana kwamba, kazi iliyofanywa kwenye Muswada huu, mabadiliko yallyofanywa ni makubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumzia kwenye vifungu viwili tu, cha kwanza ni suala la haki ya kupiga kura kwa kila raia, tuhakikishe katika zoezi hili kila raia anapata haki yake ya kupiga kura. Kwa hiyo, Tume zetu za uchaguzi ziboreshe madaftari ya kupiga kura, tuhakikishe kwamba kila mtu anapata haki ya kupiga kura, huo ndio msingi wa kwanza kwa sababu msingi wa utawala ni uchaguzi, kuchagua na kuchaguliwa. Msingi mzuri wa kuweka Katiba hii ni kura. Zile *two third* za ndani ya Bunge lenyewe la Katiba lakini hata ile kura ya maoni inahitaji watu wapige kura. Kwa hiyo, naomba kabisa Tume mbili zote za Uchaguzi ziboreshe sheria zao, ziboreshe taratibu zao tuhakikishe tunapata haki na kila mwenye haki ya kupiga kura anapiga kura. Hilo lilikuwa la kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pili upo wasiwasi kwamba Je, Muswada huu ukishindikana itakuwaje? Labda wengine hatuelewi ile process. Katika Bunge lile la Katiba ambalo tumelipa madaraka makubwa, mwanzo tulifirkiria hata Kanuni, lakini tukasema hapana Kanuni watatunga wenyewe za kuendesha shughuli za Bunge ili kupunguza madaraka ya Rais. Hadidu za rejea tunesema Kifungu cha tisa (9) na kumi na sita (16) ndiyo hadidu rejea kwa hiyo Rais hana tena mamlaka ya kutunga hadidu rejea, tunataka tufanye nini zaidi ya hapo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sasa kwa watu wanaoteuliwa katika Tume hizi, wawe watu wenyewe uwezo, wenyewe taaluma, wenyewe uadilifu na uaminifu mkubwa sana. Pia hapa kulikuwa na mashaka kuhusu Wanasheria kwamba, Wanasheria Wakuu hawa wamekuwa na madaraka ya kuingizwa pale, naona hoja moja ya msingi ni kwamba, bado umempunguzia tena Rais madaraka, ungemwachia yeye peke yake akatumia tu ushauri wa kawaida tusingembana Mwanasheria Mkuu kwa nini na wewe ulishiriki katika hili ambalo wewe ni mtaalam, lakini unapomshirkisha atakwambia Rais huyu mtu unayetaka kumchagua katika Tume hii maana yake umempa madaraka kisheria. Sasa, ile ya kwanza, ni ile ya kawaida hii sasa umempa madaraka kisheria, kwamba huyu mtu unayetaka kumchagua katika Tume mbona sifa zake zina kasoro

moja, mbili, tatu, nne, tano? Anapata ushauri wa kisheria mbali na ule wa kawaida wa Rais kwa mujibu wa Katiba anashauriana na Mwanasheria Mkuu. Kwa maudhui ya Muswada huu yeye ana madaraka au amepewa *power* ya kumshauri Rais, kwamba Rais hana njia ya kumkwepa, ni lazima achukue ushauri wake, ndiyo maana tukaweka kwamba Wanasheria hawa wawili wamsaidie Rais katika kupata watu ambao ni watalaam, ni waadilifu na wana uwezo wa kufanya kazi katika Tume hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu walikuwa wanashauri kwamba, Tume hii iingie wanasiasa, mbona *forum* yetu wanasiasa ipo tu? *Forum* ya wanasiasa ipo katika Bunge lenyewe, huku kazi yao kubwa ni kukusanya maoni ya watu, hutakiwi upeleke la kwako kule na wewe unazo *forum* zako za kutoa mawazo, katoe mawazo katika *forum* ambazo zinahusika. Tuwaachie watalaam watukusanyie maoni, wayalete maoni hayo na yatakuwa wazi, yataonekana hakuna kitakachofichwa hata kimoja. Ndivyo tulivyorekebisha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sana wanaosoma hii sheria tusome pamoja na haya mabadiliko ambayo yameletwa na Serikali baada ya Kamati kufanya kazi yake. Tukifanya hivyo tutawafanya haki Watanzania, tutapata sheria iliyo nzuri na itafanya kazi vizuri. Kitu kikubwa hapa ni kujenga uaminifu na tupendane, Taifa hili litakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Anayefuata ni Mheshimiwa Ismail Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa pia ajiandae.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia nami napenda kuungana na Wabunge wenzangu kuunga mkono hoja hii. Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Sheria na Katiba pamoja na Kamati inayohusika na masuala haya kwa kutuletea Muswada mzuri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali kuleta Muswada huu, ningependa kuwatahadharisha Watanzania wenzangu, hawa ambao wanaonekana hawakubaliani na Muswada huu au Katiba mpya, wanatafuta mwanya wa kuleta vurugu katika nchi yetu, basi. Hawana nia nyngine yoyote ambayo inaweza kutusaidia sisi Watanzania tukaendelea kuishi kwa amani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Rais alichaguliwa kwa kura nyngi na Watanzania, kwa hiyo, ni dhahiri kabisa Watanzania wana imani naye ndiyo maana walimchagua. Tarehe 31 Disemba, 2010, kwa ridhaa yake mwenyewe kama Rais akatangaza kwamba anapenda aone Katiba mpya katika Uongozi wake kabla ya kumaliza, sisi Watanzania tunataka bahati gani zaidi ya hiyo? Tumekuwa tukidai Katiba, sasa Rais ameamua tutengeneze Katiba na sasa hivi tumeletewa Muswada.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha kuna watu wanataka hata kutunyang'anya mamlaka tuliyopewa katika Bunge letu hili. Kwa mfano, kuna taasisi moja inaitwa Jukwaa la Katiba, katika gazeti la Ijumaa tarehe 4 Novemba, wametoa ukurasa mambo mengi ambayo ukiyasoma mengine yanatia kichefu chefu licha ya kukera. Nitasona kidogo tu, Jukwaa la Katiba Tanzania linapenda kuwasilisha maoni na mapendekezo ya wananchi, hivi aliyechaguliwa na wananchi hapa ni nani, ni sisi Wabunge au wao? Ni dhahiri kabisa kwamba wana nia ya kutaka kutupokonya mamlaka ambayo sisi tumepewa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunapojadili Muswada huu tunakuwa *guided* na Katiba hii siyo vinginevyo, huwezi ukajadili Muswada huu nje ya Katiba hii, kwa hiyo, nashangaa watu wanapotaka kuhoji mamlaka ya Rais, hawana nia nyngine zaidi ya kutaka kumdhaliishwa tu, tusikubali hata kidogo Rais wetu ambaye ndiyo kioo cha Taifa letu kudhalilishwa na wahuni hawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge ondoa hayo maneno ya watu wahuni.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, naomba kuondoa. Unajua wakati mwingine unapokerwa unapata jazba, kwa hiyo, unatumia maneno ambayo siyo mazuri naomba radhi.

SPIKA: Tuendelee.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Spika, uhuru wa wananchi au mamlaka yao yanarudi wakati wa kutunga Katiba hii. Kwa hiyo, baada ya Muswada huu kupitishwa wananchi wana nafasi mbili kubwa za kufanya wanachotaka wao, sasa hofu na wasiwasi huu unatoka wapi? Kwanza, watatoa maoni yao kwenye Tume na pili watapata nafasi ya kupiga kura. Sasa huu wasiwasi na hofu ya kusema kwamba Muswada huu ni wa dola unatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye Muswada wenyewe ibara ya 24, kwa kuwa litaundwa Bunge la Katiba au Bunge Maalum, nashauri Serikali iangalie tena kifungu hiki na iwaacie Bunge hilo ambalo litakuwa juu ya Bunge hili, juu ya kifungu hicho hasa kifungu namba 24 na kifungu kidogo namba 23. Vile vile napendekeza kwa kuwa *Attorney General* wa Tanzania Bara na *Attorney General* wa Zanzibar wao *automatically* ndio washauri wakuu wa Serikali zote hizi mbili hakuna haja ya kuwaingiza kwenye hili tundu, huo ni ushauri wangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wenzangu wengi wameshachangia yale ambayo nataka kuyachangia, lakini moja kubwa ambalo nimekerwa sana na wenzetu hawa wa CHADEMA, Mheshimiwa Tundu Lissu katika taarifa yake inalenga kuvunja Muungano tu hakuna kitu chochote alicholenga humu, jambo ambalo ni hatari katika Taifa letu hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna kitu cha kujivunia, katika Afrika hii hakuna nchi zilizoungana zaidi ya Tanzania, ni sisi peke yetu. Sasa tunu hii ni lazima tuitetee na kuilinda kwa nguvu zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, natoka Jimbo la Tabora Mjini, pale Tabora Mjini kuna redio moja maarufu sana inaitwa *Voice of Tabora FM*, wakati Muswada huu ulipokuwa unajadiliwa, wananchi walipata nafasi katika kipindi maarufu cha Meza Huru kujadili zaidi ya masaa mawili kila siku. Sasa hawa watu wanasema wananchi hawajadili, wanataka wajadili namna gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naungana nao katika suala hili na kuunga mkono Muswada huu ambao umeletwa mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaendelea niseme hili ambalo linanishangaza katika vyombo vy a habari, upotoshwaji ambao unaendelea katika nchi yetu na upotoshwaji huu unafanya na watu waliosoma, wanaojua wanachokifanya ambao hawatutakii mema, Watanzania wanaotaka kuvuruga amani ya nchi yetu, wanaoichonganisha Serikali na wananchi wake na wanaoongea bila hofu bila kumwogopa Mungu, wanamatukana Bunge lako Tukufu, wanamatukana Rais, wanawatukana Mawaziri. Hata watoto wadogo wakitaka kutukanana wanajificha ndio wanatukanana, lakini ya kutukanana hadharani inanitia hofu kabisa. Naijuliza hawa watu wana nani nyuma yao, nani anayewapa kiburi cha kufanya yote haya? Bunge lilidhihirishiwa jana kwamba walio nyuma ya hawa watu wenyewe viburi wapo na wanachotaka wanakijua wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nchi zingine ukutukana hadharani uko kwenye *trouble*, wala hutoi mguu wako hapo ulipotukana. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba utakapomalizia utuambie ni kifungu gani cha Katiba kinachoruhusu mtu kutukana anavyotaka tena anawatukana viongozi uje utuambie Watanzania kwamba ni kifungu gani kinaruhusu mtu kutukana anavyotukana kwenye vyombo vy a habari. Namsihi sana aje aliseme hilo. Nashangazwa sana na upotoshwaji unoendelea maana sheria iko wazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitasoma na nitaomba kunukuu maana haya yaliyofanywa na wasomi wazuri, tena wanasema mchana kweupe tena bila woga. Wanasema kwamba wataandamana na hakuna mtu yeyote atakayewafanya jambo lolote, hiyo ni dharau kubwa sana kwa Serikali yetu ambayo ina Rais wake ambaye alichaguliwa na wananchi na akaweka Mawaziri na Wabunge tupo kwa ajili ya kutunga sheria na kusimamia. Kwa hiyo, nashangaa kwamba mtu anasema kwamba watafanya wanavyotaka na hakuna mtu yeyote mwenye mamlaka ya kuwazuia. Ni dharau kubwa sana kwa Serikali yetu na hata kwa Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inawezekana wananchi hawana Muswada na inawezekana walionyayo hawataki kuitumia inavyotakiwa. Naomba kunukuu Muswada unasemaje. Muswada huu unasema ni Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuunda Tume ya mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba na kuainisha na kuchambua maoni ya wananchi kuainisha masharti kuhusu Mabaraza ya kuhalalisha masharti yaliyomo kwenye rasimu ya Katiba na mambo mengine yanayoendelea. Lakini taarifa iliyoko kwa wananchi inasema kwamba Bunge hili Tukufu linajadili Katiba. Tena wanaosema hivyo ni wasomi wazuri, wanasema tunajadili Katiba, sisi hatujadili Katiba. Wananchi mtuelewe kwamba sisi hatujadili Katiba leo. Katiba watujadili wao wenywewe, Tume itakuja kwao vijiji huko waliko wala hawatakiwi kwenda mijini, Tume itawafuata waliko na watatoa maoni yao.

Wasipotoshwe na wasikubali, wajadili kwa mantiki ya amani ya Tanzania siyo jazba ambayo naiona inaendelea. Jazba haisaidii, jazba inasaidia nini? Jazba wanaongea nayo watu waliovuta bangi na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa umma wa Watanzania unavyopotoshwa sielewi maana yake. Lakini nimeelewa jana kwamba, kuna jambo ambalo linaendelea ambalo tunatakiwa sisi kama Wabunge pia masikio yetu yawe wazi kufuatilia kwa nini wenzetu wengine wana mawazo tofauti maana wengine walisema wakipata utawala ndani ya siku 100 watatayarisha Katiba na itakuwa tayari. Sasa Muswada wa Katiba umeletwa wanaukimbia, hiyo Katiba waliyokuwa wanataka kuileta ni ya aina gani watuambie? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kifungu cha (9) katika Muswada huu na ningependa kusoma madhumuni kabla sjafika huko, ambayo ni kuweka utaratibu wa kuunda Tume ya kukusanya maoni na nimeshalisema hili. Lakini pia kuweka masharti kuhusu hadidu za rejea za Tume. Nataka wananchi waelewe kwa sababu inawezekana kuna watu ambao hawajapata huu Muswada. Kuna mengi sana ambayo yameelezwa na Muswada huu. Lakini nataka maeneo yale ambayo yanawahuhsu wananchi, kwamba kuweka utaratibu ambao utaruhusu wananchi kushiriki kwa mapana, wala siyo kwa siku mbili wala siyo kwa siku moja, wananchi mtapata muda mrefu sana wa kujadili Katiba ya nchi yenu mnataka iweje.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 4(h) kimesema kwamba, kuweka utaratibu kuhusu namna ambavyo Tume itakusanya maoni kutoka kwa Taasisi za Umma na Binafsi, Vyama vyta Hiari na Mashirika ya Kidini, lakini Kamati imeongeza wakulima na wafanyabiashara. Hata hivyo, naona wafugaji wamesahaulika katika eneo hili. Naomba wafugaji pia wakumbukwe katika kujadili Muswada huu utakapowafikia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba tena katika aya ya 10 lakini kabla sjafika kwenye aya ya 10, uundaji wa tume, wamesema kwamba Rais ndio atakayefanya kazi hiyo ya kuunda Tume na kuwachagua wale ambao ataona wanafaa. Lakini Muswada unasema watakao teuliwa kwenye Tume Rais atajali sana mambo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na wala hatakaa peke yake. Lakini pia madaraka ya Rais yanamruhusu kwamba muundo wa Tume uweje na sisi tumezungumzia muundo wa Tume. Lakini Tume pia itakuwa na watu wenye taaluma tofauti. Sioni sababu ya sisi kuwa na wasiwasi kuhusu Tume ambayo itaundwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, naomba pia katika kuunda Tume hiyo azingatie jinsia. Kuna haja sana ya kuzingatia jinsia. Tume imewekewa maadili, naomba niwaambie kwamba, Tume itakayoundwa na Rais imewekewa masharti kwamba, atakayekwenda kinyume na maadili hayo kuna adhabu ambazo zimeainishwa kwa wajumbe wa Tume. Lakini kuna jambo ambalo nimeliona katika ukurasa wa 38 kifungu cha 16(9) ambacho kinasema kwamba watakaopiga kura ni Watanzania

pekee. Wasiwasi wangu ni huu kwamba Watanzania hatuna vitambulisho vya uraia. Utamjuaje kwamba huyu ni Mtanzania na huyu siyo Mtanzania? Sheria iainishe kwamba watawatambuaje walio Watanzania na wasio Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nikienda katika kifungu cha 20(e), Rais atawateua wajumbe 16 na wajumbe hawa wametajwa; asasi zisizokuwa za Kiserikali, Asasi za Kidini, Vyama vya Siasa na kadhalika. Nataka kujua katika asasi zisizokuwa za Kiserikali, ni wajumbe wangapi watakaoteuliwa, Asasi za Kidini wajumbe wangapi, Vyama vya Siasa wajumbe wangapi, je, Rais wa Zanzibar atashirikishwa katika kuwateua wajumbe hao na katika makundi sehemu ya (v) anasema makundi yenye mahitaji maalum katika jamii, makundi hayo hayakutajwa na Sheria. Ningependa kujua makundi hayo ni makundi gani kwa sababu kuna makundi mengi katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimesoma katika Muswada huu nimeona kwamba, Mwenyekiti na Makamu wake au Spika na Naibu Spika watatakiwa kuapa, lakini Bunge la Katiba au Bunge Maalum kwa ajili ya uundaji wa Katiba sikuona ni wapi Wabunge hao wakapoapa, hakuna sehemu iliyoainishwa kwamba Wabunge hao wataapa, Wabunge ambao watakuwa katika Bunge la Katiba au Bunge Maalum kama marekebisho yalivyoletwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha 32(3) kuna jambo hapa ambalo nimeliona kwamba, Tume ya Uchaguzi itateua siku nyingine ya kurudiwa kwa upigaji kura ya maoni na utaratibu wa kura ya maoni utaanza upya. Lakini ni baada ya muda gani, hakuna muda uliotolewa ambao kama kura za hapana zitakuwa nyingi Tume itaitisha tena uchaguzi mwingine.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Watanzania baada ya mjadala huu kumalizika watajua Wabunge tunafanya nini katika kipindi hiki, hatujadili Katiba tunachojadili ni namna ya kuunda Tume. Mnaopotosha acheni upotoshaji huo. Ninjy mliaoamua kuwapotosha Watanzania, damu ya Watanzania ambayo inaelekea kumwagika kwa ajili ya vurugu ambazo zimepangwa na ambazo wanazisema wazi bila kificho zitakuwa juu yenu. Naanza kuwalaani leo hata kabla hamjaandamana. Nalaani mipango yenu hiyo kwamba Mungu aikemee na mkashindwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja hii kwamba Muswada huu ni mzuri na Watanzania wasiwe na wasiwas, Tume itakuja kwao kwa ajili ya kutoa maoni kwa kuzingatia amani tuliyonayo Watanzania na Watanzania tuonekane ni mfano kwa nchi zinazotuzunguka na kwa dunia nzima kwamba kila tunachoamua na kila tunachotaka kufanya kwa mustakabali wa nchi yetu, tunafanya kwa amani, tunafanya bila vurugu, tunalfanya bila kushinikizwa. Wanaoshinikizwa wakatafute nchi yao. Nchi yetu ni ya amani na kila kitu tunafanya kwa utaratibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

MHE. MOHAMED JUMA HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na nitachangia katika hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda uniruhusu kama utangulizi kueleza hii hali ya upotoshaji wa mambo Tanzania. Mtaniwia radhi lazima niseme kwa ujumla wote kwanza na kosa liko wapi na nini matokeo ambayo leo ndio tunayaona. Hali ya upotoshaji Tanzania ambayo inafanya kwa bahati mbaya wakati mwingine nasikitika na wanaharakati, vyombo vya habari na wanataaluma ambayo hali hii Serikali iliyopo madarakani imenyamaza kimya. Ndio maana leo inafika *stage* baadhi ya vyama vinazidi kupotosha hapa Bungeni kwa kusema maneno kama yaliyosemwa jana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tutasherehekea Uhuru wa Tanganyika, vyombo vyote vya habari havisemi hivyo vinasema uhuru wa Tanzania Bara, wakati wanajua hakuna uhuru wa Tanzania Bara. Wasomi jana wakati Lema anatoka Gerezani au Mahabusu anasema karibu tunasherehekea miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania CHADEMA na wengine wengi wakati wanajua hakuna Uhuru wa Tanzania Bara, hakuna Uhuru wa Tanzania ni uhuru wa Tanganyika wa mwaka 1961. Miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika, kwa nini Waziri wa Habari yupo asiliweke wazi? Upotoshaji

huo huo umefanya na vyombo vya habari *ITV* hivi juzi katika mdahalo uliofanyika wamethubutu kusema kwamba Wabunge wanapata milioni saba na wanapewa fedha za dereva 500,000, lakini wanadhlumu madereva wanawapatia 100,000. Wamefika kusema pamoja na marupurupu yote Mbunge anapata milioni 12,500,000/=, ni aina ya upotoshaji unaofanywa na vyombo vya habari, Serikali imenyamaza kimya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, upotoshaji unaoeendelea na Serikali imekaa kimya, utatufikisha pabaya. CHADEMA hapa hapa Bungeni tumepata jibu waliandika barua kumtaka Waziri Mkuu awakutanishe CHADEMA na CCM kuhusu Mgogoro wa Arusha lakini watu hao hao CHADEMA wanakilaumu Chama cha *CUF* ambayo ni maamuzi ya wananchi wa Zanzibar kwamba kuunda Serikali ya Pamoja. Aina ya upotoshaji inaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ambaeo unaleta mbinu za kufikia Katiba leo, watu wanaupotosha kuwa ndio mambo ya Katiba, maoni yanayotakiwa ndio yameanza hapa. Kwa hiyo, jambo langu la kwanza kama utangulizi Serikali iliyoko madarakani isiachie upotoshaji ukafika kiwango hiki, utatuharibia maisha yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika mada, hoja ya Katiba mpya amezungumza Mheshimiwa Hamad hapa tulianza muda mwangi, hoja ya Serikali tatu, *CUF* tulianza toka 1992, kama CHADEMA na wao wanataka Serikali tatu, wao ndiyo wakubali huu mchakato uliopo ili tufikie kwa hatua hiyo, wawashawishi wananchi wao kuomba Serikali tatu sio kuilaumu Zanzibar na kuidharau Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja hii ambayo imetokana na kasoro tunazoziona sisi zipo mpaka katika chaguzi zenu ndiyo maana tukaomba hoja ya kuwa na Katiba mpya na zero draft tukaipeleka kama alivyosema Mheshimiwa Hamad kwa maandamano, ni Chama cha Wananchi *CUF*, leo tumepata fursa hii na nimshukukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano kuleta fursa hii, halafu eti leo mimi mwanachama wa *CUF* niizembee, niikejeli, nitoke nje nisijadili, niisusie nina maana gani? Nilikuwa na maana gani hapo kutaka Katiba mpya, halafu leo nafasi adhimu, *golden chance* hii imeshafika, tukaifanyia dharau, itakuwa hatuwatendei haki wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi wanahitaji Katiba mpya. Baada ya miaka mingi ya Katiba iliyopo ambayo sisi kwa upande mwagine, mara zote hapa Bungeni kila Mbunge wa Zanzibar akisimama Muungano, Muungano, Muungano, Muungano, hakuna hoja nydingine nzito kila siku Muungano kwa sababu mfumo wa Muungano uliopo ndiyo unaotuleeta matatizo, matatizo yenyeewe hayatutuki isipokuwa kwa njia ya amani, ya usalama na utulivu ya kubadilisha Katiba kwa njia ya demokrasia. Nini tunataka zaidi ya hali kama hiyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Muswada wa mwanzo uliowasilishwa Bungeni tarehe 5 Aprili, 2011 ambayo nakala yake ninayo hii hapa, ulikuwa na Ibara 31 na huu wa pili una Ibara 34 na mambo yaliyokuwemo humu, ndiyo yale yale yaliyomo katika huu Muswada mwagine. Unaposema huu ni mpya, usijadiliwe, usomwe kwa mara ya kwanza una maana gani? Huu wa mwanzo, vipengele viliviyokuwemo kwa upande wetu sisi ukawa unataja *Attorney General* wa Jamhuri ya Muungano peke yake, unamtaja Waziri wa Sheria na Katiba wa Jamhuri ya Muungano peke yake, unamtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano peke yake, kitendo tunachotaka kukibadilisha kinachofanywa ni cha mchakato wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Mbia mwagine wa Jamhuri ya Muungano ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sisi upande wa Zanzibar tukasema hapana, Muswada huu umerekebishwa.

Mheshimiwa Spika, leo kila anapotajwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano na Waziri wa Zanzibar yumo, kila anapotajwa Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar yumo, anapotajwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar yumo. Pana jipya gani hapa, zaidi ya kurekebishwa na ikawekwa katika *definition* ikaelezwa, kama Wazanzibari tunataka nini zaidi ya yale tuliyoyataka ambayo yameingizwa humu katika hii. Hatuwezi kusema hii ni mpya kabisa, hapana na kwamba isomwe mara ya kwanza ni ile ile na imefanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nina rasimu ya marekebisho ambayo Chama changu cha *CUF* kuitia Naibu Katibu Mkuu wetu Mheshimiwa Mtatiro alinipatia, wamekaa kitako, wameuangalia

Muswada huu, wameangalia wapi pana mapungufu, leo nina furaha kusema kwamba, marekebisho haya ya Serikali ambayo wameleta, *schedule of amendments*, yamechukua asilimia kubwa ya haya ambayo chama changu walitaka yawemo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yale matatu au manne yaliyobakia nitayazungumza hapa ili nayo yaingizwe. Lakini chama changu cha *CUF* haiwezekani kwamba haya marekebisho waliyoyataka ni peke yao, utakuta ndiyo maoni ya Vyama vingine vyta Siasa, ndiyo maoni ya wanaharakati, ndiyo maoni ya wanataluma mbalimbali, leo ikiwa yameshaingizwa kwa hii hapa ambayo mabadiliko haya yaliyoletwa na Serikali tena nataka zaidi ya kukaa hapa, tukamaliza mjadala huu na hiyo Tume inayohitajika ikaundwa, tukaanza mchakato kamili. Siwezi kufanya kosa nikawasaliti wananchi wangu wa Jimbo la Mkanyageni na Wazanzibari wote, leo mie nitoke nje niseme Muswada huu ni mpya, hapana. Huu ni aina ya upotoshaji ambapo Bunge lako na Serikali iliyoko madarakani haifai kuvinyamazia kimya vitendo kama hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tutakapoendelea kunyaamazia vitendo hivi, matokeo yake yatakuwa mabaya, ni lazima *ku-act* kwa wakati kila jambo linapotokea. Wananchi huko mitaani wanaviamini vyombo vyta habari sana, leo vyombo vyta habari vinapofika vikazungumza kitu kinyumenyume, ni hatari na Serikali ikanyaamaza kimya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu kuna vipengele ambavyo ningependa pia viiingizwe kabla sijatoa mfano, naangalia *schedule of amendment* haraka, vingine sijaviona, kama vimo ndivyo ninavyopenda. Lakini huu Muswada haujaweka juu ya mambo yanayoweza kusababisha Mjumbe wa Bunge la Katiba kupoteza sifa. Kwa hiyo, tunataka zile sifa pamoja na kwamba yameshatajwa *kima-group* nani na nani au *group* gani anatakiwa awemo humo, lakini pia ni vizuri kuwekwa zile sifa na anapopoteza sifa, *replacement* itakuwa vipi? Ni vyema haja hiyo nayo iwepo.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna kura ya maoni, sasa Muswada huu ni vizuri pia uweke kipengele kitakachoweka wazi, je, leo kura ya maoni upande wa Tanzania Bara wakikataa, wakipata hapana au upande wa Zanzibar wakasema hapana au wote wawili wakasema hapana, nini cha kufanya? Ndiyo maana tena basi mchakato? Haiwezekani. Tunahitaji Katiba mpya. Kwa hiyo, Muswada ueleze inapotokea Tanzania Bara katika kura ya maoni wamekataa au upande wa Zanzibar wamekataa au wote wamekataa, nini cha kufanya. Hayo ndiyo mambo ya kuyajadili na tukyawewka, tukayaingiza katika Muswada huu. Halafu vile vile ni vizuri kuweka wazi muda wa kila kitu, pawe na ratiba maalum mpaka kufika inatamkwa tarehe fulani tumemaliza mchakato wa Katiba mpya na kutangaza na ili tujue hasa kwamba tunataka uchaguzi wa 2015 utumie Katiba mpya. Hayo ndiyo mambo ambayo ningependa yawemo katika mchakato wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ya msingi kwanza ni hayo ambayo nimeyaona, narudia kwa kusema upotoshaji unaoendeshwa na sehemu tofauti kama ni Chama cha Siasa, kama ni chombo cha habari, kama ni Wataalam, kama ni nani kuna baadhi ya mambo yanaweza yakadharauliwa lakini kuna baadhi ya mambo yanavuka viwango yasiachwe, tutakuja kujilaumu wenywewe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu. (*Makof*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili kusudi niweze kuchangia yale ambayo naona kimsingi yanaweza yakatusaidia kama Watanzania. Maoni haya, nayatoa kwa niaba ya Watanzania wote kuititia Chama changu cha *NCCR-MAGEUZI* juu ya yale ambayo tunayaamini yanaweza yakatusaidia na pengine kuweza kupata Sheria ambayo itawenza kuongoza mchakato mzima wa kuja kupata Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba ninukuu Katiba, Ibara ya 18 fasili ya (a) ambayo inatuambia kwamba kila mtu anao uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake. Nimejaribu kufuatilia mjadala ambao unaendelea hapa tangu jana na hadi hivi sasa ambapo tunazungumza. Waheshimiwa Wabunge wengi inaonekana hatujikiti kwenye hoja, tunajikita kwenye malumbano, tunazidi kujenga chuki, hatujengi. Hebu tuangalie kwamba, kwa nini kuna matatizo, kwa nini ndugu zangu wa CHADEMA wanapinga utaratibu huu, kwa nini CCM

wanapingana na CHADEMA na kwa nini huko mtaani pia kuna *pressure* kubwa. Ni lazima tuijilize maswali haya, ndiyo tunaweza kupata suluhisho la kudumu, badala ya kupata badiliko la muda Waingereza huita *cosmetic change*.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimnukuu Mheshimiwa Angellah Kairuki wakati anachangia katika hoja iliyopo mbele yetu, amemnukuu Baba wa Taifa kwamba 1962, kuhusiana na masuala ya Katiba, akasema Katiba ni ile inayoishi na ile iliyomo moyoni mwa watu na Mheshimiwa Ole-Sendeka nae akajaribu kutoa *experience* ya kule Kenya, akasema kwamba wananchi ndiyo walio juu ya Katiba. Nimeanza kwanza na uhuru wa watu kuweza kutoa fikra zao na kule Kenya tumeona, Mahakama iliamua na kusema kwamba, wananchi ndiyo walio juu ya Katiba na Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 8, naomba ninukuu kwa ridhaa yako, Ibara 8(1)(a) inatuambia kwamba: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo, wananchi ndiyo msingi wa Mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na Mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye hoja moja kwa moja, tatizo ambalo linapigwa kelele na Watanzania wengi huko nje, ni utaratibu au mchakato mzima wa namna gani huu Muswada umeweza kuletwa ndani ya Bunge letu, itakumbukwa wakati wa Bunge la mwezi Aprili, wananchi wengi wali-complain juu ya suala la *public hearing*, suala la kukusanya maoni kutoka kwa wananchi, walisema kwamba maoni kukusanya Dar es Salaam peke yake, Dodoma na vilevile Zanzibar iliyokuwa haikuwekwa, lakini baada ya kupiga kelele Wazanzibari, Zanzibar ikawa imeingizwa, wakasema ni vizuri tupanue kuwe na wigo mpana ili kusudi na maeneo mengine wananchi waweze kufikiwa na waweze kutoa maoni yao. Hivyo, nikiwemo nilitegemea kabla ya Muswada huu kuletwa ndani ya Bunge letu, tungepita huko kwa Watanzania wengine kwenda kukusanya maoni na hivyo huu Muswada ungesomwa kwa mara wa kwanza ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, sioni tatizo la kuahirisha mjadala huu, tukaenda kukusanya maoni kwa wananchi kwa sababu tatizo liko hapo sio jambo lingine. Sioni kwamba inatu-cost nini na sioni kwamba tuna haraka ya nini kwa sababu huko mtaani wanapiga kelele Watanzania wakiwemo, wananchi wa Jimbo la Kasulu Mjini ninakotoka wangependa nao maoni yao na ushauri wao uingizwe katika Muswada huu ambaao umeletwa ndani ya Bunge, wanasema wamenyimwa haki hiyo. Ni maoni yangu haya kutoka kwa wananchi, naomba nisikilizwe, wamezungumza wengine hatuwezi kufikiria wote sawasawa, lakini vile vile Malcolm X alituambia *you can not separate peace from freedom unless one has freedom*, naomba nipewe uhuru, nieleze kile ambacho ninachoklamini, hii ndiyo imani yangu, hivi vitu hatuhitaji kutumia nguvu, sijazoea kutumia nguvu, nalumbana kwa hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo kubwa ninaloliona wananchi hawakutaka Muswada huu usomwe kwa mara ya pili kwa sababu walilalamika huko nyuma, *public hearing* iwe expanded kwa maana kwamba, tuweze kufika katika maeneo mbalimbali na ukweli si busara kuona tunakusanya maoni Mkoani Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar peke yake, nchi hii ni kubwa sana na Serikali huwa inazungumza hapa kwamba, nchi hii ni kubwa sana, kwa hiyo, tutakwenda taratibu, sasa tunatambua ukubwa wa nchi, inapokuja kwamba tumebanwa labda bajeti yetu ina *deficit*, leo hatutaki kuheshimu uhuru wa watu ambaao wametutaka twende tukakusanye maoni yao ili tuweze kupata Sheria nzuri ambayo itatuongoza katika kushughulikia issue nzima ya Katiba mpya, tunawapuuza wananchi ndiyo maana kunatokea haya na wengine wanakosa uvumilivu ndiyo maana wametoka Bungeni. Ni uhuru wa watu wala tusiwalamu, mimi binafsi siwalaamu CHADEMA. Shida kubwa ninayoiyona ni hiyo, sasa labda pengine tuiangalie.

Mheshimiwa Spika, sasa nije moja kwa moja kwenye Muswada wetu, hilo moja kuendelea na mjadala huu na-declare interest kabisa huo Muswada haukupaswa kusomwa kwa mara ya pili, ilipaswa tungeusoma kwa mara ya kwanza na tungekwenda kukusanya maoni kwa wananchi, ingekuwa ni jambo la busara, haya yote yasingejitokeza wala *pressure* zilizoko mtaani zisingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mionganoni mwa watu ambaao tuliwasilisha hoja binafsi kwenye Bunge la Februari, 2011 la kutaka mabadiliko ya Katiba mpya, moja ya kitu kwa niaba ya Chama changu cha NCCR-MAGEUZI na wananchi wa Tanzania, nilishauri tunahitaji kufanya marekebisho

ya Ibara ya 98 ya Katiba yetu ya sasa, kifungu hicho ambacho kinaweza kikatoa mwelekeo juu ya namna gani tunavyotaka kufanya mabadiliko ya Katiba na hatimaye hata siku nyingine kama kuna shida hiyo, basi iweze kuwa rahisi badala ya kukalia mivutano na malumbano kama ambavyo yanatukumba hivi sasa. Kifungu kile ukikiangalia, hakiweki wazi, mchakato mzima, ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukafuata na taratibu gani za kufanya *constitutional amendments*, shida iko pale, lakini ukija kwenye Muswada wetu, huu Muswada una mapungufu kadhaa, kimsingi naungana na wale wote wanaosema kwamba Mheshimiwa Rais ana madaraka makubwa katika Muswada huu kama tutaupitisha, mimi siupitishi, siungi mkono kwa sababu una mapungufu yake na ndio maana sikutoka nje, nimetaka niwaeleze hapa hapa, tuelewane ni mapungufu gani ambayo ninayaona. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka Serikali msikie na ukweli watakaopitisha, kwa maoni yangu watakaopitisha Muswada huu ndani ya Bunge hili laana za Watanzania zitakuwa juu yenu, narudia tena laana za Watanzania zitakuwa juu yenu kwa sababu hawakutaka Muswada huu usomwe kwa mara ya pili, ulipashwa usomwe kwa mara ya kwanza. Mimi siendi na upepo, nawaambia kile ambacho nakiamini na nimefanya uchunguzi nimezungumza na watu, haya ni maoni ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa Tume, ninapajaribu kuangalia uhuru wa Tume katika Muswada huu, hii Tume itawajibika kwa Rais wetu pamoja na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar peke yao, tuna *experience* ya Tume nyingi ambazo zimeundwa hapa nchini, matokeo ya Tume hizi sijaona yakitekelezwa, baadhi ya Tume mengine hayakutekelezwa, kwa mfano, ile Tume ya kurekebisha maslahi ya wafanyakazi, nafikiri ilikuwa chini ya Ntukamazina kama sijasahau. Walipeleka taarifa kwa *President* wetu, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, upo uwezekano kuwa hii Tume itaweza kukusanya maoni na mwisho wa siku itakuja kupeleka, tumeambiwa kwamba kwa mujibu wa Muswada huu unavyopendekeza ipeleke taarifa kwa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar, halafu wao baadaye ndio wataona wafanye nini, ni wazi kabisa Tume hii haitakuwa huru.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kifanyike? Katika hili tulikuwa tumehitaji tuwe na Baraza la Kutunga Katiba, Baraza la Katiba Tanzania. Baraza la Katiba tungo-*specify* katika Muswada wetu, litakuwa na watu gani? Tungesema ngoja tuangalie katika Taasisi za Kidini, katika Vyama vya Kisiasa, kutoka Taasisi mbalimbali za Elimu ya Juu na kutoka kwa watu wengine itakuwa ni chombo ambacho ni *permanent*, chombo hiki kinaweza kikafanya nini? Hiki chombo kama tunataka sasa kukusanya maoni kutoka kwa watu baada ya Muswada kuwa umetengenezwa, wangkuwa na mamlaka ya kuweza kutuundia Tume na hapa kungekuwa na *checks and balances* kwa sababu kuna watu wengi ambaeo watakuwa wameshirikishwa katika mchakato mzima.

Mheshimiwa Spika, lakini huu utaratibu wa hizi Tume, kumekuwa na Tume nyingi ambazo zinaundwa ambazo matokeo yake hatuyaoni kwamba tumenufaika kwa kiasi gani. Kwa hiyo, ipo haja na kwa kweli niombe kwamba, hizi Tume naona kama vile zimenichosha, kwa hiyo naomba niishauri Serikali, huu Muswada tuuahirishe kuujadili kwa sababu Watanzania hawataki utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na hadidu za rejea kwamba, zitatolewa na Marais wetu wawili. Natambua kwamba ukuu wa Rais wa Serikali ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini hatuwezi tukakasimu, hatuwezi kuendelea kuacha wao ndio watutengenezee hadidu za rejea kwa sababu ya mamlaka walio nayo. Hata nao ni binadamu, wanaweza pia wakati mwингine wakatengeneza hadidu za rejea ambazo hazitaweza kutusaidia. Haya yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge tunakosea na sisi ni binadamu, kwa nini ye ye asikosee. Kwa nini ye ye wakati mwингine asiweze kututengenezea hadidu za rejea ambazo zinaweza zisitusaidie kupata mchakato wa Katiba mpya. Kwa hiyo, ndio maana tunasema tunahitaji kuwa na Baraza la Kutunga Katiba kwa maslahi ya Watanzania hasa tukirejea ile ibara ya (8) ambayo inasema kwamba Serikali itapata mamlaka na madaraka yake kutoka kwa wananchi. Kwa hiyo kutokuheshimu matakwa ya wananchi ni kukiuka Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, ibara ile ya 8(i)(a). Lakini pia mtachonga sana juu yangu, endeleeni, naendelea kula moto yaani kueleza ukweli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushiriki wa Wabunge na wanasiasa katika mchakato huu. Wanasiasa imeonekana kwamba wao wasishirikishwe na Wabunge wasishirikishwe, tena juzi asubuhi nilikuwa namsikia Mama yangu, Waziri wa Sheria na Katiba akieleza *TBC* kwamba Wabunge wako *busy*. Hata watumishi wengine ambao mnawaita wataalam nao wako *busy*. Humu ndani ya Bunge tuko wanataluma mbalimbali. Kwa hiyo, haimaanishi kwamba sisi Wabunge siyo watalalam, kwani mtaalam ni nani? Mtaalam ni mwanataluma. Kuna watu wana taaluma zao mbalimbali. Sasa tunapokuja katika *issue* ya kuona kwamba hawa ni wanasiasa, hawa hapa ni wataalam, humu ndani naamini kuna wataalam wa kila aina. (*Makofii*)

Kwa hiyo kwa msingi huo, suala la kutunyima fursa Waheshimiwa Wabunge, suala la kuwanyima viongozi wa Vyama vyta Siasa

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Ngoja amalizie kwanza dakika zimebakia chake.

MHE. MOSES J. MACHALI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Suala la kuwanyima Waheshimiwa Wabunge, suala la kuwanyima Viongozi wa Vyama vyta Siasa kwamba wasishiriki katika mchakato huu, siyo kweli kwamba watu hao wako *busy* na mchangano wao unaweza usiwe mzuri. Hofu ninayoionna kwa Serikali, kwanza, Raís ni Mwenyezekiti wa Chama cha Mapinduzi naye ni Mwanasiasa na amefanywa kuwa ndiye atakayekuja kutuundia Tume yetu, *how comes!* Leo uje utuambie viongozi wa Vyama vyta Siasa wasishirikishwe? Kuna nini hapo Serikali? Tutaomba mtueleze katika hili.

SPIKA: Haya ahsante, ahsante.

MHE. MOSES J. MACHALI: Nakushukuru Mheshimiwa Spika.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, taarifa ni kwa mujibu wa kifungu cha 68 na msemaji aliyejita ameendelea kusema kwamba na huu ndiyo tunasema upotoshaji kwa Watanzania kwa sababu hadidu za rejea zimetajwa sasa katika Muswada, kifungu cha (9) na (8) ndivyo vinavyotaja *terms of reference* kwa hiyo ni vizuri Watanzania waelewe kwamba hadidu za rejea zimetajwa sasa kwenye Sheria moja kwa moja na ndiyo hili moja ambalo liliombwa na Watanzania na sasa limekulbalika. Angesoma vizuri Muswada huu. (*Makofii*)

MHE. UMMY A. MWALIMU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia mjadala huu kuhusu Muswada wa mabadiliko ya Katiba yaani *The Constitutional Review Act 2011*.

Mheshimiwa Spika, mchangano wangu utajikita katika maeneo makuu matatu ambayo yamekuwa yakipigwa kelele na kwa bahati mbaya nasikitika kusema kwamba, yamekuwa yakifanyiwa upotoshwaji mkubwa sana na bahati mbaya upotoshwaji huu unafanywa na Wanasheria wenzangu ambao wamesoma Sheria na hao ambao wanajitisha ni wanaharakati na kinachosikitisha upotoshwaji huu unafanywa kwa maslahi ya nini au kwa faida ya nani? Ndiyo maana nikaomba kama Mbunge lakini pia kama Mwanasheria niweze kuchangia hoja hii ili Watanzania wawewe kuelewa ni kitu gani kinajadiliwa hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza ambalo limekuwa likipigwa kelele na kufanyiwa upotoshwaji mkubwa, ni suala la uanzishwaji wa Tume ya Kuratibu na kukusanya maoni chini ya sehemu ya tatu ya Muswada huu ambapo watu wanahoji madaraka ya Rais. Tatizo wenzetu wanaelewa kabisa madaraka ya Rais yako ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge na wanaharakati wote tuna wajibu wa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba Sura ya Pili, sehemu ya kwanza,

kifungu 33 kinasema kwamba: "Kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. Lakini pia najua kwamba kuna mihimili mitatu, kuna Bunge, Mahakama na Serikali. Lakini Katiba inasema, Rais atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu". Sasa unapohoji madaraka ya Rais kwa nini Rais anaunda Tume, mnataka Tume hii aiunde nani? (Makof)

Mheshimiwa Spika, tatizo letu hawa watu wana mtazama Rais kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wasome Katiba vizuri, ni Mkuu wa Nchi, siyo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi wala siyo mtu wa kawaida. Sasa kama wanataka kuondoa haya madaraka ya Rais wanafanya upotoshaji mkubwa na ndiyo tunasema tuptishe Muswada huu tufungue mjadala wa Katiba kama tunadhani Rais ana madaraka makubwa ndiyo tuone tuyapunguze vipi, lakini siyo sasa hivi. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nashangaa watu wana wasiwasi gani? Huu Muswada tunaoujadili licha ya kwamba Rais ana madaraka makubwa, imeweka vigezo kwamba Rais atakapoteua hao Wajumbe wa Tume kuna vigezo mbalimbali ataangalia; kuna masuala ya jinsia, masuala ya uwakilishi wa kijiografia na masuala ya uzoefu. Tuna wasiwasi gani? Huyu Rais tuna wasiwasi gani naye au tunapoteza imani naye kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kuwakumbusha Wanasheria wenzangu wanaopiga kelele huko nyuma, tutazame historia ya mabadiliko ya Katiba ambayo yamefanyika katika nchi yetu, kuna kioja gani leo kwa Rais kuunda Tume. Rais hao hao walikuwepo, Wanasheria wanajua na Wabunge wanajua na Wanaharakati wanajua. Kulilundwa Tume ya Nyalali, tulitumia Sheria Cap. 33 ambayo inampa madaraka Rais ya kuunda Tume yoyote.

Mheshimiwa Spika, Rais aliyejukwepo mwaka 1991 aliunda Tume ya Nyalali kwa ajili ya kukusanya maoni kama Tanzania ijiunge na mfumo wa Vyama Vingi au isijiunge. Nani asiyejua kwamba Tume hii iliundwa chini ya Kipengele kimoja tu cha Sheria. Mwaka 1998 Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia hiyo hiyo Cap 33, Rais aliyejukwepo aliunda Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Maoni ya wananchi kuhusu Katiba kwa ujumla. Tunaitambua kama *Kisanga Commission*. Kwa nini hatukuhoji, leo kuna tatizo gani, Rais ameamua kutuletea Muswada nzima, angeweza akatumia hiyo Sheria lakini ameamua kutumia Muswada huu katika kuunda hiyo Tume ya kukusanya na kuratibu maoni, Muswada nzima tuuchambue, tuujadili na Wabunge sisi ni wawakilishi wa wananchi. Tuna tatizo gani leo? Kuna kioja gani kwa Rais kuunda Tume, tena bahati nzuri anaunda Tume, lakini ametuletea Muswada mzima, unaeleza Tume itaundwaje, wajumbe watakuwajie. Angeweza kutumia tu Cap 33 na nani angehoji? (Makof)

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana, jana kuna watu wanaojiita kwamba ni Wanasheria sana eti wanasema mamlaka ya Rais ni ya kidikteta. Hivi dikiteta gani angeweza kuleta Muswada hapa mbele yetu asingetumia Sheria za nchi ambazo zipo? Ni usomi gani huo wa kujiona wewe ni Mwanasheria mzuri sana na mwanaharakati na wewe ndiyo mwanaharakati mzuri sana kuliko wanasheria wengine. Kwa kweli hatuwezi. Naomba niliombe Bunge lako Tukufu na bahati nzuri nimewahi kuwa sehemu ya wanaharakati na nime-focus Digrii yangu ya Pili katika masuala ya Haki za Binadamu na Demokrasia. Kwa hiyo, najua Katiba inatoa mamlaka gani kwa Rais, haki gani kwa wananchi, inatoa wajibu gani kwa wananchi na narudia alichosema Mwanasheria mwenzangu Angela Kairuki, wakasome tena vizuri Sheria na maandiko mbalimbali yaliyokuwepo wasilete uchochezi katika nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama Rais kweli angekuwa dikteta asingetuletea Muswada mzima kuuchambua hapa Bungeni. Lakini ameamua kuwa *transparent* ameamua kwamba tukae, tujadiliane na tuone ni kiasi gani tutaweza kuivusha nchi hii katika mchakato mzima wa kujadili Katiba mpya. Lakini natoa rai tena kwa Watanzania wanawake, wanaume, vijana, wavulana na wasichana wawahoji hawa ambao wanaleta uchochezi kwamba, je, uzoefu wa nchi nyingine katika kutengeneza Katiba mpya uko? Kwa nini hawayasemi? Tanzania ina tofauti gani na nchi nyingine za Kenya, Uganda na Ghana? Kuna kioja gani sis? Tuna tofauti gani na nchi nyingine? Wanasheria wanajua na hawa wanaharakati wanajua kwamba utaratibu wa kuunda Tume Maalum ya Katiba ndiyo utaratibu ambao uko sahihi, mzuri na uliozoleka. Sasa huu utaratibu umetumika Kenya, umetumika Ghana, umetumika Uganda. Tuna tatizo gani? Kwa nini usitumike Tanzania? Tanzania tunaishi tofauti na nchi zingine za Afrika? (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu niwathibitishie Watanzania, Serikali ina nia nzuri na huu utaratibu anaouleta Mheshimiwa Rais wa kuanzisha Tume ndiyo utaratibu uliozoleka. Wenzetu majirani Kenya waliunda *The Kenya Review Commission* mwaka 2005 chini ya Profesa, tuliambiwa juzi wote tunajua na zikatoka *draft* tatu za Constitution, wakajadiliana mwisho wa siku wakaamua watumie njia gani kwa wananchi kuweza *ku-validate* hizo *draft Constitution*. Lakini pia Uganda majirani zetu mwaka 2001 waliunda *The Uganda Constitutional Review Commission* hiyo hiyo kwa ajili ya kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi katika mchakato wa Katiba mpya. Zambia mwaka 2003 iliunda pia *The Constitutional Review Commission* kwa ajili ya kazi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi Rais wa Ghana ameunda pia Tume ya *ku-review Constitution* ya mwaka 2010. Ni kioja gani leo kwa Watanzania kuanzisha mchakato wa Katiba kwa kuunda Tume? Hawa wanaharakati kwa nini hawasemi ukweli, kwa nini hawawaleweshi Watanzania? Kwa sababu bahati nzuri sisi Wanasheria kuna kitu tunaita *precedent*, hiki kimefanyika katika nchi nyngine kwa nini kisifanyike hapa, mbona katika Sheria mambo mengine tunatumia?

Mheshimiwa Spika, muda unamalizika lakini niseme, suala lingine ambalo limehojiwa hapa na nimesikitika sana eti kwamba wanahoji kifungu cha 18 ambacho kinasema ripoti iwasilishwe kwa Rais. Jamani huyu mtu ndiye ameitura Tume, ametoa *terms of reference* kwa mujibu wa Muswada, *terms of reference* sasa hivi zimekuwa ni sehemu ya Muswada. Mnataka hii ripoti ipelekwe kwa nani. Tuna ushahidi *Kisanga Commission* na *Nyalali Commission* ziliundwa na ripoti zilipelekwa kwa Rais lakini kuna mapendekezo ambayo Serikali haikuyataka lakini hayakuwekwa *public*? Yaliwekwa wazi na watu kuna mengine waliyakosoa, Serikali haikuyapenda, mengine wameyafanya kazi. Kuna tatizo gani leo kwa ripoti hii kupelekwa kwa Rais, wanashawishi kusema kwamba maoni ya wananchi ooh yakienda kwa Rais yatachakachuliwa!

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania waelewe kwamba hakuna nia mbaya yoyote ya Serikali ya kutaka kuficha au kuchakachua mawazo au maoni yoyote yatakayotolewa na wananchi. Kama tulivyosema Katiba inasema kwamba chini ya ibara ya (8): "Mamlaka ya Serikali; wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii." Hatuna, wala Serikali haina dhamira yoyote ya kutaka kuchakachua mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niwathibitishie Watanzania wenzetu na hasa wanawake, sasa hivi tuko katika mchakato wa kutaka kuanzisha Tume ili mawazo yao yaweze kufanyiwa kazi. Tunataka Katiba ya namna gani? Wanawake wote wa Tanzania tutoe baraka kwa Bunge, Muswada huu upitishwe kwa sababu mimi kama mwanamke ningependa sana tuingie katika *stage* inayofuata ya Katiba mpya. Tunalamikia Sheria kandamizi, sheria zinazotunyanya. Kwa hiyo, nataka kuwasihii wanawake, mchakato unaokuja mtasema sasa kwenye hii Katiba, wenzetu wa Uganda kuna kipengele cha Katiba kinasema, sisi ya kwetu inasema tu, nina haki ya kutobaguliwa kama mwanamke.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Uganda wamekwenda mbali, Katiba yao ina-*declare* Sheria zote za nchi ambazo zinambagua na kumnyanyasa mwanamke ni batili. Wanawake wa Tanzania ndiyo muda huu. Ndiyo muda huu wa kusema tunataka. Sasa huu mchakato uende haraka sana kusudi na sisi hii Katiba sasa tutakapoanza kutoa maoni yetu tuseme Katiba itamke wazi, Sheria zote za kimila zinazobagua na kumnyanyasa mwanamke hatuzitaki. Ndiyo muda huu wanawake wa Tanzania tuachane na propaganda zisizo na maana. Tuachane na maneno yasiyo na maana, tutoe baraka kwa Serikali Muswada huu upitishwe kusudi sasa tuanze mchakato wa kutoa maoni yetu na ninatoa rai wote tushiriki kwa pamoja tunataka 50 kwa 50, tutaipataje kama Katiba haitasema 50 kwa 50. Kwa nini tucheleweshe huu mpango? Wanaochelewesha wana nia gani ya kutaka tucheleweshe huu mpango wa kuruhusu Serikali iendelee na mchakato wa kukusanya maoni ya Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kwamba wanaofanya upotoshaji huu, wanafanya lakini sijui kwa maslahi ya nani na mimi nilikuwa wanaharakati, najua siasa za kuendesha uwanaaharakati, kuna *interest* nyuma zimejficha. Lakini watuambie ni kwa manufaa ya Watanzania au ni kwa manufaa ya kwao, ni kwa manufaa ya nani? Wanaposema wananchi

hawajawakilishwa, hawa Wabunge wote wanawawakilisha wananchi au wanataka wananchi wawakilishwe katika *forum* gani zaidi ya hii? (Makof)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makof)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa nilikuwa nimepewa taarifa toka mapema, kuna mtu kati yetu alisahau miwani yake sehemu ile pale, kama yupo humu ndani basi atakapotoka achukue kwa hawa askari walipo hapo. Lakini la pili, Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee kujadili na mimi najua katika kukaa kwangu Bungeni wanaharakati walikuwa wanasaidia sana kutunga sheria, walikuwa wanasaidia kuleta *amendment* siyo vinginevyo. Ndiyo walivyokuwa wanafanya na hapa ndiyo kipindi cha kutunga Sheria na sheria hii iko mikononi mwetu, hakuna mwananchi atakayetunga hii isipokuwa sisi wenyewe.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Masele Mabumba) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza mjadala, napenda kuwatambua wageni walioko Jukwaa la Spika. *We have a Swedish Ambassador in the Speaker's Gallery, Mr. Lennarth Hjelmaker. He has been accompanied with Ms. Margareta Brismar and Mr. Daniel Axxelson. We have also Logan Wheeler and Bi. Tina Mdobilu. Also we have Dr. Caroline MacQueen. We have also Vesmone Salvassius. (Applause)*

You are most welcome to our Parliament.

Tunaendelea na mjadala wetu na napenda kuwataja tunaoanza nao sasa hivi nao ni Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Anna Tibaijuka. Tunaanza na Mheshimiwa Anna Mkanga.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naitwa Margareth Agnes Mkanga sio Anna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kutoa machache tu yanayohusiana na Muswada huu muhimu ambaa utaleta hatimaye ni nini tunataka kama Sheria Mama ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, nimshukuru Mwenyezi Mungu, jana nilijisikia kuumwaumwa kidogo nikasema aah, mbona nimeomba kuchangia? Leo kaniamsha salama kabisa, namshukuru pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja nyingi tu zilizotolewa na walionitangulia lakini kwa taratibu za Bunge, ukiona jambo linasemwa na wengi, ndio hilohilo lina maana yake inakubidi ulizingatie. Kwa hiyo, mimi nitazungumzia mlemle labda kwa lugha nyingine au kwa msisitizo wa aina yake. Hili suala ni muhimu na mimi kama mwakilishi nimeona nisikose nafasi hii ya kuzungumzia masuala yanayoelekeana na wale ninaowawakilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila mimi ninaanza kwa mshangao, tangu siku ya semina tumeelimishwa vya kutosha. Jumapili na jana, nikawa nataka kama kuchanganyikiwa nikajiuiliza hivi hapa nachanganyikiwa nini? Kwanza, mimi *personally* baada ya kuusoma vizuri Muswada huu, wala sikujuu kama utakuwa na mikingamo mpaka watu wanataka kuandamana! Nimeona huu Muswada ni *so straight forward*, kwamba ni maandalizi ya kitu. Sasa nashangaa maandalizi tunayagomea, sasa hicho kitu tutakipataje? Ndio maana nasema nashangaa! Yaani tumekazana tusipande mbegu, hivi tutavuna mahindi bila kupanda mbegu? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nashangaa upotoshaji huu unaoendelea! Hauna sababu kwa watu ambao tunaelewa kabisa! Kama wenzangu walivyosema yaani wengine nawashangaa! Mimi sio Mwanasheria, lakini mbona katika Muswada huu labda maneno tu yale ya kisheria, lakini maudhui yake mbona yanaeleweka hata kwa mtu ambaye hajaenda shule ya sheria? Tatizo ni nini? Kigumu kiko wapi? Tunataka tu kupindapinda ili tucheleweshe muda. Lengo la Mheshimiwa Rais, mimi ninadhani ilikuwa Sheria Mama hii tuiplate kabla ya mwaka 2015, ndivyo nilivyokuwa ninawaza mimi kwamba mwaka 2015, ikifika kwenye uchaguzi angalau tuwe tumeanza kutumia hiyo Sheria Mama. Sasa tunaposema turudi mara ya tano, mara ya sita, hivi si tunachelewesha nafasi ya wananchi kujadili kwa muda mrefu kabla ya muda! Tunataka kuwachelewesha tu ili baadaye waje waseme eeh, kujadili kwenyewe tumepewa dakika tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhi kusikia watu wakisema tukipata madaraka haya, miezi mitatu tu tayari Katiba, ambayo ni siku 100 unaongeza siku 10. Hivi ndio tungeendeshwa? Sielewi utaratibu ungekuwaje. Hivi hiyo Katiba ingekuwa kweli ni Katiba iliyochambuliwa, ikashirikisha wananchi kama inavyodaiwa sasa hivi, tena kwa kupanda mbegu tu? Kweli watu wangepata nafasi? Tungepata nafasi sisi, nisime watu na mimi ni Mtanzania, ningepata nafasi ya kuchanganua Katiba hiyo ambayo tungeipata kwa siku 100? Kwa hiyo, lengo labda ni kuchelewesha ifikie hiyo 100 halafu tusiwe na nafasi ya kusema tunataka mambo yetu yawe vipi! Kwa hiyo, mimi ninaendelea kushangaa, lakini ninawaomba wananchi wasishangae. Huu Muswada haukuwa na tatizo kabisa kwa sababu ni mwanzo tu ili tuweze kupata kitu kamili. Sasa mkitukataza mwanzo, basi hatutaendelea na hicho tunachokitaka. Ndio lengo tusiwe na Katiba Mpya? Manung'uniko ya muda mrefu yalikuwa ni kutaka Katiba Mpya sasa mbona tunajikanganya wenyewe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naendelea kushangaa! Wanasema mamlaka ya Rais ni makubwa sana. Navyoolewa mimi bado Katiba tunayoitumia ni ile ya mwaka 1977 iliyorekebishwa kidogo mwaka 1984. Mle tulimpa Rais madaraka kwamba, ye ye ndiye Mkuu wa Nyumba hii, Tanzania. Akiwa Mkuu ndio atatuongoza na akishatuongoza, hata Majeshi atayaongoza. Jamani hata ndani ya nyumba mtakuwa 20, lakini lazima kutakuwa na Kiongozi. Si kiongozi yule, pamoja na kwamba ni lazima ulete usawa ndani ya nyumba, uwapende watoto, hutakubali! Mimi ni kiongozi wa nyumba yangu, nawapenda wote na ninaendanao sawasawa, lakini sikubali, haitatokea kwamba eti wanidharau, huyu anapanda hapa, anapanda hapa, bila sababu, no! Nitaongoza. Kwa hiyo, hata kwenye nyumba kuna kiongozi. Sasa nashangaa kwenye nchi tunasema sio! Tulimpa madaraka wala sio kwamba aliomba. Mimi hapa naomba kutofautiana, nadhani tunakosea, huyu Rais tunamchukulia kwamba ni Mheshimiwa Kikwete kama sura ya Kikwete, jamani, Urais ni Taasisi! *Anybody can be there.* Hata wa upande wa pili huu anaweza akawa pale! Hivi ndio tutawapanda tu hovyo hovyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wajibu wake kuendelea kutuongoza kwa sababu tulimpa hiyo heshima. Hata katika Katiba hiyo Mpya, mimi sidhani kwamba haya tutayashusha sana lakini inategemea wananchi na wenzetu watakavyoona inafaa lakini kwa sasa hatuna Kiswahili kingine, Mkanga hapa apewe kuongoza kuunda Tume, mimi inanihu vipi! Kwa nini tunalilia vitu ambavyo havina hata sababu jamani? Katiba hii ambayo tunayo ndio inayotuoongoza labda mpaka hapo tutakapokuwa na hiyo Katiba Mpya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazungumzia haya, mimi nitajikita kwenye mambo machache kidogo. Kwa sehemu ile ambayo tunazungumzia uundwaji wa Tume na wale wajumbe, kama walivyoshauri wenzangu na makundi mengine yote yakaongezeka, lakini mimi kisehemu kile cha makundi mengine naishauri Serikali iyachanganue sawasawa. Maana hapa kama watu wenye ulemavu, nadhani ndipo tulipo hapa na wao wanalamika kwelikweli na wenzangu ndugu zangu wenye ulemavu nchini hapa, wakati ni huu, msiturudishe huku, tupande mbegu ili yale tuliyokuwa tunayafikiria tuyaseme hapo. Tulikuwa tunadai, aah, Mheshimiwa Rais ana zile nafasi 10, angalau hata tuwili ingekuwa vizuri! Ndio wakati unakuja huo, lakini mtupe ruhusa kwanza kuweka utaratibu ili tufike huko, hayo ndiyo tutayasema huko. Mkae mkao wa kuchangia kwa dhamira zetu yale ambayo tunataka yawepo kwenye Katiba Mpya, yatakayotuletea maendeleo, ukiingiza na yale ya kimataifa tuliyoyapata, ukahusisha na Sheria yetu ile, wakati ndio huu, tukikosa hiyo nafasi basi, hiyo fursa tusiililie! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Ibara ile ichanganuliwe vizuri ili wengine wasisahaulikesahaulike, kabisa. Hata kuisadia Tume kwamba inakwenda kwa makundi gani kuweza kupata yale walionyayo miyononi mwao ili tuweze kupata mkusanyiko wa mawazo mzuri ambao utawekwa sawasawa ndipo baadaye Bunge Maalum la Katiba liweze kuona nalo mambo yanakwenda namna gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda kukikazania hapo ni licha ya kuchanganua haya makundi, labda kidogo ingeelezwa hivi yatapatikanaje? Sawa, Mheshimiwa Rais atateua, lakini kwa mfano hili kundi maalum, sijui kitu gani, tuko lundo hivi, ni wangapi, wangapi na watapatikanaje ili waweze kuwa wajumbe wa Tume! Hilo naomba pia liweze kuwekwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilohilo naomba tena tuisaidie Tume; itakapofikia wakati wake wa kukusanya maoni huko, labda mngefafanua pia nyenzo zitakazotumika kuyafikia makundi haya. Mimi hapo ninasisitiza wenye ulemavu. Kuna wenye ulemavu wasioona na wenye ulemavu viziwi na albino, hasa hawa wawili sana hawa, viziwi! Sio wanaendewa halafu wanachekacheka tu kwa sababu hawaelewi linalosemwa, lugha yao ya alama ni muhimu. Muifikirie hapo, sijui mnaifanyaje. Wanaweza wakashindwa kutoa mawazo kwa sababu ya vikwazo vya mawasiliano. Wasiiiona labda wanaweza wakataka kuandika, wakasema tukutane tuandike mahali, bila habari ya nukta nundu, hapo inakuwa ni matatizo. Ndio haya ndugu zangu mlikuwa mnalalamika, ndio tuyaweke kwenye Katiba ijayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba kutoa ushauri unaofanana itakapokuja kwenye Bunge Maalum la Katiba. Pia kuna makundi yamesemwa hapo, naomba ufanuzi uwepo, tuangalie tutakavyofanya kuweza kupata kundi hili kuingia kwenye hilo Bunge Maalum la Katiba ili tusiwaache wengine nyuma. Hakuna nusu mtu, lakini tuangalie hapo tunachanganyaje! Nusu mtu hayupo, kwa hiyo labda atakuwa mmoja mmoja au nini, itaangaliwa jinsi inavyopaswakuwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nilikuwa nataka nishauri, kura ya maoni ya wananchi ni muhimu sana kama Muswada ulivyoelekeza. Itakuwa kama ndio karibu tunafikia kwenye mwisho wa mchakato mzima wa kupata mahindi na hiki tunachokifanya ni kupanda mbegu. Madaftari ya wapiga kura yarekebishwe mapema ili vijana ambao ndio wameibukia miaka 18 wasikose nafasi ili baadaye pasije pakawa na malalamiko ya kwamba, wengine hawakupiga kura na nini. Pamoja na kwamba, hiyo itatubidi sisi tulipata mwanga sawasawa kabisa wa sheria hii kusaidia kuelimisha pamoja na kwamba tumeambiwa wanasiasa hatuelimishi, lakini mimi nikiwa na watu wangu wale, wanawake eeh! Jamani mje mpige kura! Si nimesema! Sikuwaambia mnapiga kura kwa kitu gani lakini nimeshawaeleza, jamani eeh, muda ukitimia pigeni kura! Ndio hayo ambayo yanatupasa kwenda kuyafanya huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamechangiwa. Niwaombe Waheshimiwa Wenzangu, huu Muswada wala sio mgumu, tuupitishe kwa manufaa ya Watanzania ili wawe na uwezo wa kutunga Katiba Mpya ambayo ilitakiwa na Mheshimiwa Rais, ameona kutokana na muda na tafakari yake na Mungu tu alivyomjalia, ni vizuri jamani tukamaliza Bunge tukiwa tumeacha kitu chenye manufaa kwa nchi hii. Mimi najisikia fahari, kama Mungu ataniweka hai nikawemo humu, nasema eeh, mbona imekuwa ni vizuri. Tuwaelekeze wananchi katika mema kwa sababu tunachonuwia ni uzuri, ni wema, ni amani, ni utulivu, ni ushirikiano. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makof*)

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika mahojiano ya Muswada huu, jambo ambalo ni la kihistoria katika nchi yetu. Miaka 50 baada ya uhuru, ni jambo la kujivunia kabisa kwamba tunajikuta katika hali ya kuweza kujadili Muswada huu katika hali ya amani na utulivu. Hili jambo si dogo na inabidi tujipongeze na kuwapongeza Viongozi wetu waliotutangulia na waliopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiria kwamba, hatua tulioifikia ni kubwa sana na sina budi kumpongeza kabisa Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kazi nzuri

aliyofanya kutufikisha hapa. Kwa sababu, ukiangalia Muswada tuliokuwanao, yeye na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kazi ambayo wameifanya si haba ni kubwa sana na huwezi kupinga kwamba, hatuna Muswada ulioboreshw, umeboreshwa vya kutosha. Sasa suala linakuja; katika zoezi zima la kutafuta Katiba Mpya, ina maana tunazungumzia mustakabali wa Taifa letu, kwa hiyo, hili jambo huwezi kulichukua kimzaha-mzaha. Kitu cha kwanza kabisa, wakati ni mali tena wakati ni rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa hiyo, tukichezea wakati, tukaingia katika mambo ya ujanaujanja na propaganda bila kufanya kazi iliyo mbele yetu, mambo yatakuwa magumu kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wengi wameshælezea, nadhani sasa hivi hakuna mwananchi wa Tanzania ambaye haelewsi sasa kwamba, hii sio Katiba yenye! Hii ni *process*, ni taratibu za kupata Katiba mpya. Sasa kama mtu anataka kuchakachua kwamba, taratibu sasa inakuwa hoja zenyewe, nadhani hapo kwa kweli inabidi hayo tuyaweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme kwamba, kwanza niipongeze Kamati ya Bunge ya Sheria na Katiba, ambayo tayari imeshaupitia Muswada huu, imeshatoa maoni yake ambayo yatatusaidia sisi wengine ambao hatufuatilii jambo hili kwa kina zaidi kuliko wao na kwa utaalamu zaidi kuliko wao maana Wajumbe wengi katika Kamati ile ni Wanasheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii kufafanua kwamba, tutakapotoka kwenye hizi *procedures* tunaingia kwenye Katiba yenye, ni *substance*, hiyo sio Sheria! Kutunga Katiba, sio Sheria. Kwa sababu Katiba yenye ni chombo cha Kisheria ambacho kinælezea siasa na itikadi, watu mmekubaliana kukaa vipi katika nchi. Inaitwa *Ideological Hegemony*. Kwa hiyo, ni jambo la faraja kwamba Muswada tayari umeweka misingi ya kuzungumzia Katiba Mpya. Tume hiyo ni lazima iwe na misingi fulani, yaani *values* na *ethos* za Taifa hili ambazo tunazilinda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize hilo maana ni muhimu kwa sababu nchi yetu ya Tanzania ni nchi ambayo ipo, ni *United Republic of Tanzania*, ndivyo nchi hii inavyojulikana. Kwa hiyo, kusema kwamba tunazungumzia mchakato wa kutafuta Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni jambo ambalo halijadiliki. Kwa hiyo, kama mtu anajaribu kulijadili hapo lazima atueleze *agenda* ni nini. Mimi nafikiri hilo ni muhimu tulielewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nigosie suala la uwakilishi. Mimi nimesoma na nimejaribu kutafakari kwa umakini kabisa mchango wa wenzetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Nielewavyo mimi wameshatoa mchango wao hapo. Kwa hiyo, suala kwamba hakuna mchango wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani, nafikiri inabidi pia tulielewe kwa undani wake hata *record*, Mheshimiwa Lissu alipokuwa anatoa mchango wake alisitisiza *Hansard* ipokee *report* yake, kwa hiyo, *he is on record* kwamba ameshachangia. Sasa kama wenzake waliamua kwamba watachangia kwa kutumia mtu mmoja sisi wengine ambao tunachangia tofauti basi tunaendelea. Kwa hiyo, mimi nafikiri hiki ni kitu muhimu kukturambua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hali ndivyo ilivyo, naomba niseme kwamba uwakilishi ambao upo ndani ya Muswada, ni uwakilishi mzuri kwa sababu Bunge Maalum la Katiba kwa kweli ni shirkishi na nawapongeza wallobuni na kuhakikisha wawakilishi wengi wanakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tumepepe nafasi, Wawakilishi wa Zanzibar wamepepe nafasi, wanaharakati wenzangu na mimi nilikuwa mwanaharakati hakuna mtu asiyejua hili na wenyewe wamepepe nafasi na vikundi maalum pia vimepepe nafasi labda kama mtu anataka *chaotic situation* yaani *anarchy*, yaani kama mtu anataka *direct democracy* ambayo ipo Switzerland, ni nchi peke yake duniani ndiyo imeweza ku-practice *direct democracy* ambapo kila mtu anakuwa mezani. Nchi ya Switzerland kwa uwezo wake wa kifedha inaweza kuwa na mfumo kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme wengine tunaangalia mchakato huu kwa fani zetu, mimi ni Mchumi kwa taaluma, huwezi kuchezea wakati because time is money lakini pia lazima ujue nyenzo tulizonazo ili kumaliza zoezi hili lakini pia ni lazima tuwe na mfumo ambao utatuwezesha sisi kuweza kumaliza kazi kwa muda tulionao. Sasa kama watu wataendelea,

Wazungu wanasema *discussing work instead of doing it*, yaani mtu unakaa unazungumzia kazi badala ya kufanya kazi. Muswada huu unatuwezesha sisi Watanzania kuanza kufanya kazi, kazi ni wananchi wenyewe sasa kusema wanataka Katiba Mpya iweje, matatizo ambayo yapo au maoni ambayo yapo wala sisemi kwamba ni matatizo kwa mfano, madaraka ya Mheshimiwa Rais kwa sasa hivi Katiba inampa madaraka yake na huwezi kuyapinga maana ukiyapinga utakuwa unakiuka Katiba. Lakini wakati wa kutoa mchango utasema hayo madaraka yaweje ndio tunajaribu kuuwekea utaratibu ili kusudi wananchi wapate nafasi ya kutosha kusema wanataka iweje na kadhalika. Kwa mfano, muundo wa Serikali, hili nalo Muswada unaruhusu lijadiliwe lakini kwa misingi ambayo tunasema ni *constructive* siyo ile ya kupotosha na kuleta fujo mambo yakaharibika. Kwa hiyo, msimamo wangu nafikiria kwamba hapa tulipo ni pazuri sana, wakati ni mali hautusubiri kwa hiyo, kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kusudi kazi iendelee nikirudi kwenye Muswada wenyewe labda mapendekezo, kuna vitu vingine kwa mfano katika kutafuta muafaka na uwakilishi, kwa mfano nilikuwa naangalia Muswada wenyewe, kuna mapendekezo ambayo unaweza kusema ni *specific* mapendekezo kwa mfano kama Spika wa Bunge Maalum ametoka Tanzania Bara sasa basi itabidi Makamu wake atoke Tanzania Visiwani, sawa kabisa. Sasa unapokuja kwa Katibu wa Bunge Maalum na hapo ikionekana kwamba labda Mwenyekiti katoka Visiwani au katika upande mmoja wa Jamhuri, sasa na Katibu aangaliwe, mimi kwa mtazamo wangu nasema kwamba *this shouldn't be carried too far*, kwamba vitu vingine kuna haja ya kuwa *pragmatic* ili kusudi kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mimi nimezoea kupokea maoni tofauti na ninayachukua *positively*, kwa hiyo, nimesoma kabisa kwa karibu zaidi mchango wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa mfano kuna Ibara au kipengele kinachomruhusu Rais akilazimika kurudi Bungeni, hili mimi nimeliona Kenya. Nilikuwa Mkuu wa Umoja wa Mataifa Kenya wakati wa *process* ya kupata Katiba yao inaendelea lakini walijikuta kwamba pamoja na *BOMAS* kuwa wameshatoa Rasimu ya Katiba lakini bado kulikuwa hakuna muafaka kwa hiyo wakalazimika kurudi kwenye *drawing board*. Kwa hiyo, kuweka *mechanism* ya utaratibu huo siyo mbaya lakini mimi nafikiria kudai kwamba hakuna uwakilishi katika mchakato mzima si kweli. Mimi nasimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Muleba Kusini na kwa ujumla wao, wake kwa waume, vijana kwa watoto, wakulima na wavuvi na wafugaji, wenyewe waliniamini wakasema wewe Anna Tibajuka utatuwakilisha Bungeni. Kwa hiyo, ninapozungumza hapa ni Muleba Kusini inazungumza. Kwa hiyo, huwezi kusema hakuna uwakilishi na mimi nafikiri hapo tutakuwa tunapoteza na kuwachanganya wananchi wetu, uwakilishi wanao kwa sababu Bunge hili ndicho chombo walichokweka na walichokiamini kwamba kisimamie maslahi yao. Nadhani utakuwa huna akili timamu ukijaribu kusema kwamba hapa mtu unajiwakilisha mwenyewe kwa sababu haiendi namna hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hiyo inakubalika, basi na hivyo hivyo kwa Mheshimiwa Rais wa nchi hii, kwa sasa hivi kwa Katiba ilivyo hili ni jukumu na ni kazi kubwa ambayo ipo mikononi mwake na tunamtegemea Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kutusaidia kupata Katiba Mpya maana tukifanya mchezo, tukapoteza wakati huu, nimeshasitiza kwamba wakati ni mali, mimi kwa upande wangu na kwa niaba ya wananchi ambao ninawawakilisha naona kwamba zoezi hili limefika wakati wake kusudi wananchi wapate muda wa kutosha kutoa maoni yao. Vilevile nikizungumza kama mwanamama niungane na wale waliosema sisi wanawake tunataka kuona haki za wanawake zikiwa *declared* katika Katiba maana haki lazima ziwe *declared*, huwezikuwa na haki ambayo Sheria Mama haiitambui. Kwa hiyo, vitu kama hivi vitatupa nafasi ya kutoa maoni wananchi wote kwa ujumla wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la utata wa Bunge Maalum kwamba siyo shirkishi, mimi nataka kusema kwamba nalionia ni shirkishi kabisa na limeweka nafasi ya watu wengine ambao wako nje ya hivi vyombo vya uwakilishi na wenyewe kuwa pamoja na sisi na haitakuwa na maana yoyote kama sisi Wabunge kuwa ndani ya Tume, maana sisi tutakuwa kwenye Bunge Maalum *so you can not be judge and juror in your own case*. Kwa hiyo, sisi tutatoa ushauri kwa sababu tutakuwa na wananchi wakati wanatoa mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi huo ndio mchango wangu, naomba kabisa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako na sasa namwita Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Capt. Komba, Mheshimiwa Esther Bulaya na Mheshimiwa Simbachawene wajiandae.

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kuhusiana na mada ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mawaziri wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lakini pia na Watendaji wote walioshiriki katika mchakato huu. Nawapongeza pia wadau waliotoa maoni yao ya kuboresha mchango huu mpaka tukufikia hatua hii leo Muswada unasomwa kwa Mara ya Pili na kuchangia kwa ajili ya hatua inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi nalotaka kuwahimiza ndugu zangu Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla ni kwamba mchakato huu safari hii umetushirikisha au umeshirikisha pande zote mbili kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa hiyo, ni jambo la busara sana ambalo Serikali imelifanya, kilichobakia sasa hivi ni kwenda mbele na kufikia lengo tulilokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ninachowahimiza ndugu zangu Zanzibar waelewe kwamba kinachoendelea hapa ni kutafuta njia ya kuweza kukusanya maoni kwa ajili ya Katiba Mpya tunayokusudia iwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya siyo majadiliano ya Katiba, ni majadiliano ya Muswada wa kuunda Kamati au Tume ya kupita mitaani, vijiji, Wilayani, Mikoani ili kuchukua au kupata maoni ya Watanzania, watoe maoni yao wanataka Katiba yao Tanzania iweje, kwa hiyo, ndugu zangu huko mliko mjiandae itakapofika wakati Tume itakapokuwa tayari kila mmoja ajitokeze alipo tutoe mawazo yetu. Nafasi ndio hii, tutajitanua na kujieleza kwa kila mmoja alilokuwa nalo na Zanzibar imeshirikishwa kutoka alifu mpaka hii, mnaelewa nikisema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuwahimiza ni kwamba Katiba inayotaka kuundwa ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi Zanzibar ni wadau wakubwa wa Muungano huu. Bahati mbaya sana lakini ndio Mwenyezi Mungu aliyotujaalia Watanzania wengi walikuwepo sasa hivi iwe Visiwani au Bara wamezaliwa Tanzania, wameukuta tu Muungano, hawakuzaliwa Zanzibar ile ya Rai ya Sultani wala Tanganyika ile ya Mkoloni bali wamezaliwa Tanzania, hawajui na hawawezi kulinganisha kulikuwa na nini na sasa kuna nini na ndio maana wengine wanatoa maneno ambayo kwa kweli kadri mimi nilivyokuwa hayaona sioni kama wana dhamira hasa ya kuudumisha Muungano huu amba ni adhimu kabisa na kama ulikuwa ni umri maana Muungano una umri wa miaka karibu 47 sasa na wanaotoa mawazo yao wengine wana umri huohuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukizungumzia maudhui ambayo yapo katika hotuba hii ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kuna mambo ambayo mimi binafsi yamenitia wasiwasni kama kweli huyu mtu ni muumini wa Muungano wa Tanzania. Inanitia mashaka kabisa kwamba huyu mtu hana nia wala haja kabisa ya Muungano huu kwa sababu kwa desturi ya kuyatoa maelezo yake katika Bunge hili Tukufu, katika hotuba zake zote ni ya kudhalilisha na kukejeli Zanzibar ambayo ni sehemu kubwa ya Muungano wa Tanzania. Hapa inanipa mashaka kama kweli huyu ana dhamira kamili, sidhani! Namuona yuko tayari *at any cost* kuuvunja Muungano huu, sijui katumwa na nani au sijui anashirikiana na nani, sielewi! Hayo ni mawazo yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina sababu nyangi sana za kusema hivyo, kwa mfano, anafikia hadi kusema kwamba Zanzibar haiwezekani kabisa kuwa na uwakilishi kamili au sawasawa na Bara wakati hiki kitu sote tunafahamu kwamba ni Muungano wa nchi mbili zilizokwu huru zikajitolea kwamba tufanye kitu kimoja, iweje leo mwininge azidi na mwininge apungue? Hii nafikiri haikuwa sahihi lakini anafanya hivyo kwa makusudi siyo kwamba hajui kwa sababu yeye kama anavyojita ni Msomi lakini usomi wake mimi hapa ndio unaponishangaza. Kwa sababu haya aliyojasema au aliyoandika yeye mwenyewe na hata katika hotuba

ambayo ilipita katika mkutano wa bajeti yalikuwa yana kila dalili ya kuonyesha dharau na kejeli kwa Zanzibar. Mwisho wake mimi nilikuwa nayachukulia labda kama mashairi ya rusharoho hivi, kwa sababu mashairi ya taarabu ndiyo yana maneno ya vijembe, matusi, maneno ya kashfa na mwenyewe anapokuwa yupo pale anapozungumza hutamba hasa kama yuko kwenye *stage* lakini mimi nataka kumwambia kwamba kama yeye hajui asili ya taarabu au rusharoho, asili yake ni Zanzibar na sisi Zanzibar hatukwenda shule wala hatuendi shule kwa kutunga mashairi kama hayo anayotunga yeye, sisi mistari inatutoka tu bora tufumbue mdomo, sasa yeye anapokaa hapa akaanza kuikejeli Zanzibar au akejeli Muungano ni kitu ambacho kwa sasa sisi kinatutia uchungu sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba ndugu zangu wa Zanzibar msihangaike wala msibabaike na huu upotoshwaji unaotokea kwenye vyombo vyahabari lakini pia upotoshwaji ambao huyu Bwana alikuwa anausema jana hapa, tulieni na mshiriki kikamilifu katika mchakato utakaokuja kwa ajili ya kutoa maoni ili tuunde Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi wawakilishi wenu mliotutuma tupo hapa kushirikiana na wenzetu kama ulivyoanza mwanzo mchakato huu na tutafikisha mwisho salama salmini lakini jambo kubwa zaidi ni kudumisha Muungano wetu uendelee mpaka mwisho wa dunia hii. Nafasi ya kuitumia ni hii ndugu zangu, kila mmoja atoe maoni yake kwa jinsi anavyoona yeye, yatakusanywa, yatajadiliwa na mwisho wake tutapata Katiba muafaka kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wanaufahamu huu Muungano wa hapa Tanzania watakumbuka kwamba mnamo mwaka 1964 hata hilo jina la Tanzania yenyele halikutangazwa tarehe 26 ile tunayoishereheke. Serikali ya Zanzibar na Tanganyika ilikuwa zimeshaungana lakini jina la Tanzania lilitolewa matangazo kwamba kila mmoja ajaribu kutoa mapendekezo ya jina wakati huo mimi nikiwa shule ya msingi, nakumbuka wanafunzi na watu binafsi walitoa mapendekezo yao na mnamo mwezi wa tisa, mwisho wa mwaka ndiyo likapatikana jina la Tanzania. Sasa leo anakuja mtu kusema maneno kama haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja ambacho kilikuwa kinanishangaza sana, huyu mtu anafikia hadi kusema kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alichaguliwa kwa Katiba halali, Katiba hiyohiyo ndiyo iliyompa fursa yeye akawa hapa, leo anakuja kutamba mbele na kumuita Rais wa kifalme, haya ni matusi. Navyofahamu mimi na niliona ufalme, kule kwetu tuliwahi kutawaliwa na Sultani ambaye alikuwa ni mfalme. Katika Baraza lake la kifalme la kutunga Sheria na kutoa maamuzi Mfalme huchagua *royal family* yaani jamii zake tu hatoki mtu mwingine. Sasa huyu ana uzoefu wa huko aliko ndiko kwenye utawala wa kifalme kwa sababu kuna dada na kaka, baba na mjomba, shangazi na kaka, haya mambo hayazungumzwi hivihivi anafahamu yalipo na ndiyo uzoefu wake lakini Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais huyu amechaguliwa kwa demokrasia na kwa kura za wananchi wa Tanzania, huyu hakuchaguliwa kwa kaka njoo, dada njoo, mkwe chukua, shemeji chukua, hakuna kitu kama hicho! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi mmoja pia juu ya uhalali wa hicho Chama kwa sababu haiwezekani kabisa Chama cha *CHADEMA* kikawa kinazungumza kiusaliti kwa sababu akizungumza Msemaji wa Kambi ya Upinzani ndiyo chama, kukejeli upande wa pili wa Muungano na chama hiki kinatakiwa upande wa pili kiwe na wanachama halali ndiyo kiwe halali, lakini leo anakaa anakejeli na kutukana, hiki chama kweli kina uhalali? Mimi nafikiri kuna haja ya kufanyiwa utafiti kwani nina mashaka nacho kwa sababu wanahitajika na kule wawe na wanachama wanaokidhi haja ya kukifanya chama hiki kuwa cha Kitaifa, leo huyuhuyu anatutukana na kututumia madongo kule, jamani, mimi nina wasiwasi sana lakini kama anataka aje atuthibitishie na aje afanye maandamano kule, tunamkaribisha sana. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Aje!

MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH: Aje, tunamkaribisha na kule nako aje afanye maandamano ataona, tutampokea sisi. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi nachowahimiza tena ndugu zangu Wazanzibar, hii ni hatua ya kutafuta Tume ya kupokea maoni ya wananchi katika kujenga Katiba yetu mpya siyo mjadala wa Katiba, katiba mjadala wake bado. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu leo ni kutoa tu mapendekezo machache kwa Serikali kuhusu Muswada huu. Kwanza niseme nisije nikasahau, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusoma Muswada huu kasoro ni ndogondogo, nilizoziona mimi ni mbili tu, moja nilikuwa nataka Wazanzibar katika wale wajumbe 116 wanaoteuliwa wasipungue theluthi moja na hawa wa Bara wawe na theluthi zingine hizo ili kuweka uwiano na nguvu ya Muungano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napendekeza Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano wawe na uhuru zaidi, hawa Wanasheria wasubiri baadaye. Kwa hiyo, kile kipande cha Wanasheria kiondolewe kama alivyo sema Mheshimiwa Ole-Sendeka leo mchana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina wasiwasni mkubwa wa yule Msomi wa jana, hivi yule bwana ni Msomi kweli aliyeenda shule? Mimi nafikiri kusoma si kwenda shule, kusoma ni kuelewa unachofundishwa na kuelewa kutawala mazingira yaliyoko pale, yule bwana hajasoma kabisa, anaposema kwamba mjadala huu ama Muswada huu ni wa Serikali ya Muungano wa Tanzania, huwezi kuizungumza Tanzania bila kuizungumza Zanzibar. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utazungumzaje Serikali ya Muungano halafu hawa wanaounda Muungano, wadau wa Muungano unawaambia wasihusike, utautoa wapi Muungano, labda Muungano wa Slaa na Muungano wa nani na nani, Muungano huu ni wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zanzibar iko pale na Tanganyika iko pale, ndiyo mnakaa na Zanzibar, kichwa chake ni Rais wa Zanzibar na hii Tanganyika ambayo imejipeleka kwenye Serikali ya Muungano, kichwa chake kiko pale ambacho ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, hivyo ni lazima, ye ye anasema hiyo isiwepo kabisa. Sasa hii ni demokrasia ya wapi hii? Kwa hiyo, siunganiani naye kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, anaposema Rais wa Jamhuri ya Muungano amepewa madaraka makubwa ya kuteua Tume, sasa hii Tume ye ye anataka iteuliwe na nani? Nani ambaye tutampa kazi ya kuteua labda tuiambie CHADEMA iteue Tume, wana uwezo gani, wana Wabunge wa ngapi humu ndani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu Rais ambaye amewekwa pale kwa Katiba sahihi ya Jamhuri ya Muungano ambayo iko sasa, ye ye ndiye mkuu wa nchi, ye ye ndiye anateua Tume, wewe unataka Tume iteuliwe na nani? Labda tukamchukue Man Park wao anayepigana yule kule, labda Bruce lee maana *symbol* yetu ya kuteua mambo kitaifa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa unasema huyu asiwepo na haya yanatoka mdomoni kwa msomi Tundu. (*Makof!Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Lissu.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mwalimu kuna siku alisema, mtoto akichezea moto aungue palepale, akichezea wembe ajikate palepale. Sasa juzi mimi nimeona watu wanachezea moto, kuna kitu kinaitwa Jukwaa la Katiba, yule bwana ni hatari kuliko UKIMWI, yule aliyekuwa anaongoza ule mjadala ni hatari jina lake sijui nani...

MBUNGE FULANI: Deus.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Jina lake Deus, kwanza jina lake halitakiwa litajwe kwa sababu sisi katika dini yetu Deo ni Mungu. Yule bwana ni hatari, anasema hivi, anawangoja Wabunge waupitishe Muswada huu kwa Mara ya Pili halafu anaipa Bunge, anaipa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, anawapa Polisi, anawapa Jeshi la Wananchi, anawapa Magereza,

anawapa Mgambo, siku thelathini halafu maandamano atakayoyafanya hapo siyo CCM, siyo Rais wao, siyo Magereza, siyo Jeshi ambalo wanaweza kuzuia maandamano hayo. Kwa hiyo, sasa sisi tuko kwenye mjadala huu kwa kwenda Mara ya Pili na itaenda Mara ya Tatu maana yake tayari kuanzia leo alishatupa muda wa siku thelathini. Sasa ameshachezea moto, naomba Waziri Mkuu kama uko hapa, Waziri wa Mambo ya Ndani kama yupo hapa, usikubali kuchezewa na mtu kama yule, wimbo mbaya haimbiwi mtoto, ukiachia wimbo huu, mkakaa kimya, watafanya mambo ambayo nchi hii itakuja kushangaa. Yule bwana apewe mkong'oto kwelikweli, pale atakapoanza tu ni mkong'oto wa hali ya juu hakuna kusubiri tena. Kwa sababu hii hapa ni maoni au ni matakwa ya nchi na watu wengi walifiki CCM itakataa, lakini Rais amesema twende huko tutakapoingia miaka hamsini basi tuwe na Katiba hiyo Mpya. Sasa wakati anawa-*preamble*, hao jamaa wanatafuta mbinu nydingine ya kudhoofisha suala hili, sasa naomba Serikali msikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali msikubali, wakiandamana kutafuta mkate waandamane, wakiandamana kutafuta maji waandamane, wakiandamana kuhusu Katiba hii mkong'oto, mkiachia hapo tumekwisha maana hata vurugu za duniani zinaanza hivyohivyo. Jambo jema linageuzwa kuwa jambo baya na baadaye pale inakuwa majuto ni mjukuu, hatukubali nchi yetu tujute kwa watu kama wale. Hatuwezi kujuta kwa matakwa ya Tundu Lissu, hatuwezi kujuta kwa matakwa hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wametumwa na mimi namshukuru sana Rais, Serikali ya Jamhuri ya Muungano hata walipokataa kwamba ndoa za jisla mbili zisiwepo lakini akina Tundu Lissu hawa ukiwaangalia, Chama chao ndiyo Chama cha yule wa ndoa, Cameron yule, kwa hiyo wangechukua madaraka maana yake hapa ndani watu tuko tu (*Hapa Mheshimiwa Mbunge allonyesha ishara ya vidole*). (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali kukataa mmetufunika nguo, sasa hawa ndiyo wanakotaka kutupeleka, kama walishindwa kipindi hicho cha U-Cameron basi wasiendelee kutuvuruga katika hii Katiba, Katiba iende kama ilivyopangwa na mimi nasema hivi mtoto akillilia wembe mpe umkate, sasa hakuna kusubiri tena, mimi nasikitika kweli ikiwa wale watu wanafanya maandamano na sisi tunawaangalia eti hiyo ndiyo demokrasia, hiyo siyo demokrasia huo ni uchawi, huo ni uuaji na mchawi anatakiwa auwawe ye ye kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo tu, naunga mkono Muswada huu mia kwa mia na hawa akina Tundu Lissu waendelee kukaa nje na bahati yao hamjaniteua mimi kuwa Mwenyekiti, mngeniteua mimi hata hiyo posho hawapati, lakini ndiyo demokrasia tena, wanaingia asubuhi kutumia posho ...

MBUNGE FULANI: Wanasantini.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Halafu wanasantini wanaenda kulala, nchi nzuri hii bwana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu sana katika mustakabali wa Taifa letu hususan tunakoelekeea kwenye kusheherekeea miaka hamsini ya uhuru wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposikia Muswada huu umeingia kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ajili ya Kusomwa Mara ya Pili, binafsi nilifurahi sana. Nilifurahi kwa sababu moja kubwa, nikiwa kama Mbunge wa Vijana niliona huu ndiyo wakati muafaka kwa vijana wenzangu kupata chombo watakachoweka mawazo yao na kilio chao kikubwa kwamba Katiba iliyoko sasa imewasahau vijana na huu ndiyo wakati muafaka wa vijana kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao ili yale malalamiko yao yote yaliyokuwepo yaishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya vijana wenzangu Tanzania wakiwepo wa Mkoa wa Mara, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania na vijana wenzangu, naomba mnisikilize kwa makini, kati ya watu waliokuwa na mchecheto wa Katiba mpya ni wenzetu waliotoka nje, sasa sijui walikuwa wana-beep au walikuwa na wana dhamira ya kweli au ya uwongo, lakini hapa *the way walivyoonyesha wameshindwa kutembea kwenye maneno yao.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuhoji kuna nini? Je, walikuwa wanataka kuhodhi mjadala huu wa Katiba Mpya iwe *agenda ya Chama?* Au walikuwa wanataka kuleta *interest* za watu ambao wanawafadhili na kuwapa hela nydingi, wanaowatuma kubomoa na kuharibu amani na utulivu wa Taifa letu, vimekwama kwa hiyo hawana *agenda ya Katiba.* Wangkuwa na *agenda ya Katiba Mpya* huu ndiyo wakati wa kuja kubadilisha kilichokosewa kwenye Muswada huu ili tuweze kupata chombo cha uhakika kitakachofanya kazi kwa maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata somo nzuri sana siku ya semina ya Professa Kabudi na mimi leo hii nawaambia mbali na umri wangu mdogo nimeamua kuwa na maono nisiwe na ndoto. Mwenye maono, mwenye nia njema na Taifa hili na Watanzania, lazima ataunga mkono Muswada huu lakini wenge ndoto za kufikirika ambazo hazitambui mfumo uliopo kwa mujibu wa Katiba na waliojaa ubinasi lazima watapinga Muswada huu kwa *interest* za chama chao na kupata *agenda za kisiasa.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wakati wa Watanzania kuangalia pumba ziko wapi na mchele uko wapi, lakini naamini katika neno moja tu sauti ya wengi ni sauti ya Mungu, humu ndani tuko zaidi ya 300 waliokuwa nje ni 47, hii ni sauti ya Mungu kwa niaba ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye Muswada, nikianza na uundwaji wa Tume ambao wenzetu wameulalamikia sana, kwa nini Rais anaunda Tume. Rais ana mamlaka haya kupitia Katiba iliyopo, mchakato huu bado haujahalalisha Katiba hii kufa na Rais ana mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 33, 34 ya Katiba tuliyonayo sasa na hatuna chombo kingine ambacho kitatupeleka huko tunakokwenda zaidi ya Katiba tuliyonayo sasa.

(*Hapa alionyesha Katiba*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Hii hapa, ambayo wote tumeitumia kuapa humu ndani, hatuna chombo kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii *trend* ambayo inaendelea kujengwa na watu waliojaa ubinasi, ni muda gani ambapo wanamtofautisha Rais wa nchi hii na Chama chake, anapofanya mazuri ambayo yana manufaa na nchi huyo hafai. Haya mambo lazima tuyangale kwa kina. Rais huyuhuyu ambaye tunamsikia leo hii wanasema yuko hapa kwa ajili ya maslahi ya Chama cha Mapinduzi, ndiye Rais huyuhuyu ambaye anawachangia kwenye harambee zao bila kujali hayo Majimbo ni ya *opposition* au ya Chama Tawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha bajeti hapa, tumeona kuna mabilioni ya fedha yameenda kwenye Majimbo yao, hapo hapakuwa na uitikadi. Kama aliweza kufanya hayo kama Mkuu wa Nchi leo hii ashindwe kuteua Tume ambapo Muswada huu umemwekeea vigezo, tutakuwa hatutendei haki *status* ya Rais wa nchi yetu. Wananchi walishaamua, kila Chama kilienda kutafuta nafasi hiyo, aliyepeata ni yeze, tuache nongwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikubali Watanzania kupotoshwa kwa ajili ya watu kufanikisha malengo yao ya kisiasa na hapa ndipo naona maneno yale waliyokuwa wakiyasema kwenye jukwaa, Tanzania iwe kama Libya, ndiyo wanachotaka kukifanya na wamekosa sababu wanataka kutafuta njia hii ya Katiba Mpya ambayo nayo wamekosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kuwaunga mkono kwenye maandamano kama Serikali ingekataa kuleta Muswada huu kwa sababu naamini vijana wenzangu wangekosa fursa, lakini wameleta, tunataka tuandike historia ya nchi yetu kwa kuwa na Katiba itakayojuamuisha makundi ya watu wote Tanzania, wanagoma 47? Zaidi ya wengi waliokuja hapa wamekuja kwa ajili ya Watanzania, nawashangaa waliotoka eti wanagoma kwa kisingizio cha wananchi

hawakushirikishwa, sisi tuko kwa niaba ya wananchi na mimi nilisikitika sana kijana mwenzangu Machali alipoi-*quote* Ibara ya nane ya Katiba na kusema kwamba imekiukwa, wakati tumetoka kwenye uchaguzi na tumeletwa kwa Ibara hiyohiyo, lakini nimeona hajui kazi yake kwa kusema hatuna *mandate* ya kutunga sheria, tunayo *mandate* hiyo kwa Ibara ya Katiba na kwa mamlaka tuliyopewa na wananchi. Kwa hiyo, lazima kama Wabunge tusome, tujue kazi zetu ni zipi. Kazi ya wananchi ni hiyo inayokuja baada ya Muswada huu kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia kifungu cha 24(3) katika Katiba hii. Kifungu hicho kinataka maamuzi ya kupitisha Rasimu ya Katiba itumike theluthi mbili upande mmoja wa Muungano na theluthi nyingine upande mwingine wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikubaliani nalo kwa sababu moja kubwa katika Muswada huu tayari tumesema watakapitisha Rasimu hiyo ni Bunge Maalum na huu Muswada umeshawapa mamlaka ya kujiwekea utaratibu wao wa kuendesha Bunge Maalum, si sahihi tuanze sasa kuwawekea masharti ya kuendesha Bunge Maalum wakati tayari kwa mujibu wa Muswada huu wameshapewa mamlaka ya kujitungia utaratibu wao. Hata hili tunapaswa tullachie Bunge Maalum wao ndiyo wataweka utaratibu watakaotumia kupitisha Rasimu hiyo kabla hawajaenda kwenye kura ya maoni kuamuliwa na wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Muswada huu kuna kipengele ambacho hakijafafanua pindi upande mmoja wa Muungano baada ya kupiga kura ya maoni watakaposhindwa kufikisha asilimia 50 na upande mwingine wa Muungano wamefikisha. Je, utaratibu gani utakaotumika, ni kurudia kwa pande zote au watakaorudia ni ule upande ambao umeshindwa kufikisha ile asilimia 50? Kwa hiyo, naamini Serikali itatoa majibu ya kutosha katika kipengele hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kuusoma Muswada huu haujaeleza wazi ingawa unaweza tu uka-*assume* hivyo kwamba kama hiyo rasimu ikikataliwa kwenye kura za maoni, je, itakayoendelea kufanya kazi ni hii Katiba iliyopo sasa au lah! Sasa hicho pia ili kuondoa *contradiction*, ni vyema Muswada huu ueleze wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namalizia kwa kusema sitokubali kupata umaarufu wa kisiasa kwa kuwaongopea Watanzania katika umri huu mdogo nilionao, lakini niko radhi kuhukumiwa kwa kuwapigania Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. (*Makofî*)

MHE. BONIFACE G. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Lakini kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, naomba nichukue nafasi hii kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja iliyopo mbele yetu, ni Muswada unaoweka utaratibu wa namna ambavyo tutakwenda katika azma ya Serikali na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili tuweze kutengeneza Katiba Mpya. Napenda sana nizungumzile Muswada huu una nini ndani yake, kwa sababu mwananchi aliyeo nje na yanayotokea humu ndani na kilichoko humu ndani ya Muswada wenywewe, kinachozungumzwa na dhamira yake ni kitu tofauti na kile kinachopelekwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa kifupi tu nieleze kwamba, katika Muswada huu kuna vitu vitatu vikubwa kwa dhamira ya kuweka mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya. Kwa hiyo, kwanza Muswada huu unaweza tu mfumo wa namna ya kwenda kutunga Katiba Mpya na wala hii siyo Katiba. Sasa hiki tukiweke vizuri kwa sababu huko nje watu wanaambiwa hiyo ndiyo Katiba, wanatunga Katiba, hapana! Sisi hatutungi Katiba, hapa tunaweka tu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna nini katika Muswada huu? Katika Muswada huu kwanza kabisa kuna *Commission Tume'* ambayo muundo na kazi yake ni kwamba, itakusanya

maoni kwa kupita kwa wananchi wote katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Itapita kukusanya maoni kwa wananchi wote mtaa kwa mtaa, kijiji kwa kijiji, kata kwa kata, wilaya kwa wilaya, ili kupata mawazo ya Watanzania juu ya Katiba wanayoitaka. Hii ndiyo kazi ya Tume hiyo na ndiyo kitu cha kwanza kinachosemwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa Tume hiyo ni kwamba, itateuliwa na Mkuu wa Nchi, kwa kuzingatia watu wenye uzoefu katika masuala ya Katiba na wenye sifa na uadilifu mkubwa katika Utumishi wa Umma na wa kijamii. Kwa hivyo, utaona kwamba Tume hiyo itakuwa ni Tume ambayo dhamira yake ni kukusanya maoni kutoka kwa Watanzania kila kona ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili kinachosemwa katika Muswada huu ni muundo wa Bunge hilo la kutunga Katiba Mpya. Muswada huu unasema muundo wa Bunge hilo utakuwa ni Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Bunge hili) na Wabunge wa Baraza la Wawakilishi, kutoka Zanzibar na Wabunge wengine mia moja na kumi na sita (116) watakaoteuliwa kulingana na sifa walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Wabunge watatoka wapi? Wabunge hawa wanaotajwa kuongezwa katika idadi ya Wabunge wa Baraza la Wawakilishi na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawa mia moja na kumi na sita (116) watatoka katika makundi yafuatayo; wawakilishi wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Kijamii (*NGOs*), Madhehebu au Mashirika ya Dini, Makundi Maalum katika jamii, Walemaru, Wataalam kutoka kwenye Vyuo Vkuu vyetu, humo ndimo watapatikana mia moja na kumi na sita (116) na hivyo kutengeneza sasa idadi ya Bunge litakaloitwa Bunge la Katiba. Baada ya Bunge hilo ambalo litapokea sasa taarifa ile ya Tume ambayo italetwa pale ili iweze kuwa kama ndiyo *database* ya yale yote waliyoyakusanya, Bunge lile litazingatia hayo ili liweze kwenda kwenye kutunga sasa Katiba Mpya, ambayo itakuwa inaashiria maoni ya Watanzania wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge hilo kutunga huo Muswada wa Katiba ambao bado kwa wakati huo utakuwa unaitwa Muswada, Watanzania wote wataalikwa kwa ajili ya kwenda kupiga kura ya maoni. Nchi nzima watapiga kura ya maoni ya kusema tunaitaka Katiba hiyo au hatuitaki Katiba hiyo. Mfumo wa kupiga kura, ndiyo ule uliopendekezwa, unaofaa na ambaao ndio tuliotumia katika Uchaguzi Mkuu na umekuwa ukifanyika na Tume ya Uchaguzi ndiyo itakayosimamia kura hizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niyaseme haya ili Watanzania wajue, ili wenzetu wanaopinga, wanaotoka nje na wenyewe wasije wakaonekana kwamba pengine wanaonewa au sisi tulipo, tunaouna mkono jambo hili, tunaunga mkono tu kwa sababu hatujui, si kweli! Tunajua kinachokwenda kutokea na ni kwa maslahi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushirikishwaji wa wananchi upo katika hatua mbili; upo katika hatua ya kukusanya maoni kutoka kwao, lakini upo kwenye hatua ya kuja kupiga kura ya maoni ambayo ndiyo inaitwa *referendum*. Hapo wananchi watakuwa wameshirikishwa katika hatua zote na ndipo itakapokubaliwa hiyo Katiba Mpya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme inauma, inashangaza, inasikitisha. Nilijaribu kupitia yaliyosemwa na mapendeleko ya Kambi ya Upinzani, kilichosemwa, humu katika mapendeleko yote haya, kwanza *spirit* ya hotuba ya Kambi ya Upinzani, haitaki kutambua ukuu na uwezo alionao Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano iliyopo. Haitambui vyombo vingine vyote vya kidemokrasia katika nchi yetu, haitambui! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikaijuliza msingi wa hoja hii unatoka wapi? Nikakumbuka aah, ni pale waliposema hawamtambui hata Rais aliyechanguliwa. Kwa hiyo, tusije tukaingia kwenye *bandwagon*, tukajikuta tunaingia katika kutekeleza wazo la watu la kutoka huko nyuma. Wao walisema hawamtambui Rais toka wakati alipokuwa akiapishwa na hata alipokuja hapa Bungeni walitoka nje. Sasa leo unafikiri watamtambua kwa kipi! Hawana watakachowenza kumtambua. Kwa hiyo, wako katika mpango mzima wa kutekeleza azma yao hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyoko katika hii Kambi ya Upinzani, naomba kabisa kwa idhini ya Spika, kwa sababu hii *is a public document*, hebu Watanzania wasome, wasome mapendekezo haya. Mapendekezo haya yanaua *the whole legal system* ya nchi. Ukikubaliana na mapendekezo haya maana yake hauna nchi, hauna mamlaka katika nchi. Maana yake nchi hii ni kama inaanza *from zero!* Tanzania haianzi *from zero*. Tumethubutu, tumeweza na tunasonga mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haianzi na moja, Tanzania hajawahi kusimama katika kwenda mbele. Tumepata fursa hii adimu, ambayo tumepata kwa kibali cha Mkuu wa Nchi, ameridhia baada ya kuona kweli katika kuadhimisha miaka hamsini (50) ya uhuru, ipo haja ya kupitia upya nyumba yetu. Wapo watu wanalia kwamba, sijui madini yetu hayatunfaishi, wapo watu wanalia unajua ardhi yetu namna tunavyoimiliki lazima tuangalie upya, yapo mambo mengi Watanzania wanayalamikia, sasa mmeletewa agenda Watanzania mseme mnachokitaka katika nchi yenu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mwengine, sijui, unajua pengine niseme tu, pengine tunaweza tukawa tunakwenda na agenda sasa, matarajio ya agenda ya wenzetu yanaonekana hayajawekwa vizuri kwa sababu wao wanadhani Katiba ndiyo itakayowaingiza Ikulu, siyo kweli! Kitakachokuingiza Ikulu ni kujenga mahusiano imara, *consistent* kati ya wewe unayetaka madaraka ya kisiasa na jamii. Katika msingi huu hawafanyi hivyo, kwa sababu badala ya kuwawakilisha wananchi kinachotokea hapa ni kituko na sarakasi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanadai kwamba utaratibu wa Muswada huu haukuatuwa. Miswada yote, chombo kikubwa cha kutunga sheria ni Bunge. Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kutunga sheria na Katiba inasema hivyo. Sasa unaposema kwamba, Muswada huu Usomwe Mara ya Kwanza au ya Pili, hivi ina tija gani? Nilikuwa najaribu *ku-reason out*, hivi kweli unaposema Mara ya Kwanza na ya Pili, kwa tija ipi! Kimsingi huna chochote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada Ukigomwa Mara ya Kwanza, ukawekwa kwenye Kamati hauna *reverse*, hauwezi kurudi nyuma. Ndiyo maana Kamati ya Pindi Chana ndiyo ilioendelea kukaa na Muswada huo na kuushughulikia na hata Serikali walikuwa wanahudhurishwa kwenye Kamati ya Pindi Chana. Pindi Chana hakwenda Serikalini na Wajumbe wake wa Kamati ya Katiba na Sheria. Aliendelea kuwa-*summon* Serikali waje wafanye mabadiliko, wameyakubali, umekuja Muswada mzuri mpya uliozingatia haya niliyoyasema awali, leo wenzetu wanasema hapana! Wakati haohao, Tundu Lissu yuko kwenye Kamati hiyo, wote walio-*walk out*, karibu robo tatu wako kwenye Kamati hiyo, huko kote wameshindwa kuweka mawazo yao, waje ghafla bini vuu hapa wanasema Muswada haufai urudi Ukasomwe Mara ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unasomwa Mara ya Kwanza ili kifanyike nini! Spika, anaposema Mara ya Kwanza anamrudishia nani huo Muswada? Muswada umeshamaliza hizo hatua, Wajumbe wa Kamati wametoa mapendekezo na maoni yao, Serikali imezingatia, yamekuja Bungeni leo tunaendelea na mjadala, fursa ya kutunga sheria sasa inaanza tunapoanza kujadili na baadaye *schedule of amendment*, ndiyo tunatunga sheria, wenzetu wanatoka nje. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Watanzania tunadanganywa. Nawaambieni Watanzania msje mkadhani kwamba, idadi yetu ya Wabunge wa CCM tunawaonea Wabunge wa Upinzani, si kweli, wana lao jambo. Wana lao jambo na pengine dhamira yao ni ovu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona wenzetu wa Chama cha CUF wana- *support!* *TLP* mbona wana- *support!* *NCCR* mbona wana- *support!* Hapa ndiyo tunatunga sheria, haya maoni yote haya yangeletwa hapa tuyajadili, unasema tutoke turudishe mwanzo. Maana yake wamehisi kwamba, wamekosa *ownership*. Wao wanachotaka ni kunyang'anya umiliki wa hoja iliyopo mbele iwe yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine niwaoneshe ukurasa wa hotuba hiyo, hakuna ukurasa, Profesa Shivji, kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala alitoa mapendekezo ya Ibara ya 20(2) ya Muswada kwamba, kama itapitishwa CCM itakuwa na wajumbe kati ya 350 – 400 katika Bunge la Katiba ambalo lina Wajumbe 545. Sasa uwakilishi katika kutunga sheria ni uwakilishi wa vyombo

vilivyopo. Nchi hii haijapinduliwa, haijaondolewa mamlaka yake, haijaondolewa viongozi wake. Hivi kama huliamini Bunge hili ambalo limechaguliwa na Watanzania, utaamini chombo kipi tena? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bunge hili ndilo ambalo lililosema Wabunge wa CCM tuko mia mbili na kitu, Wabunge wa CHADEMA wako Arobaini na Saba (47), wa CUF wako wangapi! Sasa uwiano huo ndiyo ungewaeleza wao kwamba, walipaswa wasubiri wakue, wakomae, tuje tulingane ndipo waamue mambo haya makubwa. Sasa waliyataka, tumesema, ndiyo wanageuka nyuma wanatafuta agenda ya kisiasa, wawavuruge Watanzania, waache kufanya kazi, tuache kwenda mbele, sisi tunasema tutakwenda mbele na Watanzania mtutendee haki katika kutusikiliza wote. Tutendeeni haki, mnawasikiliza zaidi wenzetu kuliko sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na hawa wanaharakati wajue wanaishi kwenye nchi iliyojengwa katika misingi mizuri ya amani ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi na mwanzo wa uwepo wa Vyama vya Siasa Tanzania ni kwa ridhaa ya Chama cha Mapinduzi. Kama wao walidhani kuna *shortcut* ya kwenda huko basi waache demokrasia, waamue kufuata hiyo njia nyingine wanayoitaka, lakini kwa msingi huu, Watanzania msidanganywe. Hakika ninawaambieni tutakuja kujuta, yalianza hivihivi, Rwanda na ikatokea balaa. Mimi nasema Serikali yetu muwe ***bold***, simamieni utawala wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ENG. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA: Kuhusu utaratibu, kuhusu utaratibu, kuhusu utaratibu!

MWENYEKITI: Naam.

MHE. ENG. MOHAMMED JUMA HABIB MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge aliyemaliza kuzungumza sasa hivi, ametumia neno Wabunge wa Upinzani. Kwa mujibu wa Kanuni zako, Kanuni ya 13 na 14, Upinzani maana yake na *CUF* yumo, *TLP* yumo, *NCCR* yumo na *UDP* yumo. Ningombwa arekebishe aseme Wabunge wa CHADEMA. (*Makofi*)

MHE. BONIFACE G. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nirekebishe kwa kusema kwamba, ni Wabunge wa CHADEMA na siyo Wabunge wa Upinzani. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Simbachawene kwa kukubali kurekebisha.

Waheshimiwa Wabunge, wakati natangaza uwepo wa Balozi wa Sweden katika Bunge letu alikuwa hajaingia. Naomba tutambue uwepo wa Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mheshimiwa *Lennarth. You are welcome.* (*Makofi*)

Pia naomba mtambue uwepo wa ndugu Mark ambaye ni Mwambata wa Ubalozi wa Sweden Tanzania. *You are welcome.* (*Makofi*)

Naomba tuendelee. Sasa naomba kumwita Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, lakini pia Mheshimiwa Augustino Masele na Mheshimiwa Selemani Jafo wajiandae.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwani toka jana sjapata usingizi, ulaji wangu hauridhishi, kutokana na maelezo yaliyojitekeza hapa Bungeni. Kwanza, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tuko katika mchakato tu kwenda katika safari yetu kwa ajili ya kupata Katiba, lakini muda hasa haujafika. Wazanzibari walikuwa na kilio hiki kikubwa sana, hivi sasa muda unaendelea na utafika. Hususan, pongezi hizi zaidi nazipeleka kwa ndugu yangu

huko Dungabweni, ndugu Mavune ambaye najua mara nyingi suala hili analiulizia, namwambia astahimili, muda wake utafika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zenyehu uhuru, demokrasia, mimi nasema Tanzania ni pekee lakini jambo lolote lina kikomo chake, uhuru unafika mwisho wake, demokrasia ina lengo lake vilevile, kama utazidisha, basi bila shaka utaleta vurugu. Hivi sasa kutokana na hali inavyokwenda, huko ndiko tunakokwenda na ni hatari kwa nchi yetu katika safari hiyo ambayo Tanzania tuna kila sifa ya kwamba ni nchi yenye utulivu na ambayo wananchi wake wanapendana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukiona kuna mabadiliko, lazima ujiulize kuna nini, kulikoni! Lazima kutakuwa kuna sababu maalum. Hii inaonesha wazi kwamba mwanadamu huwezi ukaonesha kifua, isipokuwa kama kuna jambo unalitegemea nyuma. Hapa inadhihirisha wazi kwamba wenzetu CHADEMA wana mategemeo ya sehemu yoyote ambayo inawaongoza katika taratibu zao na mwenendo wao. Hii inadhihirisha wazi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kwa kweli masuala yaliyojitozea hayakuonesha kwamba ni mwenendo mzuri. Hali hii kwa kweli inadhihirisha wazi kwamba inaleta mfarakano. Mzungumzaji aliyechangia jana wa CHADEMA kuna sehemu napenda kumnuuu; "Mfumo wetu wa Kikatiba na wa kisiasa umejengwa juu ya nguzo kuu ya Urais ya Kifalme (*Imperial Residence*)"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa kweli tumeungana na baada ya kuungana Tanganyika imeshakuwa huru, Zanzibar vilevile imeshakuwa huru, tuliondoa ukoloni, huku Bara walipata kwa kura, sisi kule Zanzibar tulipata kwa Mapinduzi, kwa hivyo tukaungana. Sasa leo akisema "Kifalme" haya ni matusi. Lakini ukitaka kulifanya jambo lako ambalo unalifanya lazima utaje la mwenzako, kwa sababu lako wewe unalificha, lakini hebu tujulize walio ndani ya CHADEMA Viti Maalum kama havikwenda kwa ukoo kama inavyodhihirisha, kweli watu hawa leo kama wanachukua nchi si hatari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndivyo ilivyodhihirisha, tusifanye makosa Watanzania kwa kweli tumefanya makosa makubwa baadhi yetu na tujirekebishe. Tulishabikia sana kisiasa, lakini hatukuangalia tunaowapa wadhifa na madaraka ya Ubunge. Leo wako wapi? Hii ni mara ya pili, kama hawa kweli wanasiisa walioiva ilikuwa wajenge hoja ndani ya chombo hiki. Sasa leo mnasema mmetafuta wawakilishi wako wapi? Tusifanye makosa Watanzania, kosa hili tusirejee tena, kutenda kosa si kosa, kosa kurejea kosa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hawa waliokuwa ndio wakubwa kusema kwamba wana imani ya fedha za wananchi mbona asubuhi wanakuja wanatia saini hapa, huu ni unafiki. Sasa hawa kama kweli hawahudhurii basi na hapa asubuhi wasije kwa sababu bado Muswada huu unaendelea wanakuja kufanya nini na wamegoma kwa siku hizi zote. Halafu wanasema wana uchungu wa wananchi wanawahadaa wananchi hii ni hatari, hii ni hatari kabisa. Hii ni dhahiri kwamba kwa kweli wananchi mna haki ya kuangalia vizuri kabisa bado chaguzi zitaendelea na tutaziacha, lakini mtafute viongozi wanaofaa ili kuendesha Bunge hill. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja chama hiki pia kuangalia kama kweli usajili hasa kule Zanzibar kama kweli wametimia. Kuna haya na sisi kule tunasema mwisho Chumbe. Kuna haja ya kuangaliwa mimi nina mashaka ya usajili wao. Kwa hivyo kuna haja waliohusika kuangalia vizuri hasa kule Zanzibar kwa CHADEMA mimi sijasikia kule sauti ya CHADEMA nakuja kuisikilia hapa tu katika Bunge kwamba kuna CHADEMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu cha 20 napenda kukieleza. Katika kifungu cha 20 kuhusu kuundwa kwa Bunge la Katiba. Pale namba 2 ipo mpaka (e). Itakuwa vizuri sana kuweza kupata vigezo vinavyotumika katika kupatikana Wajumbe walioorodheshwa kuanzia moja mpaka tano, kwa nini nasema hivyo, ndiyo mifano tunalona hii kwa sababu tusijeletewa watu ambao hawastahili, kwa kuwatumi lazima pawe na taratibu maalum ambapo tunajua watu hawa wana vigezo maalum kwa sababu unaweza kusema kwamba huyu kijana fulani lakini ana matatizo yake au tunasema Sheikh au Padri pengine ana tatizo lake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yote haya inabidi yaangaliwe. Tukifanya hivyo nahisi tutafika mahali pazuri, tuiseme kwamba labda tunachukua tu kwamba huyu anastahili kwa sababu ameitwa Sheikh au ameitwa Padri lazima tuangalie vigezo vyote vile vitano vikiwa kwa vijana kwa hali zote tuziangalle kwamba hizi kweli zinaridhia katika vyama nya siasa vilivyosajiliwa ndio vyama vyenyewe ndio kama hivyo, tunaona hali yenyewe kwa hiyo haya yote inabidi tuyajue. (*Makofii*)

Lakini vilevile kuhusu Rais, mara nyingi alisema kwamba pale Rais, Wanasheria wale, lakini nahisi lazima pawe na kipengele kwamba wakati Wanasheria pale panapostahili kwa kweli anastahili Rais wa kuweza kuwa na Wanasheria. Kila tunapokwenda taaluma inazidi wakati taaluma inazidi na mambo yanazidi zaidi kuwa makubwa.

Kwa hivyo wakati mwininge tunaweza kupata vijana wa kileo, tunaweza kupata Rais ambaye mwendawazimu, haeleweki. Sasa kama hana *guidance* kwa kweli itakuwa na matatizo. Kwa hivyo, naweza kusema kwamba Mwanasheria Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar licha kwamba tuseme hawapo lakini wakati wanahitajika basi nahisi ipo haja ili kuweza kumsaidia Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tena kwamba nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini ningependa kwa kweli hili tuliangalie vizuri sana. Wenzetu wameonyesha dhahiri kwamba hawataki Muungano na umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Ninaye Mzee wangu, Mzee Juma wa Juma tulikuwa tunakwenda shule sisi tunasoma.

(Hapa kengele illilia kuashirila kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa nakushukuru sana.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae na Mheshimiwa Mussa Kombo na Mheshimiwa *Engineer Hamad Masauni wajiandae*.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mjadala huu unaoendelea jioni ya leo kuhusu Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya nchi yetu wa mwaka 2011. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja kwa mia moja kwamba usomwe kwa mara ya pili katika Bunge lako Tukufu. Niwaombe tu Watanzania wenzangu ya kwamba watuelewe sisi wawakilishi wao tunayo nia njema kabisa ya kuhakikisha kwamba tunaifikia Katiba Mpya yenyе ubora unaostahili iliyoshirikisha Watanzania wote kulingana na historia ya Taifa letu. (*Makofii*)

Aidha, niwakumbushe tu Watanzania wenzangu ya kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye Mkuu wa nchi yetu na kwa namna yoyote ile hawezu kubewza katika kushirikishwa katika jambo kubwa kama hili linalolihusu Taifa letu na mustakabali wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa sababu Bunge la Jamhuri ya Muungano haliwezi kukamilika bila ya kuwepo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria yoyote inayoweza kuanzishwa na mchakato wowote unaoweza kuanzishwa ndani ya Bunge hili hauwezi ukakamilika asipo ridhia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu iliyopo hadi sasa. Inapotokea kwamba Taifa letu linaelekeea kufikisha umri wa miaka 50 tunayo sasa nafasi ya kuanza kutazama upya wapi tulipotoka, wapi tulipo na wapi tunakoelekea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni mazoea katika Taifa letu hili katika kila tukio lolote kubwa katika nchi hii kunakuwa na mabadiliko ya Katiba. Itakumbukwa mwaka 1920 tulipata

Tanganyika Order in Council ambayo ndiyo ilikuwa Katiba ya kwanza ya Tanganyika. Baada ya hapo mwaka 1961 tulipata Katiba ya Uhuru. Katiba hizi zote zilikuwa zinawahuisha Wakuu wa nchi kwa maana ya kwamba Gavana wa iliyokuwa Tanganyika aliruhusu mchakato wa Katiba Mpya ya Uhuru ya mwaka 1961. Mwaka 1962 vivyo hivyo Tanganyika ilipotaka kuwa Jamhuri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihusika. Kwa hiyo, mazoea haya yanatuonyesha tu wazi kwamba katika kila hatua Rais hatakaa aachwe pembedi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika suala zima linalohusu Muswada huu. Muswada huu umewahuisha Watanzania wote katika hatua zile za awali. Itakumbukwa kwamba Watanzania walikusanya katika vituo vya hapa Dodoma, Dar es Salaam pamoja na Zanzibar. Kwa wasomi inajulikana wazi kwamba unapofanya hata *research*. *Research* unafanya *sampling*, sasa unapofanya *sampling* sio kwamba unawa-*consult* watu wote kila mmoja kwa nafasi yake bali unaweza ukaenda unachukua kundi la aina fulani kutoka mahali fulani likawakilisha kitu kizima na kwa maana hiyo mawazo ya wananchi waliyoyatoa Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar yalitosha kabisa kuunda kwa ukamilifu Muswada huu tunaoujadili leo.

MWENYEKITI: Samahani Waheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize na tumpe nafasi mwenzetu tunaongea mno. Tumpe nafasi atoe mawazo yake na wengine wapate nafasi. Ahsanteni endelea Mheshimiwa. (*Makofii*)

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninayo imani ya kwamba Muswada huu utakapopita utatuongoza kwa ukamilifu kabisa kuweza kulifiki Bunge la Katiba linalokusudiwa kuundwa na Mheshimiwa Rais. Muswada wenye kama ulivyo unaonyesha wazi kwamba unazo sehemu sita. Sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi, sehemu ya pili, inahusu madhumuni kuna uundaji wa Tume, kuna sehemu inayohusu utaratibu wa utendaji kazi wa Tume yenye. Sehemu ya tano inahusu kuundwa kwa Bunge la Katiba na sehemu ya sita inahusu uhalalishaji wa Katiba inayopendekezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovoyote vile hapa hatujadili Katiba, tunachojadili ni utaratibu utakaotuwezesha kufika mahali ambapo sasa mjadala wa Katiba Mpya ndipo utakuja kuanza rasmi. Kwa maana hiyo Watanzania ambao hawajafikiwa bado nafasi yao inakuja wavute subira. Kwa hiyo, ndugu zangu Watanzania ninachowaombeni ni kwamba tuvute subira na masuala ya vurugu na uvunjifu wa amani yasipewe nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao watakaonekana kwamba kwa kweli wanakuwa wakorofii na wasiotii sheria basi sheria ichukue mkondo wake. Kwa sababu nchi yetu hii tumepata uhuru kwa amani na tunaendelea kuishi kama ndugu na mambo yetu mengi tumeyafanya kwa utaratibu wa kusikilizana na kuelewana, sasa iweje tushindwe kufikia muafaka katika suala muhimu kama hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu sasa linaflikia umri wa miaka 50, ni Taifa ambalo linaendelea mbele, linaendelea kukomaa na kwa maana hiyo matokeo ya kazi ambayo itafanya hapa itakuwa ni ukumbusho kwa vizazi vingi. Kwa maana hiyo ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania ambao mnaishi leo mnayo nafasi nzuri ya kuweza kuandika historia ya nchi hii na kuacha ukumbusho katika Taifa letu baada ya kufanya kazi nzuri ya kutoa maoni yenu kwa ukamilifu bila kuogopa, bila woga na bila kushawishiwa kwa namna yoyote ile. Nafasi hii ipo mara moja na haitakaa ijirudie tena na kwa maana hiyo hata kama ikija kurudia itarudia katika mtindo mwengine. (*Makofii*)

Ndugu zangu Watanzania niwaombe kwa mara nydingine tena kwamba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu pale atakapotakiwa kuunda Tume aiunde kwa ukamilifu na wale watakaokuwa wameshirikishwa katika utengenezaji wa hiyo Tume basi wafanye kazi kwa uaminifu bila chuki na wala bila husda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mapendekezo ya kwamba Mheshimiwa Rais apewe nafasi zaidi na kwa maana hiyo Wanasheria wa Serikali waondolewe katika nafasi hiyo ya ushauri katika uundaji wa Tume, lakini watatafutiwa utaratibu wa namna watakavyoweza kufanya kazi kwa sababu kwa mujibu wa Katiba tayari wanayo majukumu yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo napenda kusema tena kwa mara nyingine kwamba naunga mkono hoja Muswada huu uendelee mbele. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa, sasa namwita Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Hamad Masauni ajiandae, atafuatitiwa na Mheshimiwa Mussa Kombo na Mheshimiwa Stephen Wasira ajiandae. Naomba Mheshimiwa Hamad Masauni aanze kuzungumza. (*Makofii*)

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kunipatia fursa ya kuweza kutoa mchango wangu. Wenzangu wameanza kwa kushangaa, mimi naanza kwa kupigwa na butwaa. Napigwa na butwaa kwa sababu leo hii nimemsikia mmoja kati ya wachangiaji waliopita ambaye anasema wametumwa na Watanzania, wanawawakilisha Watanzania wa nchi hii. Kwa bahati nzuri sana mchangiaji huyo chama chake kina uwakilishi nafikiri wa Wabunge wasiozidi wawili kama sikosei. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa sisi ambaao tuna utitiri wa Wabunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambaao tumepewa ridhaa ya kuongoza Serikali zote mbili. Sijui tunatoa kauli gani? Naomba nichukue fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali mbili hizi kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kupokea maoni ya wananchi na hasa wananchi wa Zanzibar kutoka katika Muswada ambaao uliwasilishwa mwanzo na kuweza kuimarisha na kuja na Muswada huu ambaao kwa kweli niseme kwa ujumla naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utajikita katika maeneo mawili makuu. Eneo la kwanza litatokana na mchango wa hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo iliwasilishwa jana na Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini pia muda ukiruhusu nitajikita pia kutoa maoni kuhusu Muswada huu ambaao umewasilishwa mbele yetu. Nina masikitiko makubwa sana na wewe ni shahidi na Watanzania wote ni mashahidi kwa jinsi ambavyo hotuba ile iliyowasilishwa na Mheshimiwa Tundu Lissu jinsi ambavyo ilivyokuwa inalenga katika kuhtarisha mustakabali wa umoja na mshikamano na udugu wa wananchi wa Tanzania. Lakini hotuba ile ambayo imejaa kila aina ya chuki kwa Wazanzabar imelenga katika kupotosha lakini pia imewavunja hadhi Wazanzibar na sidhani kama ni busara kutokutumia fursa hii kuweza kutoa ufanuzi kuhusu yale ambayo yameelezwu kwenye hotuba hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba hiyo haitoshi mwasilishaji ambaye mwenyewe amejipambanua kwamba ametabaharika na kuboea katika fani ya sheria ndiye amekuwa msimamizi wa uvunjifu wa misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhoji mamlaka ambayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepewa kwa muhibu wa Katiba. Katika hili mengi yamezungumzwa, wapo waliosema kwamba Rais wa Tanzania ni *Constitution icon*, wapo waliosema ndiye Amir Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania na Kiongozi Mkuu kama *Head of State* na angweza kutumia Katiba hiyo hiyo inayompa uwezo kuweza kuupitisha mchakato huo katika njia ambayo angeona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo waliosema angweza kuunda *commission of inquiry* na mchakato huo ukapita. Lakini mchakato huo pia ungeweza kupita kwa utaratibu ambaao nchi nyingi zimeweza kuitisha. Tunaambiwa Watanzania ni mielongoni mwa nchi chache sana ambazo tumeamua kuitisha mchakato huu kwa kuititia kwanza katika kuunda Bunge la Katiba lakini pili kwenye kura ya maoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo yote inaonyesha ni dhamira na nia njema ya Serikali na ya Rais wetu. Nataka niseme jambo moja la msingi sana. Mheshimiwa Rais na Serikali yake inapaswa kuponbezwa katika jambo hili kwa kuamua kurudisha madaraka kwa wananchi kuititia sisi Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaao tumepewa mamlaka na wananchi hawa tuwawakilishi kuititia Muswada huu na kuweka vigezo vya Wajumbe ambaao ndiyo watakaoweza kuchaguliwa kulingana na vigezo vitakavyosimamiliwa na sisi na kuvipitisha, lakini pia na sisi wenyewe kuwa washiriki katika Bunge la Katiba. Ni jambo ambalo limeonyesha ukomavu wa demokrasia ya hali juu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu amelizungumza jana. Mheshimiwa Tundu Lissu amesikitishwa sana na amehoji uhalali wa Wazanzibar *ku-determine* mustakabali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Inasikitisha sana sijui alikuwa anataka nchi gani *i-determine* mustakabali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ni Uingereza ya David Cameron. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini kwa mujibu wa Katiba hii ambayo ndiyo tunaitumia imeitaja Tanzania Bara, imeitaja na Tanzania Zanzibar. Ukienda kwenye Ibara ya 151 kwenye tafsiri utaona nini maana ya Tanzania Bara na nini maana ya Zanzibar sina haja ya kuinukuu. Lakini Tanzania Bara imechukua nafasi ya iliyokuwa Jamhuri ya watu wa Tanganyika na Tanzania Zanzibar imechukua nafasi ya iliyokuwa Jamhauri ya Watu wa Zanzibar. Kwa hiyo, Katiba hii inatambua uwepo wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na hawa ndiyo wadau wakuu wa Muungano na hivyo basi ushiriki wao katika kuhakikisha kwamba ni Tanzania ya aina gani kwa mujibu wa Katiba hii ni jambo ambalo halina mjadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hajalishi kwa kiwango gani nchi hizi zinawakilishwa kwa maana ya idadi ya watu wala ukubwa wa maeneo. Lakini ndiyo maana Katiba hii hii ikawa imezungumzia umuhimu wa maamuzi yanayohusu Muungano likiwemo la Katiba kwamba maamuzi yake yatokane na theluthi mbili ya Wajumbe wote. Kwa hiyo, inatushangaza sana kuona mtaalam wa sheria anahoji ushiriki wa Zanzibar katika mustakabali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia hajaishia hapo, amehoji pia imani ya Tume za Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume ambayo ilimtangaza kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matusi makubwa sana si tu kwa Wabunge tulimo humu ndani bali pia kwa wananchi wote wa Tanzania, kwamba leo hii Bunge hili ambalo ndilo linapitisha Sheria ya Uchaguzi ikiwa yeye Mheshimiwa Tundu Lissu ni mmoja kati ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ana nafasi kubwa sana katika hilo na Katiba yetu linadhihakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Sheria hizi za Uchaguzi nazo zina vifungu vya makosa ukiwemo Muswada huu ambao unataka kupitishwa. Katika Ibara 19 imeanisha makosa na adhabu za wale ambao watakiuka taratibu za uendeshaji wa zoezi letu. Kwa hiyo, mimi niseme tu, kwa ujumla ninachokiona hapa ni chuki baina ya Mheshimiwa Tundu Lissu na Wazanzibar. Nasema chuki alizonazo Mheshimiwa Tundu Lissu na Wazanzibar ni kwa sababu zifuatazo, nasema hivyo kwa sababu naamini kabisa kwamba bado CHADEMA wana nafasi ya kupinga yale ambayo Msemaji wao wa Kambi amezungumza jana na wana nafasi ya kuwaomba radhi Wazanzibar. Kwa sababu hiki chama kwa mujibu wa Sheria zetu za Uchaguzi kinahitajika kiwe na uwakilishi wa wanachama wote pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sidhani kama Wazanzibar ambao ni wanachama wa CHADEMA watakuwa hawajaguswa na haya ambayo nimeyazungumza mimi, watakuwa hawajaguswa na dharau hizi, kwamba leo inafika, Mheshimiwa Tundu Lissu anahoji eti Wazanzibar wanabembelezwa kwa sababu ya kura zao za uchaguzi wa urais kipitia CCM na ndiyo maana inadhihirisha pengine kwa CHADEMA kura za Wazanzibar kumpata kiongozi ambaye atagombea urais au nafasi ya Kitaifa hazina maana yoyote. Sasa kama hakuna thamani ya kura ya Mzanzibar katika CHADEMA sielewi Wazanzibar wanatafuta nini katika chama hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasema kwamba bado CHADEMA wana nafasi kubwa kabisa ya kurekebisha makosa haya ambayo yamefanya na Msemaji wao wa Kambi ya Upinzani, matusi haya na dhihaka dhidi ya Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla. Kinyume cha hivyo ni ishara tu ya kuangamia kwa chama kwa sababu chama hiki hakiwezi kusimama bila kuwa na wanachama wa pande zote mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niligusie ni kwamba amezungumzia pia uhalali wa Tume hii utatokana na uwakilishi wa vyama viliviyopata usajili wa kudumu. Mimi nasema labda wafuatilie historia ya nchi nyngine jinsi ambavyo walipitia katika mchakato huu. Kenya ilipita katika mchakato kama huu na ilipata matatizo makubwa sana kwa sababu ya kuingiza utashi wa vyama vya siasa katika mchakato na ndiyo ilipelekea kusababisha vurugu kubwa na hatimaye

watu kufariki. Lakini uhalali huu wanaouzungumzia ni nani ambaye anatafsiri uhalali. Ni wananchi ama ni CHADEMA au hao wanaojiita wanaharakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri ni wananchi na wananchi wanawakilishwa na Wabunge kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge na Wawakilishi kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, tunapozungumzia uhalali mimi nafikiri umekuja kwa wakati muafaka ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge ambalo lina wawakilishi wa wananchi wote wa nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimalize kwa kutoa maoni katika Muswada huu. Naomba kwa haraka haraka niende katika Ibara ya 20 ambayo inaelezea...

(Hapa kengele ililia kuashirila kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kwanza kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge hili ambaye alisimamia Kamati yetu ya Katiba na Sheria mpaka tukafika hapa. (*Makofi*)

Naomba kutoa shukrani zangu kwa Mwenyekiti wangu wa Kamati hii kwa uongozi wake mzuri aliyetuongoza mpaka tukafikia hapa leo. Naomba kutoa shukrani zangu kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano wake aliotupa katika Kamati yetu. Naomba kuwashukuru pia Serikali ya Zanzibar kujua umuhimu wa Muswada huu na kuletwa Waziri wake wa Katiba na Sheria kusaidiana na Serikali ya Muungano. Namshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kuletwa hapa pia na Naibu Mwanasheria Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, bahati mbaya sana ililotoka watu wengi hawajalionia. Ni kweli tumetukanwa sana katika Bunge lakini pia tumetolewa kitaalam kuuchangia huu Muswada. Tumekuwa na mawazo ya CHADEMA, CHADEMA, CHADEMA.

Nawaomba Wabunge wenzangu watakaokuja kuchangia tutizame Muswada unatusaidia nini. Bunge hili Tukufu lenye nchi mbili, lakini zenyen kuheshimiana nchi moja kubwa, nchi moja ndogo matusi kama haya ambayo wengi wamezungumza nataka nisaidie yasitokee tena yakatuvunja urafiki wetu na udugu wetu.

Hiki kitabu nilichonacho kinaitwa "*The Book of the States*" cha Kimarekani, nataka kukupeni zile *States* za Kimarekani zilivyokuwa ukubwa wake na nyingine ndogo lakini zinaheshimiwa vilevile wana ma-senator wawili kila *state*. Kwa mfano sensa ya mwaka 1970 California na *population* ya 19 million people. Sasa hivi ina 25 million, Delaware population yake ilikuwa 548,104, Nevada ilikuwa na *population* ya 480,738, North Dakota, walikuwa na *population* ya 617,761, Alaska ilikuwa na *population* ya 302,173 hivi sasa ina 600,000. Ni *states* za Kimarekani ambao sie tunakaa hapa tukiteea na tunatetemeka na tunasema ni Taifa kubwa lakini wanaweka heshima kwa nchi zao zile ambazo zinahaki sawa na nchi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili ni *UN*. China ina over one billion, Tanzania ina milioni 40, lakini haki ni sawa katika Umoja wa Mataifa. Tuache hapo twende Seychelles wana 120,000 wana kiti pale Umoja wa Mataifa sawasawa na Tanzania yenye watu milioni 40 lakini haki sawa kwa wote. Ndiyo chama changu kikasema, ukiniuliza "Haki" nakwambia "Haki Sawa kwa Wote" kwa sababu tuheshimiane. (*Makofi*)

Sasa mtu kama Mbunge wa CHADEMA anaesema Jimbo lake la Uchaguzi la Ubungo lina wapigakura laki nne na nusu ni sawasawa na wapigakura wa Zanzibar. Mtu kama wa CHADEMA wakati wa Bunge la Bajeti anatoa kibri kuifanya Zanzibar si lolote, si chochote. Mara ya tatu katika Bunge hili. Sasa mimi maneno yangu ya mwisho kwa hapa ni kuwaambia tu angalieni uongozi wa CHADEMA wao wenywewe wakoje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalieni tuhuma walizonazo, angalieni chama safi kama cha wananchi (*CUF*), Mwenyekiti wake ni Profesa aliyesoma, ndio maana sasa yuko *UN*, Katibu Mkuu wake ni Maalim Seif Shariff Hamad aliyesoma, sasa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Haya, nyie Watanzania, wenge akili, wenge uwezo, CHADEMA, CHADEMA, CHADEMA hawa hawana kitu, nyamazeni, tutafute tujenge nchi. Nafikiri hilo la msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nzungumzie kifungu cha 20. Kifungu cha 20 katika Muswada wetu ni uundwaji wa Bunge Maalum la Katiba. Bahati nzuri sasa hivi Wabunge wote tulioomo ndani ya Bunge hili ni 353. Wabunge hawa ndio Wajumbe wote watakoakuwa wa hili Baraza Maalum la Katiba. Wenzetu wamekataa kuwa wao hawaitaki Katiba, wametoka nje. Wenzetu ni 48, wamesema hawawezi kuwa Wajumbe wa Bunge la Katiba. Naomba kukusaidieni, unapokuwa unakataa hii rasimu, chama chako kizima kinakataa na *kina-walk out*, wanayakataa maamuzi yatakayotokea ndani ya Bunge. Na maamuzi tutakayopitisha ni kwamba Wajumbe wa hili Bunge la Katiba ni Wabunge wote. Sasa bahati mbaya wenzetu wamekataa na wenzetu waliokataa ni 48. Tutafanya nini *replacement* yake? Tutakalolifanya ni kutoa *one part* ya 116 waliochukua Zanzibar 40, tukatoa pale tutapata 76. Sasa 76 tutaongeza tupate Wabunge wengine wapya 48 wawe 124 kama vile ambavyo inatakiwa. Nafikiri mmenielewa ninalolieleza hilo. Ni hoja ya msingi. Haiwezekani mwanangu anaposwa, lakini mkwe wangu anayeniposa anasema sitaki mimi kwenda kwa baba yake nikamlipe mahari. Hata haiwezekani! Nafikiri naeleweka vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, nasema tulikubaliana katika sehemu ya 3 kifungu namba 5, Uundwaji wa Tume. Serikali ilipendekeza wawe 30, lakini sisi kwa busara tuliyonayo, tukasema waanzie 20 mpaka 30. Sasa hii inagawika asilimia 50 kwa 50. Watu 15 ikiwa 30 wametoka Bara, 15 ikiwa 30 watatoka Zanzibar. Au 20, kati ya hao 10 Zanzibar, 10 Bara kuonyesha nguvu ya Muungano kwa pamoja kwamba tunashirikiana. Vilevile tulipokuwa tunaunda hii Kamati ambayo nimezungumzia sasa ililetu mgogoro kidogo, lakini tukapendekeza, Serikali ikakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wenzangu, napenda kuwaambia kama kulitokea wakati mgumu sana kwa Waziri wa Katiba na Sheria, basi ni wakati huu. Lakini yeze na watalaaam wake na viongozi wetu kutoka Zanzibar waliposhirikiana, tukapata kitu kama hiki. Nawaombeni sana wananchi wote msisikilize mambo ambayo hayana msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukishapitisha hii, la pili ni nini? Hawa watalaaam wetu hawa, Tume hii ya watu 30 itapanga programu ya nchi nzima. Sasa hapo ndipo utakapokuwa na uwezo; nataka Serikali tatu:- Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika na tuitizame itakayyokuwa hivi, nataka Serikali moja, tuungane hivi, ndio wakati wake. Rais apunguziwe hiki, Waziri asiwe na hiki, tutakuja tutakaa, tutasema hili mtu aliyelizumgumza ni mtu mwenye akili au hana akili, wakati huo. Lakini kwanza tuijishe ili watu waweze kujua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno yote niliyozungumza, naunga mkono hoja hii, wenzangu wa CCM wamesema mia kwa mia, mimi kwa sababu nilikuwa Mjumbe wa Kamati hii, elfu moja kwa elfu moja. (*Makof*)

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii kwa ajili ya kuweza kuchangia pia Muswada huu wa Marekebisho ya Katiba. Na naiomba Serikali iende nao mwendo wa *marathon*, kwamba tunataka Katiba Mpya ili ikifika mwaka 2014, tuwe na Katiba Mpya. Naomba Serikali iende mwendo wa kasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawakilisha akina mama wa Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro una Wilaya saba, niwaombe wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro na hususan wanawake wa Jimbo la Moshi Mjini, wanawake wa Jimbo la Rombo, wanawake wa Jimbo la Hai na wengine wote, lakini hao hasa natilia umakini kwamba wasidanganyike. Hapa, tunajaribu kutengeneza Tume ambayo ndio itasimamia mchakato mzima wa Katiba. Kwa hiyo, ninaomba wasipotoshwe. Hapa hatutengenezi Katiba, hatuchukui kura za maoni za wananchi kwa ajili ya Katiba, isipokuwa tunatengeneza Tume ambayo itasimamia mchakato wa Katiba. Kwa hiyo,

ndugu zangu, ninaomba sana sana, itakapokuwa tumemaliza kuunda Tume, Tume itakuja huko, kwa hiyo, wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kutoa maoni yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi akinamama, takwimu zinasema kwamba sasa hivi tunaelekea kwenye asilimia 51 na akina baba ni asilimia 49. Kwa hiyo, kwa uhakika sisi akinamama tunahitaji nafasi kubwa. Ile asilimia 50 tunayoiongea ni kweli tunahitaji kwa sababu na sisi tunaelekea kuwa wengi. Lakini asilimia hii kama walivosema wenzangu inawezekana kwa urahisi kama itakuwa imewekwa kwenye Katiba. Lakini pia nafasi za uongozi wakati mwingine zinakuwa ni za kubembeleza kwa viongozi wetu. Lakini kama tutapata muda wa kuchangia Katiba, wa kutoa maoni, basi inawezekana kabisa nafasi za akinamama zikawekwa bayana na akinamama wakapata nafasi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite kwenye Ibara ya 5 na 6 ambayo inaongelea kuhusu madaraka makubwa ambayo amepata Rais kwa ajili ya kuteua Tume.

Mheshimiwa Spika, naomba niwaambie wananchi wa Tanzania na hasa wale wenye *interest* na Katiba hii kwamba mchakato huu wa Muswada haufuti Katiba iliyopo. Katiba ya zamani inabakia pale pale, kwa hiyo, tukienda kwenye mchakato huu haimaanishi kwamba Katiba ya zamani inafutika.

Kwa hiyo, kwenye Ibara ya 33(1), Katiba inasema Rais ni Mkuu wa nchi, ni Mkuu wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu. Kwa madaraka hayo, kwa uhakika ana haki na wajibu wa kusimamia mchakato mzima wa Katiba. Kwa hiyo, manung'uniko yanayoletwa na wenzetu ni manung'uniko yanayopotosha wananchi na naomba wananchi myasikie haya kwamba Mheshimiwa Rais ana madaraka makubwa kwa Katiba iliyopo na hamna namna ambavyo tutamtenganisha na mchakato huu tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika kifungu cha 6(3) cha Muswada kimeeleza kabisa kwamba Rais ana maelekezo na ushauri kwamba namna gani anaweza kuteua Wajumbe wa Tume. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kifungu cha 9(2), hiki kimelalamikiwa kwamba Muswada unakataza mambo mengine kujadiliwa. Watalaam wanasesma hebu wasome *between the lines*. Ni kwamba kifungu hiki hakikatazi mtu kujadili jambo, lakini ni ukweli ulio wazi kwamba hatutaki mtu ajadili jambo aseme kwamba tuvunje Muungano, hiyo hatukubali. Hatukubali pia kwamba uwepo wetu wa Kitalfa, amani na utulivu, mtu ajadili kwamba anataka kuvuruga. Tunahitaji pia kama utajadili mambo haya, ujadili pia ukuzaji na uhifadhi wa haki za binadamu. Na tukumbuke pia uwakilishi mkubwa wanaopewa Zanzibar, tukumbuke kwamba Zanzibar ni *Sovereign State*, ni nchi kama nchi nyingine. Kwa hiyo, hakuna haja ya kulalamika kwamba Zanzibar inachukua uwakilishi mkubwa kwa sababu Zanzibar ni *Sovereign State*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba pia nitoe angalizo kwamba kwenye Sehemu ya 16(5)(a) yapo malalamiko ambapo nimekuwa naambiwa na marafiki zangu nije huko hasa akinamama, wakisema kwamba kwanza Tume itakavyokuwa inaenda kuchukua kura za maoni *ita-delegate powers* kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao ni wateule wa Rais. Lakini wanashahau kwamba huyu Mkuu wa Mkoo kama ataita m kutano, Mkuu wa Mkoo hana watu. Mkuu wa Mkoo hata akimtegemea Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya lazima aende mpaka kwenye vijiji amtumie Mwenyekiti wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji wale ndiyo wana watu. Na hao Wenyeviti wa Viji na Wenyeviti wa Vitongoji wamechaguliwa na watu, wapo ni wa vyama tofauti. (*Makof*)

Kwa hiyo, hakuna mantiki tukisema kwamba hawa ni wateule wa Rais kwa hiyo watachagua, wanasesma wale watu watakuoja kwenye kura za maoni watakuoja watu ambao wamechaguliwa, ni wa CCM. Siyo kweli! Na tukumbuke kule vijijini, watu wanachagua watu siyo kwa chama, mara nyingi wanachagua mtu. Kwa hiyo, hata kama kuna mtu wa chama kingine na wanachama waliopo pale ni wa Chama cha Mapinduzi, kama yule mtu ni mzuri, wanamchagua. Kwa hiyo, ndugu zangu naomba tuondoe hofu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa angalizo kwenye kipengele cha 29(2). Tumesema Tume italazimika na vyama vya siasa na vyama vya kijamii vinaweza kutoa elimu ya uraia na kuhamasisha upigaji wa kura za maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huu wa kuondoka Bungeni, ikawa hakuna uwakilishi na vyama hivi tukawapeleka wakaenda kuwahamasisha wananchi kwenye kura za maoni. Naomba hapa pawekwe angalizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, naomba tu niseme kwamba uzoefu unaonyesha kwamba nchi nyingine zote zinazofanya mchakato wa Katiba, Tume ikishafanya kazi, zoezi linaenda moja kwa moja kwa wananchi (*referendum*). Kwa hiyo, hakuna Bunge la Katiba. Kwa hiyo, sisi tuna haja ya kujivunia kwamba tunaenda hatua mbele zaidi kwa sababu tunafanya ushirikishwaji mwingi zaidi kwa kuanza na Tume halafu tunaenda Bunge la Katiba halafu tunaenda kwa wananchi (*referendum*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuweka historia ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Muswada huu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2011. Kwa umri wangu huu, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kusimama kwenye Bunge hili na mimi kutoa mchango wangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Sheria na Katiba wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuipongeza Kamati na wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia mpaka Muswada huu umewasilishwa kwenye Bunge hili kwa ajili ya majadiliano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuwafahamisha Watanzania kwamba wenzetu wa CHADEMA wamekubali kabisa Muswada huu uwasilishwe Bungeni kwa mara ya pili kwa kuwasilisha maoni yao. Kwa Kanuni waliyoutumia, Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2007, CHADEMA wametimiza matakwa ya Kanuni za Bunge kwa kuwasilisha maoni yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningewaelewa sana kama jana wasingewasilisha kabisa maoni yao. Kwa mujibu wa ripoti yao iliyowasilishwa na Msemaji wao, ripoti hii imewasilisha mapendekezo mbalimbali na mapendekezo hayo yanaashiria kabisa wao wamekubali kwa namna moja au nyingine tuendelee na hatua zingine kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie wanaharakati wote wanaotumia Jukwaa la Katiba, CHADEMA wamewaingiza mkenge. Katika taarifa yao waliyowasilisha humu, wameitoa mapendekezo mbalimbali na naomba ninukuu pendekezo moja tu ambalo wao walipendekeza utaratibu wa kidemokrasia zaidi wa uteuzi wa Tume. Kwa hiyo, wanapendekeza iwe Tume ya vyama. Sasa kama wao walikuwa wanasema tuanze, turudi kwenye hatua ya kwanza, mapendekezo haya walikuwa wanampa nani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba niwafahamishe Watanzania kwamba ni namna gani CHADEMA wameona kabisa Muswada huu mzuri, ukurasa wa 23 katika ripoti yao, nawanukuu: "Ni Muswada muhimu kuliko pengine Miswada yote ambayo Bunge la Kumi litapata fursa ya kujadili na kuipitisha. Ni Muswada wa kihistoria kwa vile tangu Uhuru wa Tanganyika miaka 50 iliyopita na tangu Muungano miaka karibu 48 iliyopita, Watanzania hatujawahi kupata fursa ya kujadili na kuamua mustakabali wa Taifa letu Kikatiba kwa utaratibu ambao unapendekezwa katika Muswada huu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno yao wenye kipengele cha 29(2). Tume kutoea kuundwa Katiba kwa utaratibu ambao unapendekezwa kwenye Muswada huu, naomba Watanzania wote waipitie ripoti yao ambayo ipo hata kwenye mitandao

mbalimbali, wasome mstari kwa mstari wataelewa tupo nao kwa pamoja ingawa humu ndani hawapo. Na kwa kuwa wamesusa sisi tunaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni mbalimbali na kupitia hilo Jukwaa la Katiba ambalo linakusanya tu watu mbalimbali, nimesikiliza Jumapili kupitia *ITV*. Nasikitishwa sana na upotoshwaji unaofanywa na Jukwaa hili la Katiba na naiomba Serikali kwa kuwa wao wame-beep, na tunasema mtu mzima hatishiwi nyau, kama walivyosema wenzangu, tusikubali kuhatarisha amani hii kwa kiini cha Jukwaa la Katiba. Kwanza, hatutambui ameliunda nani, limeundwa lini na kwa sheria gani ya kuundwa kwa Jukwaa hilo la Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukwaa la Katiba linawapotosha Watanzania kwa sasa na wengi wanaochangia pale, utaskia wanachangia vipengele ambavyo wanaviona vina upungufu kwenye Katiba yetu. Sisi hatujafika huko, tunaandaa utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia nashangaa na Wabunge wenzangu wameshangaa asubuhi ya leo, kwamba hivi kama wao walithubutu kusema ndani ya siku mia moja wanaweza, iweje leo sisi tumeanza mchakato huu wanaanza kuona kwamba haiwezekani? Nakumbuka Bunge la mwezi wa nne, wao kupitia kwa viongozi wao ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uongozi waliomba Muswada huu uwasilishwe kwa *certificate of urgency*, kwa nini leo unawasilishwa wanasema hapana, wana lao jambo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi naomba nichangie vipengele viwili tu si vizuri sana kwenye sheria, lakini nachangia kipengele cha uteuzi na mamlaka ya Rais Kifungu cha 5 na ninaomba nimnukuu kwa faida ya Watanzania wote kwa sababu semina tulioipata Wabunge kupitia Profesa Kabudi Palamagamba haikuoneshwa kwa Watanzania wote, lakini Profesa Kabudi alitupa uzoefu kwamba Tanzania hatuna matatizo na Tume zinazoundwa na Rais na leo asubuhi tumemskia Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy Mwalimu akitaja kifungu ambacho Marais wote wamekitumia kuunda Tume na Tume zile tumeona na sisi wengine tumeona kwenye taarifa mbalimbali mapendekezo walijotoa, hata mengine yalikuwa machungu kwa Serikali, kwa hiyo, hata kama walikuwa wanateuliwa na Rais lakini walikuwa na uhuru wa kupendekeza chochote walichokiona kinafaa, leo kwa nini tunaogopa Tume hii isiundwe na Rais ambaye mamlaka hiyo amepewa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni hofu ambayo wanajengewa Watanzania kwamba Tume inaundwa na Rais, itakuwa haipo huru, lakini Tume ile kazi yake ni kukusanya maoni, sisi tunatakiwa tulipe baraka Bunge hili lipitishe huu Muswada ili maoni yakusanywe na Tume, kazi yake ni kukusanya, haiongezi na wala haipunguzi, inakusanya, inaratibu, inaadidika vizuri na inawasilisha. Na hata kwenye Muswada huu Tume imetakiwa watakapowasilisha ripoti/rasimu waweke watalaan waliowaita na taarifa mbalimbali ambazo zitaonesha ni namna gani wamefanya kazi kwa uhuru. Na mwishowe Bunge Maalum litaitishwa na wao wenzetu waliotoka 48 ni Wajumbe wa Bunge hilo. (*Makofi*)

Sasa kama wana wasiiasi na kutokana na uhuru wa vyombo vyaya habari tutakuwa tunasikia kila kitu ambacho wananchi watakuwa wanatoa maoni yao na maoni yenye wtuayajua, vifungu ambavyo vina kasoro kwenye Katiba yetu tunavijua, tatizo ni nini sasa? Wana lao jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nichangie uwasilishwaji wa ripoti ya Tume kwa Rais na Rais wa Zanzibar, hapa mimi nashangaa huyu Rais wetu kwa mfano kwa mujibu wa Katiba yetu anamteua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, anakagua mahesabu, ripoti yake anaiwasilisha kwa Rais na Rais pia baadaye anampa Waziri wa Fedha anaiwasilisha humu Bungeni, na ripoti zote za huyu *CAG* ambaye anateuliwa na Rais hawa Vyama vyaya Upinzani hasa CHADEMA ndiyo wanaitegemea na ndiyo wimbo wao wa kila siku, nchi ina ufsadi wanategemea ripoti ya *CAG* ambaye anateuliwa na Rais na *CAG* anampelekea ripoti Rais, sasa tatizo ni nini katika Tume hii? Ndiyo maana tunasema hapa wana lao jambo siyo sawa sawa. Mimi kwa kipengele hiki sina wasiiasi ila ninachoshauri tu kwamba kwenye kifungu hiki cha 18 tumuwekee muda Rais atakaa na ripoti hiyo kwa muda gani ambapo atamuomba Mwenyekiti wa Tume aiwasilishe rasimu hiyo kwenye Bunge Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa mtazamo huu kwa sababu Rais huyu, kwa kuwa anawateua watu mbalimbali na Tume zinafanya kazi yake, na tumeshuhudia hakuna uchakachuaji wa Tume ambazo tumezunga zimeundwa kwa mujibu wa masuala mbalimbali ya Katiba ambayo yamejitokeza, lakini pia hata ukipitia ripoti ya CAG, kwa nini Mheshimiwa Rais ripoti ya CAG asiifanyie uchakachuaji ripoti ambayo inaiumbua Serikali mara kwa mara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nadhani waseme lingine kwa kuwa wameona kabisa sasa hivi hawana ajenda. Hawana ajenda ya maandamano, hawana ajenda ya mikutano ya hadhara na ninawaomba Watanzania msikubali kutumiwa na chama hiki hakina nia njema na ninyi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti nimalizie kwa kuwaomba wanaharakati wanaopotosha, wanaotumiwa na viongozi wanasheria maarufu sijui, ambao wanapotosha kudhani kwamba sasa hivi tupo kwenye kuandaa Katiba, nawaomba mimi nimetumwa na wanawake wa Mkao wa Pwani, na wao tena wanasema tunakutegemea wewe Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa nne tulipewa kila mmoja nakala ya Muswada turudi Majimboni kwetu, turudi Mikoani kwetu tukaongee na wananchi wetu, CHADEMA hawakufanya hiyo kazi ndiyo maana leo hapa hawapo, kwa hiyo sisi tunawaomba Watanzania, tulipewa dhamana na sisi wengine mliuona tulivaelewesha, kazi hiyo tulifanya, kuwasilishwa kwa mara ya pili ndiyo sahihi na tuendelee na Serikali msirudi nyuma mwendo mdundo na hatua za kisheria zichukuliwe hakuna cha kuandamana, hakuna nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, na mimi nianze kwa kuishukuru Serikali na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa nafasi ambayo kwa ujumla wake haijawahi kutokea, ni historia kwa Bunge letu na ni historia kwa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kuzungumza juu ya mchango wangu napenda nirudie kusoma tafsiri ya neno Katiba. Katiba maana yake ni sheria ya msingi ilioandikwa au isiyoandikwa ambayo inaweka mfumo wa Taifa kwa kuainisha misingi ya Taifa ambayo jamii italazimika kuifuata, mgawanyo wa madaraka na majukumu ya mihimili mikuu ya dola kwa kuainisha muundo wa Serikali, Bunge na Mahakama. Usimamizi wake, mgawanyo na ukomo wa mamlaka ya vyombo mbalimbali vya dola na kwa kuainisha namna na taratibu za utekelezaji wa mamlaka yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaisoma hii kwa sababu tulikotoka ni historia, ni muhimu na si sawasawa kudharau kule tulikotoka kwa sababu tuna mifano ya nchi ambazo zimeendelea kuenzi Katiba zao zilizotungwa kwenye miaka ya 1600 kwa mfano *Suri San Marino, United State of America* yenye Katiba yao ni ya mwaka 1788, Norway ya mwaka 1814 na Belgium ni ya mwaka 1831. Hii inaonesha namna ambavyo Katiba zilivyoishi kwa miaka chungu mzima zikifanyiwa mabadiliko kwa kukua na kuheshimu kule walikotoka kwa kuenzi na kuhakikisha kwamba wanaboresha na siyo kudharau moja kwa moja na kupinga kile kilichopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si sawasawa kupinga na kudharau Katiba ambayo sasa iko hai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi ni yule ambaye pamoja na changamoto zote zilizopo mbele yake katika kutekeleza majukumu yake anakuwa na uwezo wa kukabiliana nazo na siyo yule mwenye kuzikimbia, Watanzania tunashuhudia sasa viongozi tuliovapa madaraka wanakimbia changamoto zilizombele yao badala ya kuzikabili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni udhaifu na inaonesha dharau kwa wale ambao wametupa madaraka hayo na kutuamini. Bunge la Jamhuri ya Muungano la Tanzania kazi yake mojawapo ni kutunga sheria na Muswada uliopo mbele yetu ni kutunga sheria na kwa maana hiyo, pamoja na heshima ya Rais, lakini tunachokifanya sasa ni kuwa na Tume ambayo itakwenda sasa kwa

wananchi kukusanya maoni yao yanayohusu mchakato mzima wa kuelekea kupata Katiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki kimo kwa mujibu wa sheria na sisi tuliosimama hapa ndiyo tunaowawakilisha Watanzania, siyo sawasawa Mbunge mmoja kusimama akasema Watanzania wanasema, aliwauliza lini? Kama ni uwakilishi inawezekana kabisa akazungumzia Jimboni kwake alikotoka, kama hivyo maana yake ametumia mbini fulani inawezekana alitumia mtandao wa kisasa akapata taarifa juu ya maoni ya wananchi kwenye Jimbo lake na hivyo akazungumzia juu ya uwakilishi wa eneo anakotoka lakini ni lazima tuheshimu uwakilishi wa Wabunge wengine waliopo humu ndani katika tafsiri si sawasawa kusema Watanzania wanasema isipokuwa useme Jimbo fulani wanasema au useme wewe Mbunge fulani unasema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau naomba nizungumzie yaliyomo katika sheria hii ile Ibara ya 23 na Ibara ya 24 na nikiomba kufanyike mabadiliko katika kile kipengele cha tatu kiondolewe ili ile Ibara ya 23(2) kifanye kazi hiyo ya kipengele kile cha tatu. Naomba nisome, kwenye mamlaka ya Bunge la Katiba kipengele cha pili kinasema mamlaka ya Bunge la Katiba, kutunga masharti ya Katiba yatakelezwa kupitia Muswada utakaowasilishwa na Waziri na kupitishwa na Bunge la Katiba.

Kipengele cha tatu katika Ibara ya 24 inazungumzia ili masharti ya Muswada wa Katiba yapate kupitishwa katika Bunge la Katiba yatahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge la Katiba kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge la Katiba kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele hiki naomba kirudishwe kwenye *paragraph* ya pili ili Bunge hilo la Katiba liwe na mamlaka na iweze kutunga Kanuni zake za kuweza kupitisha namna ambavyo watapitisha rasimu hiyo ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuyazungumzia hayo nisingependa kurudia yale ambayo wenzangu wameanza kuyazungumzia katika upande wa namna ambavyo chama cha CHADEMA kilivyoonesha kwenye Bunge letu, lakini niunge mkono hoja na nimalizie kwa kuwashawishi wananchi kwa kufahamu kwamba tulipo sasa tunachokifanya ni kuunda Tume, Tume ambayo itarudi huko kwa wananchi, itaandaa utaratibu wa kuwafahamisha wananchi, itaandaa utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi, itaandaa taratibu za kuweza kuyaainisha na kuyaandika na baadaye yatapata mchakato wa pili kuingia katika Bunge la Katiba, lakini mwisho wa siku kitakachofika kabla ya kusema sasa Katiba tuliyokuwa nayo inakufa ni baada ya wananchi kukubali au kukataa rasimu ya Katiba ambayo itakuwa imeshapitishwa au baada ya kuwa imeshapitishwa na Bunge letu la Katiba litakapokuwa limeundwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Watanzania wanaelewa haya na sasa hivi wanaelewa kwamba tunachokijadili siyo Katiba, imeshangaza hata juzi nilikuwa nikisoma gazeti moja Chama kimoja cha Wafanyakazi wanasema kwamba wao hawajawekwa mle ndani, Katiba hiyo siyo halali, sasa hivi wananchi tunachokizungumzia ni uundwaji wa Tume na siyo Katiba, yaliyomo kwenye Katiba yatakuja kupata muafaka na muda wake wa kujadiliwa, na ninaamini kwamba Tume itakayoteuliwa na Rais na mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Katiba itafanyakazi na itahakikisha kwamba wale watakaotoka wataweza kutoa ulinganifu mzuri wa maeneo ya kijiografia, taaluma yao na uwezo wao wa uwakilishi katika nchi nzima kama tulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, msemaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Munde Tambwe, una dakika kumi.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia suala hili kubwa la kihistoria ndani ya nchi yetu. Pia nampongeza Waziri wa Katiba, naipongeza Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala lakini nichukue fursa ya pekee kumpongeza Rais Jakaya Kikwete kwa kukubali kuweka mchakato

wa Katiba Mpya. Ninaamini ametumia busara, hekima kwa uamuzi mkubwa alioufikia kwa kutaka Watanzania tupate Katiba Mpya katika miaka yetu 50 ya Uhuru, tunampongeza sana Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba niongee na wananchi wangu wa Tabora, niwaambie kwamba ninawaheshimu sana, ninathamini uwezo wao walionipa wa kuja hapa Bungeni kuwawakilisha na niwaambie kabisa sitoweza hata siku moja kutoka nje ya Bunge, hata kama Muswada huo siuafiki nitakaa humu ndani niweze kupambana, niweke yale ninayoyahitaji mimi na siyo kutoka nje ya Bunge, kwa kufanya hivyo nitakuwa siwatendei haki wananchi wa Tabora walionichangua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa Muswada wa kuunda Tume ili kuwezesha upatikanaji wa Katiba Mpya. Kwenye Muswada huu tumeona mambo mbalimbali lakini jambo kubwa tumeona madaraka aliopewa Rais. Ukienda kwenye kifungu cha 5 utaona Rais amepewa mamlaka ya uteuzi, Kifungu cha 6 atateua Wajumbe wa Tume, amepewa mamlaka mbalimbali lakini suala hili napata shida kidogo kwa wananchi ambao wanapotoshwa kuambiwa kwamba Rais ana mamlaka makubwa sana kwa hiyo apunguziwe mamlaka hayo. Kwa kweli Watanzania wenzangu mnapotoshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 33 na 34 Rais anayo mamlaka kama Mkuu wa nchi. Kwa hiyo, ana haki zote za kufanya hivyo aliyowekewa katika Muswada huu. Vilevile niwaambie tu Watanzania sisi siyo wa kwanza jambo hili limefanyika Kenya, Zambia, Ghana na Katiba Mpya ikapatikana. Kwa hiyo, tulichofanya sisi siyo geni sana wamefanya Waafrika wengine na limeleta matunda mazuri. Kwa hiyo, mimi naamini kabisa mamlaka aliyonayo Rais ni mamlaka aliopewa Kikatiba na hakuna mtu mwingine yeoyote aliyempa ni sheria imempa mamlaka hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashangaa kumwambia Rais ana mamlaka makubwa kama Mkuu wa nchi kuteua Tume na mambo mengine aliopewa kwenye Muswada huu, lakini hawashangai kwamba Rais ndiye aliyetamka kukubali kwamba tuunde Katiba mpya, nashangaa kwanini hawakuhoji kwanini anatamka tuunde Katiba mpya, walifurahi na wakalipokea vizuri. Lakini niwaambie tu Watanzania wenzangu tusikubali kabisa kupotoshwa, tusikubali kudanganyika, huu mchakato ndiyo utakaotuletea sisi Watanzania kusema kero zetu zote tulizonazo, baada ya kuundwa kwa Tume Watanzania tutapewa nafasi ya kutoa maoni yetu. Kila mtanzania atatoa maoni yake Tume itachukua kero hizi na kuleta ndani ya Bunge la Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli napata taabu kuona kwamba kuna watu wanasesma vitu hivi vitachakachuliwa, kwa sababu katika hilo Waheshimiwa Wabunge wote tutakuwemo mle ndani na tutatoa maoni yetu na tutachangia kila kitu kitakacholetwa na Tume mle ndani ya Bunge la Katiba. Napata taabu kuona kwamba kuna watu wanasesma vitu vitachakachuliwa na wenyewe watakuwemo humo humo, mimi nawaomba Watanzania tusikubali kudanganywa, nchi yetu ni ya kidemokrasia itaunda Bunge ambalo Wabunge wote wanaowawakilisha ninyi lakini itachukua pia watu kutoka taasisi mbalimbali ili kuleta uwiano, usawa na kupata kile kitu ambacho Watanzania wanakihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wa nchi anayo mamlaka ya kufanya haya yote ambayo anayafanya ambayo wenzetu wamekuwa wanayaona kama ni jambo sasa la kuwashawishi Watanzania, ni kitu ambacho hakiwezekani ile ni Katiba hamna mtu yeoyote anayeweza kukiuka Katiba na sasa hivi bado tunatumia Katiba ile ile ambayo huyu ni Mkuu wa nchi na anayo mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mdogo tu wakati tunaingia kwenye mfumo wa vyama vingi tulipiga kura za maoni, Watanzania karibu asilimia 80 walikataa mfumo wa vyama vingi, asilimia 20 ndiyo walikubali mfumo wa vyama vingi, lakini kwa uwepo wa Katiba hiyo hiyo mkuu wa nchi alikubali kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi, ingawa asilimia 80 ya Watanzania walikataa, lakini nashangaa leo hawatambui umuhimu wa nchi. Kwa kweli watu hawa mimi ninawashangaa sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa moja kwa moja kwenye suala zima la kazi ya Tume, inaanisha misingi mikuu ya Kitaifa ambayo Wajumbe wa Tume wazingatie pindi watakapokuwa wanatekeleza majukumu. Kwa mfano uwepo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, suala kama hili la Muungano wa Tanzania ni suala ambalo haliepukiki, naomba niseme kabisa Watanzania huko tunakotoa maoni yetu sisi Wabunge tuwaelimishe wananchi kabisa kuhusu Muungano wa Tanzania. Ni lazima tuienzi mifumo yetu mizuri, ni lazima tuienzi amani yetu na utulivu tulionao. Tusikubali kabisa kupoteza amani hii, tusikubali kabisa kwa sababu za watu binafsi, kwa *interest* zao kwa maslahi yao, kupoteza amani tuliyonayo Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna fununu za kinafiki kwamba kuna makatazo ya wananchi wasitoe maoni kuhusu kujadili Muungano. Siyo kweli! Wananchi wamepewa uhuru wa kutoa maoni yao, wamepewa fursa ya kutoa maoni yao ili kuboresha suala zima la Muungano wa Jamhuri ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukemee vitendo ambavyo vinasababisha mmomonyoko wa maadili, vitendo ambavyo vinachochea vurugu kwa Watanzania. Mijadala inayoendelea huko nje kwa kweli ni mijadala ambayo itatusababishia vurugu kubwa, mimi nashukuru tumejadili kwa siku tatu, ninaamini Watanzania wengi wataona, Watanzania wengi sasa wataelewa na watapembua pumba ni zipi na mchele ni upi tofauti na walivyokuwa wanadanganywa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mdahalo wa Jumapili pale *ITV*, kwa kweli ilikuwa ni uongo mkubwa na upotoshaji mkubwa, kwa kweli tunaomba Serikali ichukue hatua, kufanya hivyo ni kuhatirisha amani ya nchi yetu na utulivu tulionao. Mimi naomba niulize hawa watu Jukwaa la Katiba walisajiliwa lini na kwa sheria zipi? Limesajiliwa kwa malengo yapi? Kwa lengo la kuhamasisha maandamano, kwa lengo la kuwafundisha Watanzania, kwa lengo la kuwatia moyo Watanzania, mimi naomba kuelewa maana tumepewa siku 30 maandamano hayataisha, yataendelea milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kabisa watu wa namna hii Serikali itoe tamko la kulaani mambo yao wanayoyafanya, tamko la kulaani uchochezi wao na kukomesha kabisa uchochezi wa aina hiyo. Serikali yetu inatoa fursa ya kutoa maoni ninaamini watu hao watakuwa na nafasi ya kutoa maoni yao na maoni yao yataingizwa kwenye Bunge. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge kwanza nawapongeza sana kwa namna mlivyoshiriki mjadala wetu, kabla ya kuahirisha naomba niwataje ambaao kesho asubuhi baada ya kipindi cha maswali na majibu wataendelea. Tutakuwa na Mheshimiwa Suleiman Jafo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Said Mtanda na wengine watatajwa kwa kadri muda utakavyokuwa unaruhusu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya naomba kuahirisha shughuli zote kwa siku hii ya leo hadi kesho saa tatu asubuhi. Ahsanteni. (*Makofii*)

(*Saa 1.43 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
Tarehe 16 Novemba, 2011 saa tatu asubuhi*)

